# KANUSHO / DISCLAIMER

Tafsiri hii ya Kiswahili ya Katiba ya Kenya imetolewa ili kukusaidia kuelewa Katiba. Nakala rasmi ya Katiba ya Kenya (2010) imechapishwa kwa Kiingereza na Baraza la Kitaifa la Kuripoti Sheria (Kenya Law).

Tafsiri hii imetayarishwa na kurejelea vyanzo rasmi kwa kadiri ya uwezo wetu, lakini si rasmi. Iwapo kuna tofauti yoyote kati ya tafsiri hii na nakala rasmi ya Kiingereza, nakala rasmi ya Kiingereza ndiyo yenye nguvu. Hii si ushauri wa kisheria.

Official notice: The official Constitution of Kenya is published in English by Kenya Law. This Kiswahili document is an unofficial translation provided to help you understand the Constitution. It has been prepared with reference to official sources to the best of our knowledge, but it is not official. If there is any difference, the official English text prevails. This is not legal advice.

Chanzo / Source: KenyaSimplified — kenyasimplified.org

**JAMHURI YA KENYA**

# KATIBA INAYOPENDEKEZWA YA KENYA

**Mei 6, 2010**

Draft for approval

**Imechapishwa na Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa Sehemu ya 34 ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya (Na. 9 ya 2008)**

Draft for approval

**UTANGULIZI**

**SURA YA KWANZA**

**MAMLAKA YA WANANCHI NA UKUU WA KATIBA HII**

1. Mamlaka ya Wananchi
2. Ukuu wa Katiba hii
3. Kuilinda Katiba hii

**SURA YA PILI**

**JAMHURI**

4. Kutangaza Jamhuri
5. Eneo la Kenya
6. Ugatuzi na kufikia huduma
7. Lugha ya taifa, lugha rasmi na lugha nyingine
8. Nchi na dini
9. Nembo za Kitaifa na siku za kitaifa
10. Maadili ya kitaifa na kanuni za utawala
11. Utamaduni

**SURA YA TATU**

**URAIA**

12. Haki za raia
13. Kupata na Kudumisha Uraia
14. Uraia kwa kuzaliwa
15. Uraia kwa kujiandikisha
16. Uraia mara mbili
17. Kupokonywa Uraia
18. Sheria kuhusu Uraia

Draft for approval

**SURA YA NNE**

**SHERIA YA HAKI**

**Sehemu ya 1- Masharti ya jumla kuhusiana na Sheria ya Haki**

19. Haki na uhuru wa kimsingi
20. Utekelezaji wa Sheria ya Haki
21. Utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi
22. Utekelezaji wa Sheria ya Haki
23. Mamlaka ya mahakama kudumisha na kutekeleza Sheria ya Haki
24. Mipaka ya haki na uhuru wa kimsingi
25. Haki na Uhuru usioweza kuwekewa Mipaka

**Sehemu ya 2- Haki na uhuru wa kimsingi**

26. Haki ya kuishi
27. Usawa na Uhuru dhidi ya kubaguliwa
28. Hadhi ya Binadamu
29. Uhuru na usalama wa mtu
30. Utumwa na kazi ya kulazimishwa
31. Faragha
32. Uhuru wa dhamiri, dini, imani na maoni
33. Uhuru wa kujieleza
34. Uhuru wa vyombo vya habari
35. Upataji habari
36. Uhuru wa kutangamana
37. Mikutano, maandamano, migomo na malalamiko
38. Haki za kisiasa
39. Uhuru wa kwenda popote na makaazi
40. Ulinzi wa haki ya kumiliki mali
41. Mahusiano ya kikazi

Draft for approval

42. Mazingira

43. Haki za kiuchumi na kijamii

44. Lugha na Utamaduni

45. Familia

46. Haki za Watumiaji wa Bidhaa

47. Hatua ya Haki za Kiutawala

48. Uwezo wa kufikia Haki

49. Haki za waliotiwa mbaroni

50. Haki katika kusikizwa kwa kesi

51. Haki za walio kizuizini, walioshikwa ama waliofungwa

**Sehemu ya 3 -Utekelezaji mahususi wa Haki**

52. Ufafanuzi wa sehemu hii

53. Watoto

54. Watu wenye ulemavu

55. Vijana

56. Makundi  yaliyotengwa na kubaguliwa

57. Wazee katika jamii

**Sehemu ya 4 - Hali ya Hatari**

58. Hali ya hatari

**Sehemu ya 5- Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa**

59. Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa

Draft for approval

**SURA YA TANO**

**ARDHI NA MAZINGIRA**

**Sehemu ya 1-Ardhi**

60. Kanuni za sera ya ardhi

61. Uainishaji wa ardhi

62. Ardhi ya umma

63. Ardhi ya jamii

64. Ardhi ya kibinafsi

65. Umilikaji Ardhi wa wasio raia

66. Kanuni za matumizi ya ardhi na mali

67. Tume ya Kitaifa ya Ardhi

68. Sheria kuhusu Ardhi

**Sehemu ya 2-Mazingira na Maliasili**

69. Kanuni na wajibu kuhusiana na mazingira

70. Utekelezwaji wa haki za mazingira

71. Makubaliano kuhusiana na maliasili

72. Sheria kuhusu Mazingira

**SURA YA SITA**

**UONGOZI NA MAADILI**

73. Majukumu ya uongozi

74. Kiapo cha uaminifu kwa Maafisa wa Serikali

75. Mienendo ya Maafisa wa Serikali

76. Uadilifu wa kifedha kwa Maafisa wa Serikali

77. Vizuizi katika shughuli za Maafisa wa Serikali

78. Uraia na uongozi

79. Sheria ya kuundwa kwa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi

Draft for approval

80. Sheria kuhusu uongozi

**SURA YA SABA**

**UWAKILISHAJI WATU**

**Sehemu ya 1 – Mfumo na utaratibu wa uchaguzi**

81. Kanuni za jumla za mfumo wa uchaguzi
82. Sheria kuhusu uchaguzi
83. Kusajiliwa kama mpiga kura
84. Wagombea uchaguzi na vyama vya kisiasa kuzingatia kanuni za upigaji kura
85. Ustahili wa kusimama kama mgombea wa kibinafsi
86. Upigaji kura
87. Mizozo ya Uchaguzi

**Sehemu ya 2- Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka**

88. Tume Huru ya uchaguzi na Mipaka
89. Kuwekea mipaka maeneo ya uchaguzi
90. Ugawaji orodha ya viti vya chama

**Sehemu ya 3- Vyama vya kisiasa**

91. Kanuni za kimsingi kwa vyama vya kisiasa
92. Sheria ya vyama vya kisiasa

**SURA YA NANE**

**BUNGE**

**Sehemu ya 1 – Kuundwa na jukumu la Bunge**

93. Kuundwa kwa Bunge
94. Jukumu la Bunge
95. Jukumu la Baraza Kuu la Kitaifa

Draft for approval

96. Jukumu la Seneti

**Sehemu ya 2 – Uhusika na uanachama wa Bunge**

97. Uanachama wa Baraza la Kitaifa

98. Uanachama wa Seneti

99. Sifa za kufaa na kutofaa katika kuchaguliwa kama mbunge

100. Kukuza uwakilishi wa makundi yaliyotengwa

101. Uchaguzi wa wabunge

102. Muhula wa Bunge

103. Kuondoka afisini kwa Mbunge

104. Haki ya kumwondoa mamlakani mbunge

105. Kutathmini maswali kuhusu ubunge

**Sehemu ya 3- Afisi za Bunge**

106. Maspika na Manaibu Spika wa Bunge

107. Kuongoza vikao Bungeni

108. Viongozi wa Vyama

**Sehemu ya 4 – Taratibu za Kutunga sheria Bungeni**

109. Matumizi ya Mamlaka ya kutunga sheria

110. Miswada kuhusu Serikali za Kaunti

111. Miswada maalum inayohusu Serikali za Kaunti

112. Miswada ya kawaida inayohusu serikali za Kaunti

113. Kamati za Upatanishi

114. Miswada ya Fedha

115. Idhini ya Rais na Urejeshaji

116. Kutekelezeka kwa sheria

Draft for approval

**Sehemu ya 5- Taratibu za jumla na Sheria za Bunge**

117. Mamlaka, haki na kinga za Bunge
118. Kufikiwa na kushiriki kwa umma
119. Haki ya kulalamikia Bunge
120. Lugha rasmi za Bunge
121. Idadi ya wabunge katika vikao
122. Kupiga kura Bungeni
123. Maamuzi ya Seneti
124. Kamati na Kanuni kuendesha Bunge
125. Uwezo wa kuitisha ushahidi

**Sehemu ya 6 – Vipengele vya Ziada**

126. Eneo la vikao vya Bunge
127. Tume ya Huduma za Bunge
128. Makarani na wafanyikazi wa Bunge

**SURA YA TISA**

**MAMLAKA KUU YA SERIKALI**

**Sehemu ya 1- Kanuni na muundo wa Mamlaka Kuu ya Kitaifa**

129. Kanuni za mamlaka kuu
130. Mamlaka kuu ya Kitaifa

**Sehemu ya 2- Rais na Naibu wa Rais**

131. Mamlaka ya Rais
132. Majukumu ya Rais
133. Mamlaka ya huruma ya Rais
134. Matumizi ya mamlaka ya Urais kwa Rais wa muda
135. Maamuzi ya Rais

Draft for approval

136. Uchaguzi wa Rais

137. Sifa za kimsingi za kuchaguliwa na kutochaguliwa kwa Rais

138. Taratibu katika Uchaguzi wa Rais

139. Kifo kabla ya kuchukua hatamu

140. Maswali kuhusu uhalali wa uchaguzi wa Urais

141. Kuchukua hatamu za Urais

142. Muhula wa Afisi ya Rais

143. Kulindwa dhidi ya kufunguliwa mashtaka.

144. Kuondolewa kwa Rais kwa misingi ya kukosa uwezo

145. Kuondolewa kwa Rais kupitia kwa kura ya kutokuwa na imani

146. Nafasi ya kazi katika afisi ya Rais

147. Majukumu ya Naibu wa Rais

148. Kuchaguliwa na Kuapishwa kwa Naibu wa Rais

149. Nafasi ya kazi katika afisi ya Naibu wa Rais

150. Kuondolewa kwa Naibu wa Rais

151. Malipo na marupurupu ya Rais na Naibu wa Rais

**Sehemu ya 3- Baraza la Mawaziri**

152. Baraza la Mawaziri

153. Maamuzi, majukumu na kuwajibika kwa Baraza la Mawaziri

154. Katibu wa Baraza la Mawaziri

155. Makatibu Wakuu

**Sehemu ya 4- Afisi nyinginezo**

156. Mwanasheria Mkuu

157. Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma

158. Kuondolewa na kujiuzulu kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma

Draft for approval

**SURA YA KUMI**

**MAHAKAMA**

**Sehemu ya 1 – Mamlaka ya Mahakama na mfumo wa kisheria**

159. Mamlaka ya Mahakama

160. Uhuru wa Mahakama

161. Afisi na maafisa wa Mahakama

162. Mfumo wa Mahakama

**Sehemu ya 2- Mahakama za Mamlaka Kuu**

163. Mahakama ya Juu

164. Mahakama ya Rufani

165. Mahakama Kuu

166. Uteuzi wa Jaji Mkuu, Naibu wa Jaji Mkuu na Majaji Wengine

167. Kipindi cha kuhudumu afisini kwa Jaji Mkuu na majaji wengine

168. Kuondolewa kutoka afisini

**Sehemu ya 3 -Mahakama Ndogo**

169. Mahakama Ndogo

170. Mahakama za Kadhi

**Sehemu ya 4 – Tume ya Huduma za Mahakama**

171. Kuundwa kwa Tume ya Huduma za Mahakama

172. Majukumu ya Tume ya Huduma za Mahakama

173. Hazina ya Mahakama

Draft for approval

**SURA YA KUMI NA MOJA**

**SERIKALI YA UGATUZI**

**Sehemu ya 1- Malengo na kanuni za Serikali ya Ugatuzi**

174. Malengo ya ugatuzi

175. Kanuni za Serikali za ugatuzi

**Sehemu ya 2 – Serikali za Kaunti**

176. Serikali za kaunti

177. Wanachama wa Baraza la kaunti

178. Spika wa Baraza la kaunti

179. Kamati za mamlaka kuu za kaunti

180. Uchaguzi wa gavana wa kaunti na naibu wa gavana wa kaunti

181. Kuondolewa kwa gavana wa kaunti

182.Nafasi katika afisi ya gavana wa kaunti

183. Majukumu ya mamlaka kuu za kaunti

184. Maeneo ya miji na majiji

185. Mamlaka ya kisheria ya mabaraza ya kaunti

**Sehemu ya 3 – Mamlaka na shughuli za Serikali za Kaunti**

186. Mamlaka na majukumu ya serikali za kaunti na kitaifa

187. Kuhamisha mamlaka na majukumu kati ya viwango vya serikali

**Sehemu ya 4 – Mipaka ya kaunti**

188. Mipaka ya kaunti

**Sehemu ya 5 – Mahusiano katika Serikali**

189. Ushirikiano kati ya serikali ya kitaifa na za kaunti

190. Usaidizi kwa serikali za kaunti

191. Mkinzano ya sheria

Draft for approval

**Sehemu ya 6 – Kusimamishwa kwa muda kwa Serikali za kaunti**

192. Kusimamishwa kwa muda kwa Serikali ya kaunti

**Sehemu ya 7 – Jumla**

193. Sifa za wagombea uanachama wa baraza la kaunti
194. Kuondoka afisini kama mwanachama wa baraza la kaunti
195. Uwezo wa baraza la kaunti kuita mashahidi
196. Kushiriki kwa umma, mamlaka, haki na kinga kwa baraza la kaunti
197. Usawa na tofauti za kijinsia katika baraza la kaunti
198. Serikali ya kaunti katika kipindi cha mpito
199. Kuchapishwa kwa sheria za kaunti
200. Sheria kuhusu sura hii

**SURA YA KUMI NA MBILI**

**FEDHA ZA UMMA**

**Sehemu ya- 1 Kanuni na utaratibu wa fedha za umma**

201. Kanuni za fedha za umma
202. Mgawo unaolingana wa mapato ya kitaifa
203. Ugavi sawa na sheria nyingine za kifedha
204. Hazina ya Usawazishaji
205. Mashauriano kuhusu sheria za kifedha zinazoathiri kaunti

**Sehemu ya 2- Fedha zingine za umma**

206. Mfuko wa Jumla na fedha zingine za umma
207. Hazina za mapato za serikali za kaunti
208. Hazina ya Dharura

Draft for approval

**Sehemu ya 3- Nguvu za kuzalisha mapato na deni la umma**

209. Mamlaka ya kutoza kodi na ushuru

210. Kutoza ushuru

211. Ukopaji wa serikali ya kitaifa

212. Ukopaji wa kaunti

213. Udhamini wa Mikopo na serikali ya kitaifa

214. Deni la Umma

**Sehemu ya 4- Ugavi wa mapato**

215. Tume ya ugavi wa mapato

216. Majukumu ya Tume ya Ugavi wa Mapato

217. Ugavi wa mapato

218. Miswada ya ugavi wa kila mwaka wa mapato

219. Uhamishaji wa ugavi sawa

**Sehemu ya 5- Bajeti na matumizi**

220. Umbo, yaliyomo na wakati wa bajeti

221. Mswada wa Makadirio ya Bajeti na Matumizi ya Mwaka

222. Matumizi kabla ya kuidhinishwa kwa bajeti ya kila mwaka

223. Matumizi ya ziada

224. Miswada ya Matumizi ya Fedha za Kaunti

**Sehemu ya 6- Udhibiti wa fedha za umma**

225. Udhibiti wa fedha

226. Akaunti na ukaguzi wa mashirika ya umma

227. Ununuzi wa bidhaa na huduma za umma

**Sehemu ya 7- Maafisa wa kifedha na taasisi**

Draft for approval

228. Msimamizi wa  Bajeti

229. Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu

230. Tume ya Mishahara na Kuzawidi

231. Benki Kuu Ya Kenya

**SURA YA KUMI NA TATU**

**HUDUMA ZA UMMA**

**Sehemu ya 1 – Maadili na kanuni za  huduma kwa umma**

232. Maadili  na kanuni za  huduma kwa umma

**Sehemu ya 2- Tume ya Huduma za Umma**

233. Tume ya Huduma za Umma

234. Mamlaka na Majukumu ya Tume ya Huduma za Umma

235. Kuajiri wafanyakazi wa serikali za kaunti

236. Kuwalinda wafanyikazi wa umma

**Sehemu ya 3 – Tume ya Kuwaajiri Walimu**

237. Tume ya Kuwaajiri Walimu

**SURA YA KUMI NA NNE**

**USALAMA WA KITAIFA**

**Sehemu ya 1- Idara za Usalama wa Taifa**

238. Kanuni za usalama wa taifa

239. Idara za usalama wa Taifa

240. Kuundwa kwa Baraza la Usalama wa Taifa

**Sehemu ya 2 - Majeshi ya Ulinzi wa Kenya**

241. Kuundwa kwa Vikosi vya Ulinzi wa Kenya na Baraza la Ulinzi

Draft for approval

**Sehemu ya 3 – Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa**

242. Kuundwa kwa Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa

**Sehemu ya 4 – Huduma za Polisi za Kenya**

243. Kuundwa kwa Huduma za Polisi za Kenya

244. Malengo na Majukumu ya Huduma za Polisi za Kenya

245. Amri katika Huduma za Polisi za Kenya

246. Tume ya Huduma za Polisi za Kenya

247. Huduma nyingine za polisi

**SURA YA KUMI NA TANO**

**TUME NA AFISI HURU**

248. Utekelezaji wa Sura

249. Malengo, mamlaka na ufadhili wa Tume na afisi huru

250. Muundo, uteuzi na masharti ya afisi

251. Kuondolewa kutoka afisini

252. Wajibu wa jumla na mamlaka

253. Ushirikishwaji wa Tume na afisi huru

254. Kuripoti kwa Tume na afisi huru

**SURA YA KUMI NA SITA**

**MAREKEBISHO YA KATIBA HII**

255. Marekebisho ya Katiba hii

256. Marekebisho yatakayopendekezwa na Bunge

257. Marekebisho yatakayopendekezwa na jihudi za wengi

**SURA YA KUMI NA SABA**

**MASHARTI YA JUMLA**

Draft for approval

258. Utekelezaji wa Katiba hii

259. Kufasiri Katiba hii

260. Ufasiri

**SURA YA KUMI NA NANE**

**MASHARTI YA MPITO NA MATOKEO**

261. Sheria zinazohuasiana na Matokeo

262. Masharti ya Mpito na matokeo

263. Tarehe ya kutekelezwa

264. Kutotumika kwa Katiba ya awali

**MIPANGILIO**

**MPANGILIO WA KWANZA:** Kaunti
**MPANGILIO WA PILI :** Nembo za Kitaifa
**MPANGILIO WA TATU:** Viapo vya Kitaifa na Uthibitisho
**MPANGILIO WA NNE:** Mgao wa Majukumu kati ya Serikali ya Kitaifa na Serikali za kaunti
**MPANGILIO WA TANO:** Sheria kutungwa na Bunge
**MPANGILIO WA SITA:** Masharti ya Mpito na Matokeo

Draft for approval

**UTANGULIZI**

**Sisi watu wa Kenya,**

**TUKITAMBUA** utukufu wa Mungu Muumba wa vyote:

**TUKIWAHESHIMU** mashujaa wetu waliojitoa mhanga kupigania uhuru na haki nchini mwetu-

**TUKIJIVUNIA** tofauti zetu za kikabila, kitamaduni na kidini na kuazimia kuishi kwa amani na umoja tukiwa taifa moja huru-

**TUKITHAMINI** mazingira yetu ambayo ndiyo turathi yetu na kuazimia kuyadumisha kwa manufaa ya vizazi vijavyo-

**TUKIJITOLEA** kukuza na kuhifadhi maslahi ya watu binafsi, familia, jamii na taifa-

**TUKITAMBUA** matarajio ya Wakenya wote kwa Serikali iliyo na misingi bora ya haki za binadamu, usawa, demokrasia, haki za kijamii na utawala wa kisheria-

**TUKITUMIA** uhuru wetu na haki yetu ya kuamua aina ya uongozi tunaotaka na tukiwa tumeshiriki kikamilifu katika kuiunda Katiba hii-

**TUNAKUBALI,** kutekeleza, na kujipatia sisi wenyewe na vizazi vijavyo, Katiba hii.

**MUNGU IBARIKI KENYA**

Draft for approval

## SURA YA KWANZA

## MAMLAKA YA WANANCHI NA UKUU WA KATIBA HII

### Mamlaka ya wananchi

**1.** (1) Mamlaka yote makuu ni ya wananchi wa Kenya na yanaweza kutekelezwa tu kulingana na Katiba hii.

(2) Wananchi watatekeleza mamlaka yao kwa njia ya moja kwa moja au kupitia kwawawakilishi wao waliochaguliwa kidemokrasia.

(3) Mamlaka ya wananchi katika Katiba hii yamepewa idara zifuatazo za Serikali, ambazo zitatekeleza majukumu yao kulingana na Katiba hii –

(a) Bunge na mabaraza ya kutunga sheria katika Serikali za Kaunti;

(b) Serikali ya kitaifa na mifumo ya Serikali za Kaunti; na

(c) Idara ya mahakama na tume zingine huru ;

(4) mamlaka ya wananchi yanatekelezwa katika-

(a) kiwango cha kitaifa; na

(b) kiwango cha kaunti.

### Ukuu wa Katiba hii

**2.** (1) Katiba hii ni sheria kuu ya Jamhuri na inaunganisha asasi zote za nchi katika viwango vyote viwili vya Serikali na watu wote.

(2) Hakuna mtu anayeweza kudai au kutumia mamlaka ya Taifa ila tu kwa idhini ya Katiba hii.

(3) Uhalali au uthabiti wa Katiba hii hauwezi kupingwa na mahakama yoyote au idara yoyote ya Serikali.

(4) Sheria yoyote, ikiwemo sheria ya mila na tamaduni, ambayo haiambatani na Katiba hii ni batili na kiwango cha ukinzani huo pamoja na kitendo chochote au utendaji unaopingana na Katiba hii si halali.

(5) Sheria za jumla za kimataifa zitakuwa sehemu ya sheria za Kenya.

(6) Mkataba au maagano yoyote ambayo yataidhinishwa na Kenya yatakuwa sehemu ya sheria za Kenya chini ya Katiba hii.

### Kuilinda Katiba Hii

**3**. (1) Kila mtu ana jukumu la kuiheshimu, kuitetea na kuilinda Katiba hii.

(2) Jaribio lolote la kubuni Serikali bila kufuata Katiba hii ni kinyume cha sheria.

Draft for approval

## SURA YA PILI

## JAMHURI

**Kutangaza Jamhuri**

4. (1) Kenya ni Jamhuri huru.

(2) Jamhuri ya Kenya itakuwa Taifa la demokrasia ya vyama vingi lililobuniwa kwa misingi ya maadili ya kitaifa na kanuni za uongozi kama ilivyotajwa katika Kifungu cha 10.

**Eneo la Kenya**

**5.** Eneo la Jamhuri ya Kenya ni lile la nchi na maji ya Taifa la Kenya katika tarehe ya kuanza kutekelezwa, na nyongeza zingine za eneo au maji kama itakavyobainishwa na sheria ya Bunge.

**Ugatuzi na Kufikia Huduma**

**6**. (1) Eneo la Kenya limegawanywa katika kaunti zilizotajwa katika Mpangilio wa Kwanza.

(2) Serikali katika viwango vya kitaifa na kaunti ni tofauti na zinategemeana na

Zitaendesha mahusiano yao ya uelewanaji kwa misingi ya mashauriano na ushirikiano.

(3) Asasi ya Serikali ya kitaifa itahakikisha ufikiaji wa huduma zake bora katika sehemu zote za Jamhuri kwa njia inayofaa na kulingana na hali ya huduma inayotakikana

**Lugha ya Taifa, Lugha Rasmi na lugha nyingine.**

**7.** (1) Lugha ya taifa ya Jamhuri ni Kiswahili.

(2) Lugha rasmi za Jamhuri ya Kenya ni Kiswahili na Kiingereza.

(3) Serikali-

(a) Itakuza na kulinda lugha tofauti za wananchi wa Kenya; na

(b) Italinda na itastawisha matumizi ya lugha za kiasili, Lugha Ishara ya Kenya, Breli na njia nyingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu.

**Nchi na Dini**

**8.** (1) Hakutakuwa na dini ya Taifa.

Draft for approval

**Nembo za Kitaifa na siku za kitaifa**

**9.** (1) Alama za kitaifa za Jamhuri ni –

(a) bendera ya taifa;

(b) wimbo wa taifa;

(c ) nembo ya taifa; na

(d) muhuri wa Serikali

(2) Alama za kitaifa ni kama zilivyotajwa katika Mpangilio wa Pili.

(3) Siku kuu za kitaifa ni –

(a) Siku kuu ya Madaraka, kuadhimishwa Juni 1;

(b) Siku kuu ya Mashujaa, kuadhimishwa Oktoba 20; na

(c) Siku kuu ya Jamhuri, kuadhimishwa Disemba 12.

(4) Siku kuu ya kitaifa itakuwa siku ya mapumziko kote nchini.

(5) Bunge linaweza, kupitia kwa sheria, kuamua ni siku gani itakuwa ya kitaifa na kuelekeza maadhimisho yake kama siku ya mapumziko.

**Maadili ya kitaifa na kanuni za utawala**

**10.** (1) Maadili ya kitaifa, kanuni na malengo yaliyo katika Sura hii yatazingatiwa na idara mbalimbali za Serikali, watumishi wa umma na watu wote wanapo –

(a) tekeleza au kufasiri Katiba hii;

(b) tumia, tekeleza au kufasiri sheria yoyote; au

(c) tunga, au kutekeleza maamuzi kuhusu sera ya kitaifa.

(2) Maadili ya kanuni za uongozi ni pamoja na –

(a) Uzalendo, umoja wa kitaifa, kushirikiana na ugatuzi wa mamlaka, utawala wa sheria, demokrasia na kushiriki kwa watu;

(b) heshima ya binadamu, usawa, haki za jamii, kushirikishwa, haki za binadamu, kutobagua na kulindwa kwa makundi yaliyotengwa.

(c) utawala mwema, uadilifu, uwazi na uwajibikaji; na

(d) maendeleo endelevu.

**Utamaduni**

**11.** (1) Katiba hii inatambua utamaduni kama msingi wa taifa na jumla ya ustaarabu wa watu na taifa la Kenya.

(2) Serikali–

Draft for approval

(a) itakuza aina zote za kitaifa na kitamaduni za kujieleza kupitia fasihi, sanaa, sherehe za kitamaduni, sayansi, mawasiliano, habari, vyombo vya habari, uchapishaji, maktaba na turathi nyingine za kitamaduni;

(b) itatambua jukumu la sayansi na teknolojia za kiasili katika maendeleo ya nchi;

(c) itatambua haki za kiubunifu za watu wa Kenya;

(3) Bunge litatunga sheria-

(a) kuhakikisha kwamba jamii zinapewa fidia au mrabaha kwa kutumiwa kwa turathi zao za kitamaduni; na

(b) kutambua na kulinda umiliki wa mbegu na mimea mbalimbali ya kiasili, sifa tofauti za kimaumbile na matumizi yake miongoni mwa jamii za Kenya.

Draft for approval

## SURA YA TATU

## URAIA

**Haki za Raia**

**12.** (1) Kila raia -

(a) anastahiki kupata haki, fursa, na faida kwa mujibu wa Katiba hii; na
(b) ana haki ya kupata hati ya usafiri ya Kenya na hati yoyote ya usajiliwa au utambulisho unaotolewa na Serikali kwa raia wake.

(2) hati ya usafiri au hati nyingine ya usajili au utambulisho iliyotajwa katika ibara ya (1) (b), inaweza kunyimwa mtu, kusimamishwa kwa muda au kupokonywa mtu kwa mujibu wa Sheria ya Bunge ambayo inatosheleza kigezo kilichotajwa katika Kifungu cha 24.

Draft for approval

**Kudumisha uraia na Kupata Uraia**

**13.** (1) Kila mtu ambaye alikuwa raia punde tu kabla ya kuanza kutumika Katiba hii atadumisha hali ya uraia wake .

(2) Uraia unaweza kupatikana kwa kuzaliwa, au kujiandikisha .

(3) Uraia haupotezwi kwa sababu ya ndoa au kuvunjika kwa ndoa.

**Uraia kwa kuzaliwa**

**14.** (1) Kila mtu ni raia wa Kenya iwapo, wakati wa siku ya kuzaliwa kwake, iwe amezaliwa nchini Kenya au la, bora tu ikiwa mama au baba yake ni raia.

(2) Ibara ya (1) itatumika sawa kwa mtu ambaye alizaliwa kabla ya siku ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, iwe amezaliwa nchini au la, ikiwa mama au baba yake ni, au alikuwa raia.

(3) Bunge linaweza kutunga sheria kuwekea mipaka athari za ibara ya (1) na (2) kwa raia wa Kenya ambao wamezaliwa nje ya Kenya.

(4) Mtoto anayepatikana nchini Kenya ambaye anaonekana kuwa na umri wa chini ya miaka minane, na ambaye uraia wake haujulikani na pia wazazi hawajulikani, atachukuliwa kuwa raia kwa kuzaliwa.

(5) Mtu ambaye ni raia wa Kenya kwa kuzaliwa na ambaye amekoma kuwa raia kwa sababu ya kupata uraia wa nchi nyingine ana haki, kwa kutuma maombi, kurejeshewa uraia wa Kenya.

**Uraia kwa kujiandikisha**

**15.** (1) Mtu ambaye ameolewa na raia kwa muda wa angalau miaka saba ana haki, kutuma maombi ya kusajiliwa kama raia.

(2) Mtu ambaye amekuwa mkazi halali nchini Kenya kwa muda wa miaka saba

mfululizo, na ambaye anatimiza masharti yote ya sheria yaliyoidhinishwa na Bunge, anaweza kutuma maombi ya kujiandikisha kama raia.

(3) Mtoto ambaye si raia na ambaye ni wa kupangwa na raia, ana haki ya kuwa raia kwa kutuma maombi .

(4) Bunge litatunga sheria itakayotoa masharti ambayo yatazingatiwa kuwapa uraia watu binafsi ambao ni raia wa nchi nyingine.

(5) Kifungu hiki kitatumika kwa mtu kuanzia tarehe ya kuanza kutumiwa kwa Katiba hii , lakini mahitaji yoyote ambayo ni lazima yatimizwe kabla ya mtu anayestahili kusajiliwa kama raia, yatachukuliwa kama yaliyotimizwa pasi na kuzingatia iwapo mtu huyu aliyatimiza kabla au baada ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, au kwa kiwango fulani kabla au baada ya tarehe ya kutekelezwa.

**Uraia mara mbili**

**16.** (1) Mtu ambaye ni raia kwa kuzaliwa hapotezi uraia wake kwa sababu ya kupata uraia wa nchi nyingine.

**Kupokonywa uraia**

**17.** (1) Iwapo mtu amepata uraia kwa kusajiliwa, uraia huo unaweza kupokonywa iwapo-

(a) mtu huyo alijipatia uraia huo kwa njia ya ulaghai, udanganyifu wa uwakilishi au kuficha ukweli unaotakikana;

(b) iwapo mtu huyo, katika vita vyovyote ambavyo Kenya ilihusika, kinyume na sheria alifanya biashara au kuwasiliana na adui au amejihusisha au kushiriki biashara na ambayo kwa kujua, ilitekelezwa kwa namna ambayo ilikuwa ni kusaidia adui;

(c) katika kipindi cha miaka mitano baada ya kusajiliwa, amepatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu au zaidi; au

(d) wakati wowote ule baada ya kusajiliwa amepatikana na hatia ya uhaini au hatia ambayo-

(i) amepewa adhabu ya kifungo cha angalau miaka saba au zaidi; au

(ii) hukumu kali zaidi inaweza kutolewa.

(2) Uraia wa mtu ambaye alichukuliwa kuwa raia kwa kuzaliwa kama inavyofikiriwa katika Kifungu cha 14 (4) unaweza kupokonywa iwapo-

(a) uraia ulipatikana kwa njia ya ulaghai, udanganyifu wa uwakilishi au kuficha ukweli unaotakikana kwa mtu yoyote;

(b) utaifa au kuzaliwa kwa mtu huyo kunajulikana na kufichua kwamba mtu huyo alikuwa raia wa nchi nyingine; au

Draft for approval

(c) umri wa mtu huyo unakuja kujulikana na kufichua kwamba alikuwa na umri wa zaidi ya miaka minane alipopatikana nchini Kenya.

**Sheria kuhusu Uraia**

**18.** Bunge litaunda sheria —

(a) kueleza taratibu ambazo kupitia kwazo mtu anaweza kuwa raia;

(b) kuongoza uingiaji na kukaa nchini Kenya

(c) kutoa hali ya wakaazi wa kudumu;

(d) kutoa nafasi ya kukana uraia kwa hiari;

(e) kutoa taratibu za kupokonywa uraia;

(f) kuamua majukumu na haki za raia; na

(g) Kwa jumla, kuyawezesha masharti ya Sura hii.

Draft for approval

## SURA YA NNE

## SHERIA YA HAKI

**Sehemu ya 1- Masharti ya jumla kuhusiana na Sheria ya Haki**

**Haki na uhuru wa kimsingi**

**19.** (1) Sheria ya Haki ni kiungo muhimu katika utawala wa kidemokrasia nchini Kenya na ndiyo msingi wa sera za kijamii, kiuchumi na kitamaduni.

(2) Lengo la kutambua na kulinda haki za binadamu na uhuru wa kimsingi ni kulinda heshima ya watu binafsi na jamii tofauti na kukuza haki za kijamii na kufanikisha uwezo wa binadamu wote.

(3) Haki na uhuru wa kimsingi zinazotajwa katika sura hii-

(a) ni za kila mtu binafsi na wala hazikabidhiwi na Serikali;

(b) hazitengi haki na uhuru mwingine wa kimsingi ambao haukutajwa katika Sura hii, lakini zinazotambuliwa na kukubaliwa na sheria, ila kwa kiwango ambacho hazikubaliani na Sura hii; na

(c) zinazingatia mipaka inayoelezwa katika Katiba hii.

Draft for approval

**Utekelezaji wa Sheria ya Haki**

**20.** (1) Sheria ya Haki inahusu sheria zote na inajumlisha idara zote za Serikali na watu wote.

(2) Kila mtu ana haki na uhuru wa kimsingi uliotajwa katika Sheria ya Haki, kwa kiwango kikubwa kuambatana na hali ya haki hiyo au uhuru huo wa kimsingi.

(3) Katika kutekeleza Sheria ya Haki, mahakama inapaswa-

(a) kukuza sheria kupita kiwango ambacho sheria imeiangazia haki au uhuru wowote wa kimsingi; na

(b) kuchukua fasiri inayopendelea kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa haki au uhuru wa kimsingi.

(4) Katika kufasiri Sheria ya Haki, mahakama, mahakama maalum, au mamlaka nyingine zitaendeleza-

(a) maadili yanayoongoza jamii iliyo wazi na ya kidemokrasia kulingana na heshima ya ubinadamu, ulinganifu, usawa, na uhuru; na

(b) imani, madhumuni na malengo ya Sheria ya Haki.

(5) Katika utekelezaji wa haki yoyote chini ya Kifungu cha 43, endapo Serikali inadai kuwa haina rasilimali za kutekeleza haki hiyo, mahakama, mahakama maalum au mamlaka yoyote itaongozwa na kanuni zifuatazo-

(a) ni jukumu la Serikali kuonyesha kuwa rasilmali hazipo;

(b) katika kugawa rasilmali, Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuna uwezekano mkubwa wa kunufaishwaa na haki au uhuru wa kimsingi kwa kuzingatia hali halisi, kukiwemo kutengwa kwa baadhi ya makundi au watu binafsi; na

(c) Mahakama, mahakama maalum au mamlaka nyingine haziwezi kuingilia uamuzi wa idara ya Serikali kuhusu ugavi wa rasilmali zilizopo, hasa kwa misingi kuwa itakuwa imefikia uamuzi tofauti.

**Utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi**

**21.** (1) Ni wajibu wa kimsingi wa Serikali na kila idara ya Serikali kuzingatia, kuheshimu, kulinda, kuendeleza, na kutimiza haki na uhuru wa kimsingi katika Sheria ya Haki.

(2) Serikali itachukua hatua za kisheria, kisera na nyinginezo ikihusisha uwekaji wa viwango ili kufanikisha ufikiaji wa haki kama ilivyohakikishiwa katika ibara ya 43.

(3) Ni wajibu wa mashirika yote ya Serikali na watumishi kushughulikia mahitaji ya makundi maalum katika jamii, wakiwemo wanawake, wazee, watu wenye ulemavu, watoto, vijana na jamii za walio wachache au zilizotengwa, pamoja na jamii fulani za kikabila, kidini na kitamaduni.

(4) Serikali itabuni na kutekeleza sheria ili kutimiza wajibu wake wa kimataifa kuhusu haki za binadamu na uhuru wa kimsingi.

**Utekelezaji wa Sheria ya Haki**

**22.** (1) Kila mtu ana haki ya kuwasilisha kesi mahakamani akidai kunyimwa, kukiukwa, au kutishiwa haki au uhuru wa kimsingi ulioko katika Sheria ya Haki

(2) Pamoja na kuwasilishwa na mtu anayewawakilisha, kesi chini ya ibara ya (1) inaweza kuwasilishwa mahakamani na-

(a) mtu anayemwakilisha mtu mwingine asiyeweza kujiwakilisha;

(b) mtu ambaye pia ni mwanachama wa kundi fulani au kwa hiari ya kundi au tabaka fulani la watu;

(c) mtu aliyejitolea kwa niaba ya umma; na

(d) muungano uliojitolea kwa niaba ya mtu mmoja au kundi miongoni mwa wanachama.

(3) Jaji Mkuu ataweka kanuni zinazoruhusu kesi zilizotajwa katika kifungu hiki ambazo zitaridhisha kigezo kwamba-

(a) haki za kulalamika zilizotolewa katika ibara ya (2) zinatekelezwa kwa ukamilifu;

(b) urasmi unaohusiana na kesi hizo, kukiwemo kuanzishwa kwa kesi, unawekwa kwa kiwango cha chini, na hasa pakiwa na haja, mahakama itakubali kuwepo kwa kesi kwa misingi ya rekodi zisizo na ulazima wa urasmi;

Draft for approval

(a) hakuna fedha zitakazotozwa kwa kuanzisha kesi;

(b) mahakama, kwa kuzingatia kanuni za haki za kimsingi haitazuiwa bila sababu na mahitaji madogo madogo; na

(c) shirika au mtu binafsi mwenye ujuzi maalum anaweza, kwa idhini ya mahakama, kujitokeza kama rafiki wa mahakama.

(4) Kukosekana kwa kanuni zinazoangaziwa katika ibara ya (3) hakutamnyima yeyote haki ya kuwasilisha malalamiko kulingana na Kifungu hiki, kusikizwa kwa malalamiko hayo na kuamriwa na mahakama.

**Mamlaka ya mahakama kudumisha na kutekeleza Sheria ya Haki**

**23.** (1) Mahakama Kuu ina mamlaka kwa mujibu wa Kifungu cha 165 kusikiliza upya na kuamua kesi inayohusu kunyimwa, kukiukwa, kuvunjwa au kutishiwa kwa haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria ya Haki.

(2) Bunge litatunga sheria kutoa uwezo wa kiasili kwa mahakama ya chini katika kusikizwa upya na kuamuliwa kwa kesi dhidi ya kunyimwa, kuvunjwa na kukiukwa kwa Sheria ya Haki.

(3) Katika kesi yoyote inayoletwa mbele yake chini ya Kifungu cha 22, mahakama inaweza kutoa usaidizi, ukiwemo-

(a) kukiri haki;

(b) agizo la kusimamisha kesi;

(c) amri ya uhifadhi;

(d) kutangaza kutofaa kwa sheria yoyote inayonyima, kuvunja, kuingilia na kutishia Sheria ya Haki na isiyokubalika kwa misingi ya Kifungu cha 24;

(e) amri ya kufidiwa; na

(f) amri ya marekebisho ya kisheria

**Mipaka ya haki au uhuru wa kimsingi**

**24.** (1) Haki ya uhuru wa kimsingi iliyo katika Sheria ya Haki haiwezi kuwekewa mipaka isipokuwa kupitia kwa sheria na iwe tu kwamba mipaka ina maana, na ni ya haki katika jamii iliyo wazi na ya kidemokrasia, na chini ya misingi ya heshima ya binandamu, usawa na uhuru, na kwa kuzingatia vipengele muhimu vikiwemo-

(a) hali ya haki hiyo au uhuru wa kimsingi;

(b) umuhimu wa lengo la mipaka hiyo;

(c) hali na kiwango cha mipaka hiyo;

Draft for approval

(d) haja ya kuhakikisha kuwa kufurahia wa haki hizo na uhuru huo wa kibinafsi kwa mtu yeyote hautatizi haki na uhuru wa kimsingi wa watu wengine; na

(e) uhusiano uliopo kati ya mpaka na lengo lake na endapo kuna njia zingine zisizotatiza za kufikia lengo hilo.

(2) Licha ya ibara ya (2), sharti la sheria linalowekea mipaka haki au uhuru wa kimsingi-

(a) ikiwa ni sharti lililotungwa au kurekebishwa kabla au baada ya siku ya kuanza kutumika Katiba hii, si halali, isipokuwa sheria hiyo haswa inadhihirisha madhumuni ya kuiwekea mipaka haki hiyo au uhuru wa kimsingi na kiwango cha mipaka hiyo;

(b) halitachukuliwa kama kuzuia haki au uhuru uliotajwa katika Sheria ya Haki isipokuwa pale ambapo sharti hilo linaeleza wazi na kwa yakini kuhusu haki au uhuru wa kimsingi unaopaswa kuzuiwa na hali au kiwango cha mipaka hiyo; na

(c) halitazuia haki au uhuru wa kimsingi unaotajwa katika Sheria ya Haki ili kupunguza uzito na umuhimu uliowekwa katika haki hiyo.

(3) Serikali au mtu anayetaka kuhalalisha mpaka fulani atapaswa kuthibitishia mahakama, mahakama maalum au mamlaka nyingine kuwa mahitaji ya Kifungu hiki yameridhishwa.

(4) Masharti katika Sura hii kuhusu usawa yatatumika kwa wote ila tu pale ambapo patahitajika utekelezaji wa Sheria ya Kiislamu mbele ya mahakama za Kadhi kwa waumini wa Kiislamu kwa mujibu wa hadhi zao za kibinafsi, hali ya ndoa, talaka na urithi.

(5) Licha ya ibara za (1) na (2), sharti la sheria linaweza kuwekea mipaka utekelezaji wa haki na/au uhuru wa kimsingi katika masharti kwa watu wanaohudumu katika Vikosi vya Usalama vya Kenya, au Huduma za Polisi za Kitaifa-

(a) Kifungu cha 31- Faragha;

(b) Kifungu cha 36 -Uhuru wa kutangamana

(c) Kifungu cha 37- Mikutano, maandamano, migomo na malalamiko;

(d) Kifungu cha 41 –Mahusiano ya kikazi;

(e) Kifungu cha 43 – Haki za kiuchumi na kijamii;

(f) Kifungu cha 49 –Haki za watu waliotiwa mbaroni;

**Haki na Uhuru Usioweza Kuwekewa Mipaka**

**25.** Licha ya sharti lolote lingine katika Katiba hii, hakutakuwa na mipaka dhidi ya haki na uhuru wa kimsingi ufuatao-

Draft for approval

(a) uhuru dhidi ya mateso, unyanyasaji au adhabu zilizokiuka ubinadamu;

(b) uhuru dhidi ya utumwa;

(c) haki kwenye kesi ; na

(d) haki ya kuitikia amri ya kufikishwa mahakamani.

**Sehemu ya 2- Haki na uhuru wa kimsingi**

**Haki ya kuishi**

**26.** (1) Kila mtu ana haki ya kuishi.

(2) Maisha ya mtu huanza baada ya kutunga mimba.

(3) Mtu hatauawa kimaksudi, isipokuwa kwa kiwango kinachoidhinishwa na Katiba hii au kwa sheria nyingine iliyoandikwa;

(4) Uavyaji mimba hauruhusiwi, isipokuwa kwa maoni ya mtaalamu wa masuala ya afya, kuna haja ya matibabu ya dharura, au maisha au afya ya mama imo hatarini au kwa kuidhinishwa na sheria nyingine iliyoandikwa;

**Usawa na Uhuru dhidi ya kubaguliwa**

**27.** (1) Kila mtu ni sawa mbele ya sheria na ana haki ya kulindwa na kupata manufaa sawa ya sheria.

(2) Usawa unajumuisha kupata haki na uhuru wote wa kimsingi kwa njia iliyo kamili na sawa.

(3) Wanawake na wanaume wana haki ya usawa ikiwemo haki ya kupata nafasi sawa katika shughuli za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii.

(4) Serikali, kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, haitakuwa na ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa misingi yoyote ikiwemo asili, jinsia, ujauzito, hali ya mtu kindoa, hali ya kiafya, asili ya kikabila au kijamii, rangi, umri, ulemavu, dini, dhamiri, imani, utamaduni, mavazi, lugha au kuzaliwa.

(5) Mtu hatakuwa na ubaguzi dhidi ya mwingine kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo katika misingi iliyotajwa na kuonyeshwa na ibara ya (4).

(6) Ili kutoa athari kamilifu za kutimiza haki zinazohakikishiwa na Kifungu hiki, Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo kukiwemo vitendo sawazishi na sera ambazo zimebuniwa kupinga athari za kutonufaika kwa watu binafsi au makundi ya watu kwa sababu ya ubaguzi wa hapo awali.

(7) Hatua yoyote inayochukuliwa chini ya ibara ya (6) itashughulikia kikamilifu fidia yoyote kwa kuzingatia uhitaji ulioko .

Draft for approval

(8) Pamoja na hatua zinazokusudiwa katika ibara ya (6), Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo ili kutekeleza kanuni kwamba, idadi ya watu waliochaguliwa au kuteuliwa katika mashirika haitakuwa na wanachama zaidi ya thuluthi mbili wa jinsia moja.

**Hadhi ya Binadamu**

**28.** (1) Kila mtu anamiliki heshima ya kuzaliwa kama binadamu na haki ya kutaka hali hii iheshimiwe.

**Uhuru na usalama wa mtu**

**29.** Kila mtu ana haki ya uhuru na usalama wake unaohusisha haki ya-

(a) kutonyimwa uhuru kiholela bila sababu;

(b) kutozuiliwa bila kushtakiwa mahakamani, isipokuwa wakati wa hali ya hatari ambapo kifungo cha aina hiyo kinaelezwa katika Kifungu cha 58;

(c) kuwa huru dhidi ya aina zote za ghasia kutoka kwa umma au watu binafsi;

(d) kutoteswa kwa njia yoyote ile, iwe ya kimwili au kiakili;

(e) kutopewa adhabu ya viboko; au

(f) kutotendewa au kupewa adhabu za kikatili, kudhalilisha au kushusha hadhi ya ubinadamu.

**Utumwa na kazi ya kulazimishwa**

**30.** (1) Hakuna mtu atazuiliwa katika utumwa.

(2) Mtu hatahitajika kufanya kazi ya kulazimishwa.

**Faragha**

**31.** Kila mtu ana haki ya faragha yake, inayohusisha haki ya-

(a) kutosakwa yeye mwenyewe, makao yake au mali yake;

(b) mali kutonyakuliwa;

(c) habari kuhusu familia au masuala ya kibinafsi ambayo hayahitajiki au kufichuliwa pasi na umuhimu wowote;

(d) faragha ya mawasiliano yao kutoingiliwa.

Draft for approval

**Uhuru wa dhamiri, dini, imani na maoni**

**32.** (1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kuwa na msimamo, dini, mawazo, imani na maoni.

(2) Kila mtu ana haki, ama kibinafsi au na wengine katika jamii, kwa wazi au kifaragha, kufuata dini au imani yoyote kupitia ibada, matendo, mafundisho au maadhimisho, yakiwemo mazingatio ya siku za ibada.

(3) Mtu hatazuiwa kuingia ama kujiunga na taasisi yoyote, kunyimwa ajira au kufika mahali fulani au kufurahia haki yoyote kwa sababu ya imani yake ya kidini.

(4) Mtu hatalazimishwa kutenda au kujihusisha na kitendo chochote ambacho ni kinyume na imani ya dini yake.

**Uhuru wa kujieleza**

**33.** (1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kujieleza unaohusisha-

(a) uhuru wa kutafuta, kupokea au kutoa habari au kauli;

(b) uhuru wa ubunifu wa kisanii; na

(c) uhuru wa kiakademia na utafiti wa kisayansi.

(2) Haki ya uhuru wa kujieleza haiambatani na -

(a) propaganda ya vita;

(b) uchochezi wa ghasia;

(c) hotuba za chuki; au

(d) utetezi wa chuki ambao -

(i) unajumuisha uchochezi wa kikabila, kuwatusi wengine au uchochezi wa kusababisha maafa; au

(ii) unaotokana na misingi yoyote ya ubaguzi iliyotajwa au kuonyeshwa katika Kifungu cha 27 (4).

(3) katika kutekeleza uhuru wa kujieleza, kila mtu ataheshimu haki na hadhi ya watu wengine.

**Uhuru wa vyombo vya habari**

**34.** (1) Uhuru na kujitegemea kwa vyombo vya matangazo, kuchapisha na vingine vya habari ya aina yoyote unahakikishwa lakini hauhusishi masharti yaliyotajwa katika Kifungu cha 33 (2) .

(2) Serikali –

(a) haitadhibiti au kuingilia mtu yeyote anayehusika na utangazaji, uchapishaji au

Draft for approval

usambazaji wa chapisho lolote au usambazaji wa habari kwa kutumia nyenzo yoyote; au

(b) haitamwadhibu mtu yeyote kwa kutoa maoni au mawazo au masuala yaliyomo kwenye matangazo, machapisho au usambazaji.

(3) Vyombo vya utangazaji na vyombo vingine vya habari na vya kielektroniki vina uhuru wa kujiendeleza kwa kuongozwa tu na taratibu za leseni ambazo-

(a) zimeratibiwa kuhakikisha udhibiti wa mawimbi ya hewa na aina nyingine za usambazaji wa mawimbi; na

(b) haviingiliwi na Serikali, maslahi ya kisiasa au ya kibiashara.

(4) Vyombo vyote vya habari vinavyomilikiwa na Serikali-

(a) vitakuwa huru kuamua kuhusu habari, tahariri na matangazo yao au mawasiliano mengine;

(b) havitaegemea upande wowote; na

(c) vitatoa nafasi sawa ya kuwasilisha maoni tofauti tofauti na mawazo yanayokinzana.

(5) Bunge litatunga sheria itakayotoa nafasi ya kuanzisha shirika ambalo-

(a) litakuwa huru dhidi ya udhibiti wa Serikali au kuingiliwa kisiasa;

(b) litaangazia maslahi ya sekta zote za jamii; na

(c) litaweka viwango na kudhibiti vyombo vya habari na kutathmini uzingativu wa viwango hivyo.

Draft for approval

**Upataji habari**

**35.** (1) Kila mwananchi ana haki ya kupata-

(a) habari ilizonazo Serikali; na

(b) habari zozote alizonazo mtu mwingine na zinazohitajika ili kutekeleza au kulinda haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi.

(2) Kila mtu ana haki ya kudai marekebisho au kubatilishwa kwa habari zozote za uongo au za kupotosha zinazomhusu mtu huyo.

(3) Serikali itachapisha na kutangaza taarifa yoyote inayoathiri taifa.

**Uhuru wa kutangamana**

**36.** (1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutangamana ambayo inahusu haki ya kuanzisha, kujiunga na ,au kushiriki katika majukumu ya mashirika.

(2) Mtu hatalazimishwa kujiunga na muungano wa aina yoyote.

(3) Sheria yoyote kuhusu usajili wa miungano ya makundi ya kijamii itahitaji kwamba-

(a) usajili huo hauwezi kuzuiwa au kuondolewa bila sababu maalum; na

(b) kutakuwa na haki ya kusikizwa kwa kesi hiyo kabla ya usajili huo kuvunjiliwa mbali.

**Mikutano, maandamano, migomo na malalamiko**

**37.** Kila mtu ana haki, bila haja ya kuomba ruhusa, ya kukutana, kuandamana, kugoma, na kuwasilisha malalamiko yake kwa mamlaka ya umma ila tu afanye hivyo kwa amani na bila kutumia silaha.

**Haki za kisiasa**

**38.** (1) Kila mwananchi ana uhuru wa kuwa na uchaguzi wa kisiasa, ikiwemo haki ya –

(a) kuunda, au kushiriki katika uundaji wa chama cha kisiasa;

(b) kushiriki katika shughuli za, au kusajili wanachama kwa niaba ya chama cha kisiasa; au

(c) kufanyia kampeni chama cha kisiasa.

(2) Kila mwananchi ana haki ya kushiriki katika uchaguzi huru, wa haki na unaofanyika mara kwa mara kwa misingi ya haki ya kupiga kura kwa wote na uhuru wa hiari ya mpiga kura kwa -

(a) shirika au afisi yoyote ya umma iliyobuniwa chini ya Katiba hii na inayofanya uchaguzi; na

(b) kiongozi wa afisi yoyote ya chama cha kisiasa ambacho mwananchi huyo ni mwanachama.

(3) Kila raia akiwa mtu mzima ana haki pasipo na masharti yasiyo na busara,-

(a) kujiandikisha kama mpiga kura;

(b) kupiga kura ya siri katika uchaguzi wowote au katika kura ya maamuzi; na

(c) kugombea wadhifa katika afisi ya umma, au afisi katika chama cha kisiasa ambacho yeye ni mwanachama na endapo atachaguliwa, ashike usukani.

**Uhuru wa kutembea na makaazi**

**39.** (1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutembea.

Draft for approval

(2) Kila mtu ana haki ya kuondoka nchini Kenya.

(3) Kila mwananchi ana haki ya kuingia, kubaki na kuishi kokote nchini Kenya.

**Ulinzi wa haki ya kumiliki mali**

**40.** (1) Kwa kuzingatia Kifungu cha 65, kila mtu ana haki, kibinafsi au kwa kuungana na wengine kupata na kumiliki mali-

(a) ya aina yoyote; na

(b) katika sehemu yoyote ya Kenya.

(2) Bunge halitatunga sheria inayoruhusu Serikali au mtu yeyote –

(a) kidhalimu kumpokonya mtu mali ya aina yoyote, au thamana ama haki juu ya, mali ya aina yoyote;

(b) kumzuia, au kwa njia yoyote kumnyima kufurahia haki chini ya Kifungu hiki katika misingi iliyobainishwa katika Kifungu cha (27) (4).

(3) Serikali haitamnyima mtu yeyote haki ya kuwa na mali ya aina yoyote, au nia au haki ya kuwa na mali ya aina yoyote isipokuwa endapo kuzuiwa huko-

(a) kunatokana na upataji ardhi au nia ya kutaka ardhi au kubadilisha maslahi fulani ili kupata ardhi, au hatimiliki ya ardhi, kwa mujibu wa Sura ya Tano; au

(b) ni kwa matumizi ya umma au ni kwa manufaa ya umma na inatekelezwa kwa mujibu wa Katiba hii au Sheria nyingine yoyote ya Bunge

Kwamba-

(i) inahakikisha malipo kwa ukamilifu ya kumfidia mtu huyo kabla ya mali hiyo kuchukuliwa;

(ii) inampa mtu yeyote, mwenye maslahi au haki juu ya mali hiyo, njia ya kufikia mahakama ya kisheria.

(4) Sharti linaweza kuundwa ili kuruhusu fidia kulipwa kwa wakazi wa ardhi kwa nia nzuri chini ya ibara ya (3), ambao huenda hawana hatimiliki ya ardhi hiyo.

(5) Serikali itaunga mkono, kukuza na kulinda hakimiliki ya usomi kwa watu wa Kenya.

(6) Haki chini ya Kifungu hiki haijumlishi mali yoyote ambayo haijapatikana kisheria.

**Mahusiano ya kikazi**

**41.** (1) Kila mtu ana haki ya kanuni sawa za kikazi.

(2) Kila mfanyakazi ana haki ya-

Draft for approval

(a) kulipwa ipasavyo;

(b) mazingira ya kufaa ya kufanyia kazi;

(c) kuunda, kujiunga au kushiriki katika shughuli na mipango ya vyama vya wafanyakazi; na

(d) kugoma.

(3) Kila mwajiri ana haki ya-

(a) kuunda au kujiunga na vyama vya waajiri; na

(b) kushiriki katika shughuli na mipango ya vyama vya waajiri.

(4) Kila chama cha wafanyakazi na vyama vya waajiri vina haki ya-

(a) kuamua usimamizi wake, mipango na shughuli zake;

(b) kupanga; na

(c) kuunda na kujiunga na shirikisho.

(5) Kila chama cha wafanyakazi, muungano wa wajiri na mwajiri wana haki ya kushiriki katika maafikiano ya pamoja.

Draft for approval

**Mazingira**

**42.** (1) Kila mtu ana haki ya kuishi katika mazingira safi na salama, ambapo ni pamoja na haki ya-

(a) kutunziwa mazingira kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo kupitia kwa hatua za kisheria na nyinginezo hasa zile ambazo zinakusudiwa katika Kifungu cha 69;

(b) Kuhakikisha kuwa wajibu unaohusu mazingira, ulio chini ya Kifungu cha ya 70 umetimizwa.

**Haki za kiuchumi na kijamii**

**43.** (1) Kila mtu ana haki ya -

(a) kupata kiwango cha juu kabisa kinachowezekana cha afya, kinachohusu haki ya huduma za malezi ya kiafya ikiwa ni pamoja na malezi ya afya ya uzazi;

(b) kupata makao ya kuridhisha, na viwango vinavyostahili vya usafi

(c) kutokuwa na njaa, na kupata chakula cha kutosha na kinachostahili;

(d) kupata maji safi na salama na ya kutosha;

(e) usalama wa kijamii ; na

(f) elimu.

(2) Mtu hatanyimwa matibabu ya dharura.

(3) Serikali itatoa ulinzi wa kijamii unaofaa kwa wale ambao hawawezi kujisimamia wao wenyewe na jamii zao.

**Lugha na utamaduni**

**44.** (1) Kila mtu ana haki ya kutumia lugha na kushiriki katika maisha ya kitamaduni ya chaguo lake.

(2) Mtu anayetoka katika jamii ya utamaduni au lugha fulani ana haki, pamoja na wanajamii wenzake-

(a) kufurahia utamaduni wake na kutumia lugha yake; au

(b) kuunda, kujiunga na kudumisha vyama vya kitamaduni na kilugha na miungano mingine ya raia katika jamii.

(3) Mtu hatamlazimisha mwingine kufanya, kuzingatia au kupitia mila zozote za kitamaduni.

**Familia**

**45.** (1) Familia ndicho kitengo cha asilia na kimsingi cha jamii na msingi muhimu katika mpangilio wa Jamii, na itafurahia kutambuliwa na kulindwa na Serikali.

(2) Kila mtu mzima ana haki ya kuoa mtu wa jinsia tofauti na yake na kulingana na makubaliano yao.

(3) Wahusika katika ndoa wana haki sawa wakati wa kuoana, katika ndoa na wakati wa kuvunjwa kwa ndoa yao.

(4) Bunge litatunga sheria inayotambua-

(a) ndoa zilizotekelezwa chini ya utamaduni wowote, au mfumo wowote wa kidini, kibinafsi au sheria ya familia; na

(b) Sheria ya kibinafsi au familia chini ya utamaduni wowote, au inayofuatwa na waumini wa dini fulani kwa kiasi kwamba, ndoa au mifumo kama hiyo ya kisheria inazingatia Katiba hii.

**Haki za watumiaji wa Bidhaa**

**46.** (1) Watumiaji wa bidhaa na huduma wana haki ya-

(a) kupata bidhaa na huduma za ubora wa kukubalika;

Draft for approval

(b) habari zenye manufaa kwao ili waweze kupata faida kamili kutokana na huduma na bidhaa hizo;

(c) kulindwa afya yao, usalama wao, na maslahi yao ya kiuchumi; na

(d) kufidiwa kwa hasara au matatizo yatakayotokana na kasoro ya bidhaa au huduma hizo.

(2) Bunge litatunga sheria ya kuhakikisha ulinzi wa watumiaji na wa matangazo huru, kweli na ya kufaa.

(3) Kifungu hiki kinahusu bidhaa na huduma zitakazotolewa na mashirika ya umma au watu binafsi.

Draft for approval

**Hatua ya haki za kiutawala**

**47.** (1) Kila mtu ana haki ya vitendo vya utawala ambavyo ni vya haraka, ufanisi, vya kisheria, vinavyofaa na sawa.

(2) Kila mtu ambaye haki yake au uhuru wake wa kimsingi umeathiriwa au unaweza kutatizwa kabisa na hatua ya kiutawala, ana haki ya kupewa sababu kwa njia ya maandishi kuhusu hatua hiyo.

(3) Bunge litatunga sheria ya kuidhinisha haki zilizotajwa katika ibara ya (1) na sheria hiyo-

(a) itatoa nafasi ya kurekebishwa kwa hatua hiyo ya kiutawala na mahakama au, ikiwezekana mahakama huru isiyoegemea upande wowote; na

(b) kuendeleza uongozi unaofaa.

**Uwezo wa Kufikia Haki**

**48.** Serikali itahakikisha uwezekano wa watu wote kufikia haki na malipo yoyote yakihitajika, yatakuwa ya kufaa na hayatazuia uwezekano wa kutendewa haki.

**Haki za waliotiwa mbaroni**

**49.** (1) Kila mtu aliyetiwa mbaroni ana haki ya-

(a) kuarifiwa kwa upole na kwa lugha anayoielewa, kuhusu-

(i) sababu ya kukamatwa;

(ii) haki ya kunyamaza; na

(iii) matokeo ya kutonyamaza;

(b) kunyamaza;

(c) kuwasiliana na wakili na watu wengine ambao msaada wao unahitajika;

(d) kutolazimishwa kutubu au kukiri hatia, hali ambayo inaweza kutumiwa katika ushahidi dhidi yake;

(e) kutenganishwa na watu wanaohudumia vifungo;

(f) kufikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo, lakini si baada ya-

(i) saa ishirini na nne baada ya kukamatwa; au

(ii) iwapo hizo saa ishirini na nne zimekamilika wakati ambapo vikao vya mahakama haviendelei au kwa siku isiyo ya mahakama, kufikia mwisho wa siku ya mahakama inayofuatia;

(g) kufunguliwa mashtaka au kuarifiwa kuhusu sababu ya kuendelea kuzuiliwa kwake, au kuachiliwa huru siku yake ya kwanza ya kufikishwa mahakamani; na

(h) kuachiliwa kwa dhamana kwa sababu zinazoeleweka kabla ya kushtakiwa isipokuwa kukiwa na sababu nyingine za kulazimisha kutendwa kinyume cha dhamana hiyo.

(2) Mtu hatawekwa rumande kwa kosa linaloweza kuadhibiwa kwa kutozwa faini pekee au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi sita.

Draft for approval

**Haki katika kusikizwa kwa kesi**

**50.** (1) Kila mtu ana haki ya kutaka mzozo wowote unaoweza kusuluhishwa kisheria kuamuliwa katika kikao cha haki mahakamani au, ikiwezekana asasi au mahakama maalum iliyo huru na isiyoegemea upande wowote.

(2) Kila mshtakiwa ana haki ya kesi yake kusikizwa kwa njia ya haki, ikiwemo haki ya-

(a) kuaminiwa kutokuwa na hatia hadi ithibitishwe kinyume;

(b) kuarifiwa kuhusu mashtaka na kupewa taarifa ya kutosha kuyahusu;

(c) kuwa na wakati na vifaa vya kutosha kutayarisha nyenzo za kujitetea;

(d) kushtakiwa kwenye mahakama ya umma iliyobuniwa kwa mujibu wa Katiba hii;

(e) kuanzishwa na kumalizika kwa mashtaka bila kucheleweshwa;

(f) kuwepo wakati wa kesi isipokuwa pale ambapo mienendo ya mshtakiwa inatatiza vikao vya kesi hiyo;

(g) kuchagua na kuwakilishwa na wakili na kuelezwa kuhusu haki hii moja kwa moja;

(h) kuwa na wakili aliyetolewa na Serikali kwa gharama ya Serikali yenyewe, endapo haki yake ya msingi imevunjwa, na aarifiwe kuhusu haki hii moja kwa moja;

(i) kunyamaza, na kutotoa ushahidi wakati wa kesi;

(j) kuelezwa mwanzoni kuhusu ushahidi ambao kiongozi wa mashtaka ananuia kutumia na kuweza kuufikia ushahidi huo.

(k) kuleta na kupinga ushahidi;

(l) kutolazimishwa kutoa ushahidi wa kujifunga;

(m) kuwa na usaidizi wa mkalimani bila ya kulipishwa endapo mshtakiwa hawezi kuelewa lugha inayotumiwa katika kesi;

(n) kutohukumiwa kwa kitendo, au kosa ambalo wakati wa utendekaji au ukosaji halikuwa-

(i) kosa nchini Kenya; au

(ii) kosa la jinai chini ya sheria ya kimataifa;

(o) kutoshtakiwa kwa kosa la kulinganishwa na tendo au kosa ambalo mtu huyo amewahi ama kuachiliwa au kuhukumiwa kwalo;

(p) kunufaika kwa angalau adhabu ndogo kabisa katika adhabu zilizoruhusiwa endapo adhabu iliyoidhinishwa kwa kosa lake imebadilishwa kati ya muda wa utendekaji wa kosa hilo na wakati wa kuhukumiwa; na

(q) kukata rufani au kuchunguzwa upya kwa kesi hiyo na mahakama ya ngazi ya juu.

(3) Kila kifungu hiki kinapohitaji taarifa kutolewa kwa mtu, taarifa hiyo itatolewa katika lugha anayoielewa mtu huyo.

(4) Ushahidi unaopatikana katika njia inayokiuka haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi uliotolewa katika Sheria ya Haki utaachwa endapo utekelezaji wa ushahidi huo utafanya kesi kukosa haki au uwe kikwazo katika upatikanaji wa haki.

(5) Mshtakiwa-

(a) anayeshtakiwa kwa kosa fulani, kando na kosa ambalo mahakama inaweza kukamilisha kwa haraka, atakuwa na ruhusa endapo ataomba, ya kupata nakala ya rekodi za kesi.

(b) ana haki ya kupata nakala ya rekodi ya kesi ya vikao vya mashtaka kwa wakati unaofaa baada ya kukamilishwa kwa kesi hiyo, kwa malipo fulani kama inavyoidhinishwa na sheria.

(6) Mtu aliyehukumiwa kwa kosa la jinai anaweza kulalamikia mahakama kuu ili kusikizwa upya kwa kesi iwapo-

(a) rufani yake imetupiliwa mbali na mahakama ya ngazi za juu ambayo mtu huyo alikuwa na haki ya kukata rufani, au awe hakukata rufani katika muda unaoruhusiwa kufanya hivyo; na

(b) ushahidi mpya na wa kushawishi umepatikana.

(7) Ili kutimiza haki, mahakama inaweza kuruhusu msuluhishi kusaidia mlalamishi au mshtakiwa kuwasiliana na mahakama.

Draft for approval

(8) Kifungu hiki hakikatazi kuzuiwa kwa vyombo vya habari ama umma kutokuwa mahakamani, kama kuzuiwa huko ni muhimu, katika jamii huru na ya kidemokrasia, ili kuwalinda mashahidi, wanyonge, maadili, utulivu wa umma, ama usalama wa kitaifa.

(9 Bunge litatunga sheria ya kutoa ulinzi, haki na hali ya waathiriwa wa hatia.

**Haki za walio kizuizini, walioshikwa ama waliofungwa**

**51.** (1) Mtu yeyote anayezuiliwa kisheria, awe amehukumiwa au la, ana haki zote na uhuru wa kimsingi unaoelezwa kwenye Katiba hii, isipokuwa kwa kiwango kwamba haki au uhuru huo wa kimsingi hauambatani kabisa na sababu yake ya kuwa kwenye jela.

(2) Mtu yeyote aliye kizuizini ama aliyezuiliwa ana haki ya kulalamika ili kutolewa amri ya kufikishwa mahakamani.

(3) Bunge litatunga sheria ambayo-

(a) itatoa kanuni za kushughulikiwa kibinadamu kwa walio kizuizini, waliokamatwa au waliofungwa jela; na

(b) kuzingatia sheria mwafaka za haki za binadamu za kimataifa.

Draft for approval

**Sehemu ya 3 -Utekelezaji mahususi wa haki**

**Ufafanuzi wa sehemu hii**

**52.** (1) sehemu hii inafafanua kwa undani baadhi ya haki ili kuhakikisha kiwango cha juu katika kutekeleza haki hizo na uhuru wa kimsingi kwa makundi fulani ya watu.

(2) sehemu hii haitafasiriwa kama kuwekea mipaka au kustahilisha haki yoyote.

**Watoto**

**53.** (1) Kila mtoto ana haki ya-

(a) jina na uraia kuanzia anapozaliwa;

(b) elimu ya msingi bila malipo na ya lazima;

(c) Lishe bora ya kimsingi, makazi na huduma za afya ;

(d) kulindwa dhidi ya kutumiwa vibaya, kutelekezwa, tamaduni za kuumiza, aina zozote za ghasia, matendo na adhabu zisizo za kibinadamu, kutumiwa vibaya, na kazi yoyote ya kunyanyasa au ya kuhatarisha;

(e) kutunzwa na kulindwa na wazazi, ambayo inahusu wajibu sawa kutoka kwa mama na baba wa kumkimu mtoto, iwe wameoana au la; na

(f) kutofungwa kinyume na matakwa yake isipokuwa endapo hiyo ndiyo hatua ya mwisho, na wakizuiliwa-

(i) kuzuiliwa kwa muda mfupi na unaostahili tu; na

(ii) kutenganishwa na watu wazima katika jela huku ikizingatiwa umri na jinsia ya mtoto.

(2) maslahi ya mtoto ni muhimu sana katika kila suala linalomhusu mtoto.

**Watu Wenye Ulemavu**

**54.** (1) Watu wenye ulemavu wana haki ya-

(a) kuheshimiwa na kupewa heshima ya binadamu ikiwemo, kushughulikiwa, kuzungumziwa na kutajwa, kwa njia isiyowadunisha au kuwadhalilisha;

(b) kupata elimu katika taasisi za elimu na vifaa vya watu wenye ulemavu vilivyofungamanishwa na jamii kwa minajili ya maslahi yao;

(c) kufikia ipasavyo sehemu zote zinazofikwa na umma, usafiri wa umma na habari na mawasiliano;

(d) kutumia lugha ya ishara, Breli, na njia nyingine mwafaka za mawasiliano; na

(e) kupata nyenzo na vifaa vinavyoweza kuwasaidia kukabiliana na matatizo ya ulemavu huo;

(2) Serikali itahakikisha kuendelea kwa utekelezaji wa kanuni kwamba, angalau asilimia tano ya maafisa katika mashirika, wanaochaguliwa au kuteuliwa, ni watu wenye ulemavu.

**Vijana**

**55.** (1) Serikali itachukua hatua, ikiwemo miradi ya vitendo sawazishi, kuhakikisha kwamba vijana-

(a) wanapata elimu na mafunzo yanayofaa;

(b) wana fursa ya kujumuika, kuwakilishwa na kushiriki katika nyanja za kisiasa, kijamii kiuchumi na nyanja nyingine za maisha;

(c) wanapata kazi; na

(d) kulindwa dhidi ya tamaduni zinazodhuru na kunyanyasa.

**Makundi yaliyotengwa na kubaguliwa**

**56.** (1) Serikali itatekeleza mipango inayonuia kuhakikisha kuwa makundi yaliyotengwa na kubaguliwa -

(a) yanashiriki na kuwakilishwa katika uongozi na nyanja zote za maisha;

Draft for approval

(b) yanapewa nafasi maalum katika nyanja za elimu na uchumi;

(c) yanapewa fursa maalum ya kuajiriwa;

(d) yanakuza tamaduni zao, lugha na kaida zao; na

(e) yanapata maji, huduma za afya na miundombinu ya usafiri;

**Wazee katika jamii**

**57.** (1) Serikali itachukua hatua kuhakikisha kuwa haki za wazee-

(a) kushiriki kikamilifu katika masuala ya jamii;

(b) kutafuta maendeleo ya kibinafsi;

(c) kuishi kwa hadhi na heshima na kuwa huru dhidi ya dhuluma;

(d) kupata malezi ya kufaa na msaada kutoka kwa familia zao na Serikali.

**Sehemu ya 4- Hali ya hatari**

**Hali ya hatari**

**58.** (1) Hali ya hatari inaweza kutangazwa tu kwa kuzingatia Kifungu cha 132 (4) (d) na pale tu-

(a) Nchi inatishiwa na vita, uvamizi, upinzani mkubwa, vurugu, janga la kitaifa au dharura zingine za umma; na

(b) tangazo hilo ni muhimu katika kukabiliana na hali ya hatari iliyotangazwa.

(2) Tangazo la hali ya hatari, na sheria yoyote itakayotungwa au hatua nyingine itakayochukuliwa kutokana na tangazo hilo, itatekelezeka tu -

(a) kwa matazamio; na

(b) kwa muda usiozidi siku kumi na nne kutoka siku ya kutangazwa kwa hali hiyo ya hatari, isipokuwa Baraza Kuu la Kitaifa liamue kuendeleza tangazo hilo.

(3) Baraza Kuu la Kitaifa linaweza kuendeleza tangazo la hali ya hatari –

(a) kutokana na uamuzi uliochukuliwa-

(i) kufuatia mijadala ya wazi Bungeni; na

(ii) idadi kubwa ya wabunge kama inavyodokezwa katika ibara Ya (4); na

(b) kwa muda usiozidi miezi miwili kwa wakati mmoja.

(4) Nyongeza ya kwanza ya kipindi cha hali ya hatari inahitaji kuungwa mkono na

Draft for approval

thuluthi mbili ya kura za wabunge, na itakayofuatia inahitaji kuungwa mkono na angalau robo tatu ya wabunge.

(5) Mahakama ya Juu inaweza kuamua kuhusu kufaa kwa-

(a) tangazo la hali ya hatari;

(b) nyongeza yoyote ya muda wa tangazo la hali ya hatari; na

(c) sheria yoyote itakayotungwa au hatua yoyote nyingine itakayochukuliwa, kwa sababu ya tangazo la hali ya hatari.

(6) Sheria yoyote inayotungwa kwa sababu ya tangazo la hali ya hatari,

(a) inaweza kuzuia uhuru wa kimsingi ulio katika Sheria ya Haki iwapo tu ni kwa kiwango kwamba-

(i) uzuiaji huo unastahili kutokana na dharura hiyo; na

(ii) sheria hiyo inaambatana na majukumu ya Jamhuri chini ya sheria ya kimataifa kuhusiana na hali ya hatari.

(b) Haitatekelezwa hadi ichapishwe kwenye Gazeti rasmi la serikali.

(7) Tangazo la hali ya hatari au sheria inayotungwa au hatua yoyote nyingine inayochukuliwa kwa sababu ya tangazo lolote, haitaruhusu au kuidhinisha kufidia kwa Serikali au mtu yeyote kwa misingi ya tendo lolote la ukiukaji wa sheria.

Draft for approval

**Sehemu ya – 5 Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya**

**Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya**

**59.** (1) Tume ya Haki za Kibinadamu na Usawa imeundwa.

(2) Majukumu ya Tume hii ni-

(a) kuendeleza kuheshimika kwa haki za binadamu na kuendeleza utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu katika Jamhuri;

(b) kuendeleza usawa wa kijinsia na usawazishaji kwa jumla, kuratibu na kuhakikisha jinsia imezingatiwa katika maendeleo ya kitaifa;

(c) kuimarisha na kulinda uzingativu wa haki za binadamu katika taasisi za umma na za kibinafsi;

(d) kufuatilia, kuchunguza na kuripoti uzingativu wa haki za binadamu katika nyanja zote za kitaifa zikiwemo idara za usalama wa kitaifa;

(e) kupokea na kuchunguza malalamiko kuhusu tuhuma za ukiukaji wa haki na hivyo basi kuchukua hatua za kupata marekebisho yanayofaa pale ambapo haki za binadamu zimekiukwa;

(f) kwa juhudi zake au kwa misingi ya malalamiko, kuchunguza au kutafiti juu ya haki za binadamu, na kutoa mapendekezo ya kuimarisha utendakazi wa mashirika ya Serikali;

(g) kuwa kama chombo kikuu cha Serikali katika kuhakikisha uzingativu wa majukumu yaliyo chini ya maagano na mikataba inayohusu haki za binadamu;

(h) kuchunguza mienendo yoyote katika masuala ya serikali, au kitendo au kosa katika utawala wa umma katika nyanja zote za serikali zinazotuhumiwa au kushukiwa kudhulumu au kutofaa, na kupelekea utovu wa nidhamu au dhuluma;

(i) kuchunguza malalamiko yoyote kuhusu mienendo ya afisa ambayo ni pamoja na matumizi mabaya ya mamlaka, matendo mabaya, dhihirisho la kutotenda haki au kuvunja sheria, au kunyanyasa, na kutoshughulika;

(j) kuripoti malalamiko yaliyochunguzwa katika aya ya (h) na (i) na kuchukua hatua za kurekebisha;

(k) kutekeleza jukumu lingine lolote linaloagizwa na sheria.

(3) kila mtu ana haki ya kulalamika kwa tume akidai kwamba haki na uhuru wa kimsingi katika Sheria ya Haki zimenyimwa, zimekiukwa, zimevunjwa au kutishiwa.

(4) Bunge litatunga sheria kutoa uwezo kamili wa sehemu hii, na sheria nyingine yoyote kama hii inaweza kupanga upya Tume hii na kuzifanya kuwa mbili au zaidi zilizotenganishwa.

(5) Iwapo Bunge litatunga sheria ya kupanga upya Tume chini ya ibara ya (4) -

(a) sheria hiyo itagawa kila jukumu la Tume iliyotajwa katika Kifungu hiki kwa tume moja au nyingine zinazoirithi.

(b) kila mojawapo ya tume hizi zilizorithi, itakuwa na mamlaka sawa na ile ya Tume ambayo imetajwa katika Kifungu hiki; na

(c) kila tume iliyorithi itakuwa tume kwa maana ya iliyoko katika Sura ya Kumi na Tano, na itakuwa na hadhi na mamlaka sawa na tume zilizo chini ya Sura hii.

Draft for approval

## SURA YA TANO

## ARDHI NA MAZINGIRA

### Sehemu ya 1- Ardhi

### Kanuni za sera ya ardhi

**60.** (1) Ardhi nchini Kenya itashikiliwa, kutumiwa na kusimamiwa katika misingi ya usawa, ufanisi, uzalishaji na uendelevu, na kwa mujibu wa kanuni zifuatazo-

(a) uwezo sawa wa kupata ardhi;

(b) usalama wa haki za ardhi;

(c) usimamizi endelevu na wa manufaa, wa rasilmali za ardhi;

(d) usimamizi wa ardhi kwa uwazi na kwa gharama ya kufaa;

(e) hifadhi na utunzaji bora wa maeneo muhimu kiekolojia;

(f) kumaliza ubaguzi wa kijinsia katika sheria, mila na desturi zinazohusiana na mali iliyomo katika ardhi hiyo; na

(g) kuhimiza jamii kutatua mizozo kuhusu ardhi kupitia mifumo ya kiasili inayoambatana na Katiba hii.

(2) Kanuni hizi zitatekelezwa kupitia kwa sera ya ardhi ya kitaifa inayoundwa na kuchunguzwa upya kila mara na serikali ya kitaifa kupitia kwa sheria.

Draft for approval

### Uainishaji wa ardhi

**61.** (1) Ardhi yote nchini Kenya ni ya Wakenya wote kama taifa, jamii na kama watu binafsi.

(2) Ardhi yote nchini Kenya inaainishwa kama mali ya umma, jamii au ya kibinafsi.

### Ardhi ya umma

**62.** (1) Ardhi ya umma ni-

(a) ardhi ambayo wakati wa kuanza kutumika kwa Katiba hii ni mali ya Serikali inavyoelezwa na Sheria ya Bunge wakati huo;

(b) ardhi inayomilikiwa, kutumiwa au kukaliwa kisheria na taasisi yoyote ya Serikali, isipokuwa pale ambapo ardhi hiyo inakaliwa na idara ya Serikali chini ya kukodi kibinafsi;

(c) ardhi iliyokabidhiwa Serikali kwa njia ya kuuza, kurudishiwa au kusalimishwa;

(d) ardhi ambayo haimilikiwi kisheria na mtu yeyote au jamii yoyote;

(e) ardhi ambayo mrithi wake hawezi kutambuliwa kwa vyovyote kisheria;

(f) ardhi yoyote iliyo na madini au mafuta inavyoelezwa kisheria;

(g) misitu ya Serikali kando na misitu inayotajwa katika Kifungu cha 63 (2) (d) (i), hifadhi ya wanyama, chemichemi za maji, mbuga za kitaifa, hifadhi za wanyama za serikali na sehemu maalum zilizolindwa;

(h) barabara zote kulingana na Sheria ya Bunge;

(i) mito yote, maziwa yote na sehemu nyingine za maji kama inavyoelezwa na Sheria ya Bunge;

(j) mipaka ya bahari, maeneo maalum ya kiuchumi na chini ya bahari;

(k) miamba ya kibara;

(l) ardhi yote kati ya nyanda za juu na za chini za maji;

(m) ardhi yoyote ambayo haijaainishwa kama ya kibinafsi au ya jamii chini ya Katiba hii; na

(n) ardhi yoyote itakayotangazwa kuwa ya umma na Sheria ya Bunge-

(i) itakayotumika katika tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii; na

(ii) iliyoidhinishwa baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(2) Ardhi ya umma itatolewa na kumilikiwa na Serikali ya Kaunti kwa amana kwa niaba ya wakazi wa Kaunti hiyo na itasimamiwa kwa niaba yao na Tume ya Kitaifa ya Ardhi iwapo imeainishwa chini ya-

(a) ibara ya (1) (a),(c), (d) au (e); na

(b) ibara ya (1)(b) mbali na ardhi inayoshikiliwa, inayotumiwa au inayomilikiwa na idara za Serikali ya kitaifa.

(3) Ardhi ya umma, inayoainishwa chini ya ibara ya (1) (f) hadi (m) itatolewa na kumilikiwa na Serikali ya kitaifa kwa amana kwa niaba ya wananchi wa Kenya na itasimamiwa kwa niaba yao na Tume ya Kitaifa ya Ardhi.

(4) Ardhi ya umma haitatolewa au kutumiwa isipokuwa kwa kuzingatia Sheria ya Bunge inayofafanua hali na masharti ya kutolewa au matumizi hayo.

**Ardhi ya jamii**

**63.** (1) Ardhi ya jamii itatolewa na kumilikiwa na jamii zinazotambuliwa kwa misingi ya kikabila, kitamaduni au mahitaji ya kijamii yanayofanana .

(2) Ardhi ya umma inahusisha-

(a) ardhi iliyosajiliwa kwa jina la wawakilishi wa kikundi kilicho chini ya masharti ya sheria yoyote;

Draft for approval

(b) ardhi yoyote iliyokabidhiwa jamii fulani kupitia kwa njia yoyote ya kisheria;

(c) ardhi nyingine yoyote itakayotangazwa na Sheria ya Bunge kama ardhi ya jamii; na

(d) ardhi ambayo-

(e) inamilikiwa kihalali , kusimamiwa au kutumiwa na jamii maalum kama misitu ya jamii, malisho ya mifugo au madhabahu;

(f) ardhi ya kinasaba na ardhi ambayo kitamaduni ilimilikiwa na jamii ya wawindaji; au

(g) kisheria inashikiliwa kama ardhi ya amana na serikali za Kaunti lakini isiyojumuisha ardhi ya umma iliyoshikiliwa kama amana na serikali za kaunti chini ya Kifungu cha 62 (2).

(3) Ardhi yoyote ya jamii ambayo haijasajiliwa itashikiliwa kwa amana na Serikali za kaunti kwa niaba ya jamii hizo.

(4) Ardhi ya jamii haitatolewa au kutumiwa vinginevyo isipokuwa kwa misingi ya sheria inayofafanua hali na viwango vya haki za kila mwanajamii kibinafsi au wanajamii wote kwa pamoja.

(5) Bunge litatunga sheria kuidhinisha utekelezwaji wa Kifungu hiki.

Draft for approval

**Ardhi ya kibinafsi**

**64.** Ardhi ya kibinafsi inajumuisha-

(a) ardhi yoyote iliyosajiliwa na inayomilikiwa na mtu yeyote chini ya umilikaji ardhi bila masharti;

(b) ardhi inayomilikiwa na mtu yeyote kwa kukodisha; na

(c) ardhi yoyote nyingine iliyotangazwa kuwa ya kibinafsi chini ya Sheria ya Bunge.

**Umilikaji Ardhi wa Wasio Raia**

**65.** (1) Mtu asiye raia anaweza kumiliki au kutumia ardhi kwa misingi ya kukodisha pekee, na mkataba huo hata ukitolewa hautazidi miaka tisini na tisa.

(2) Masikizano, makubaliano au uhawilisho wa aina yoyote unaompa mtu asiye raia wa Kenya uwezo wa kumiliki ardhi kwa zaidi ya miaka tisini na tisa utachukuliwa kwamba maafikiano hayo ni ya miaka tisini na tisa na wala sio zaidi.

(3) Kwa madhumuni ya Kifungu hiki-

(4) kampuni au shirika lolote litakubaliwa tu kama raia iwapo shirika hilo linamilikiwa kabisa na raia mmoja au zaidi;

(5) mali inayoshikiliwa kama amana itachukuliwa kama inayomilikiwa na raia iwapo tu faida ya manufaa yote ya amana hiyo inashikiliwa na raia.

(6) Bunge linaweza kutunga sheria kuweka masharti zaidi ya utekelezaji wa Kifungu hiki.

**Kanuni za matumizi ya ardhi na mali**

**66.** (1) Serikali inaweza kudhibiti matumizi ya ardhi yoyote au haki yoyote kuhusu ardhi kwa ajili ya ulinzi, usalama wa umma, mpangilio wa umma, maadili ya umma, afya ya umma, au mpango wa matumizi ya ardhi.

(2) Bunge litatunga sheria kuhakikisha kwamba uwekezaji katika mali ni kwa manufaa ya jamii na chumi zao.

**Tume ya Kitaifa ya Ardhi**

**67.** (1) Tume ya Kitaifa ya Ardhi imeundwa.

(2) Majukumu ya Tume ya Kitaifa ya Ardhi ni-

(a) kusimamia ardhi ya umma kwa niaba ya Serikali ya kitaifa na kaunti;

(b) kupendekezea Serikali ya kitaifa sera ya kitaifa kuhusu ardhi;

(c) kushauri Serikali ya kitaifa kuhusu utaratibu wa kina wa kusajili umiliki wa ardhi kote nchini.

(d) kufanya utafiti kuhusiana na ardhi na matumizi ya rasilmali nyingine za kiasili na kutoa mapendekezo kwa mamlaka yanayohusika;

(e) kuanzisha uchunguzi wake au kutokana na malalamiko kuhusu ukiuakaji haki uliopo au wa kihistoria kuhusu ardhi na kupendekeza suluhisho mwafaka;

(f) kuhimiza matumizi ya njia za kiasili zinazokubalika za kusuluhisha mizozo inayohusu ardhi;

(g) kutathmini ushuru unaotozwa ardhi na thamani ya mali isiyoweza kuhamishwa katika eneo lolote linalotambuliwa na sheria;

(h) kusimamia na kuwa na jukumu la kuangalia mpango wa matumizi ya ardhi nchini;

(3) Tume ya Kitaifa ya Ardhi inaweza kutekeleza majukumu mengine yatakayotolewa na sheria ya nchi.

Draft for approval

**Sheria kuhusu Ardhi**

**68.** (1) Bunge-

(a) litarekebisha, kuunganisha na kusawazisha sheria zilizopo kuhusu ardhi;

(b) litarekebisha sheria za kisekta kuhusu matumizi ya ardhi kwa mujibu wa kanuni zilizotajwa katika Kifungu cha 60 (1);

(c) litatunga sheria-

(i) kushauri kuhusu kiwango cha juu na cha chini cha ekari za ardhi ya kumilikiwa baada ya kuzingatia ardhi ya kibinafsi;

(ii) kudhibiti njia ambazo ardhi yoyote inaweza kubadilishwa kutoka kwenye ngazi moja hadi nyingine;

(iii) kudhibiti utambuaji na uhifadhi wa mali ya kindoa na hasa boma la kindoa wakati wa ndoa na wakati wa uvunjwaji wa ndoa hiyo;

(iv) kulinda, kuhifadhi na kutoa nafasi ya kupatikana kwa ardhi yote ya umma;

(v) kuwezesha kuchunguzwa upya kwa nafasi ya ardhi ya umma ili kuimarisha mali au uhalali wake;

(vi) kuwalinda wategemezi wa jamaa za wafu na haja ya kupata ardhi yakiwemo maslahi ya mume na mke wanaoishi katika ardhi;

(vii) kutoa nafasi kwa suala jingine lolote linalohitajika katika kuendeleza masharti ya Sura hii.

Draft for approval

**Sehemu ya 2- Mazingira na Maliasili**

**Kanuni na wajibu kuhusiana na mazingira**

**69.** Serikali –

(a) itahakikisha matumizi, usimamizi, na uhifadhi wa mazingira na maliasili unaodumishwa na kuhakikisha usawa katika ugavi wa faida zinazopatikana.

(b) itafanya juhudi ili kutimiza na kuhakikisha kuwa angalau asilimia kumi ya ardhi ya Kenya imepandwa miti;

(c) italinda na kukuza hakimiliki za rasilmali za kiakili na elimu ya jadi ya uanuwai wa viumbe na rasilmali za kinasaba za kuzaliwa za jamii;

(d) itahimiza kushiriki kwa umma katika usimamizi, utunzaji, na uhifadhi wa mazingira.

(e) italinda rasilmali zote za kinasaba na uanuwai wa kielimu viumbe;

(f) itaanzisha mifumo ya kutathmini athari ya mazingira, ukaguzi wa mazingira na usimamizi wa mazingira hayo;

(g) itatupilia mbali michakato na shughuli ambazo zinaweza kuhatarisha mazingira; na

(h) kutumia mazingira na maliasili kwa manufaa ya Wakenya.

(2) Kila mtu anawajibika kushirikiana na idara za Serikali na watu wengine kulinda na kuhifadhi mazingira na kuhakikisha kuna maendeleo ya kiekolojia na matumizi ya rasilmali.

**Utekelezwaji wa haki za mazingira**

**70.** (1) Iwapo mtu anadai kuwa haki ya kupata mazingira safi na yenye afya inayotambuliwa na kulindwa chini ya Kifungu cha 42 imekiukwa, inakiukwa au inaelekea kukiukwa, kunyimwa, kuvunjwa au kutishiwa, mtu huyo anaweza kuwasilisha kesi mahakamani ili asikilizwe mbali na hatua nyingine za kisheria zitakazoshughulikia suala hilo.

(2) Kutokana na ombi chini ya ibara ya (1), mahakama inaweza kutoa amri au maelekezo yanayostahili-

(a) kuzuia, kukomesha au kuachisha tendo au kosa lolote hatari kwa mazingira;

(b) kumshurutisha afisa yeyote wa umma kuchukua hatua ya kuzuia au kukomesha tendo au kosa lolote hatari kwa mazingira; ama

(c) kutoa fidia kwa mwathiriwa yeyote anayeathirika kutokana na ukiukaji wowote wa haki ya kupata mazingira safi na salama kiafya.

(3) Kwa madhumuni ya Kifungu hiki, haitakuwa lazima kwa anayetoa maombi kuonyesha kwamba mtu amepata hasara au kujeruhiwa.

Draft for approval

**Makubaliano kuhusiana na maliasili**

**71.** (1) Mapatano yoyote yanaweza kuidhinishwa na Bunge iwapo-

(a) yanahusisha utoaji wa haki au makubaliano na, au kwa niaba ya mtu yeyote, ikiwemo Serikali ya taifa kwa mtu mwingine, ya kutumia maliasili yoyote iliyo nchini Kenya; na

(b) yataafikiwa siku ya kuanza kutumia Katiba hii au baadaye.

(2) Kupitia utungaji wa sheria, Bunge litatoa viwango vya maafikiano yatakayoidhinishwa chini ya ibara ya (1).

**Sheria kuhusu Mazingira**

**72.** (1) Bunge litatunga sheria ya utekelezaji kamili wa masharti ya Sehemu hii.

## SURA YA SITA

## UONGOZI NA MAADILI

**Majukumu ya uongozi**

**73.** (1) Mamlaka yaliyotolewa kwa afisa wa Serikali-

(a) ni amana ya umma inayopaswa kutekelezwa katika njia ambayo-

(i) inaambatana na majukumu na makusudi ya Katiba hii;

(ii) inadhihirisha heshima kwa watu;

(iii) inaleta sifa katika taifa na hadhi kwenye afisi; na

(iv) inakuza imani ya umma katika maadili ya kiafisi; na

(b) yanampa afisa huyo wa Serikali jukumu la kuhudumia watu badala ya nguvu za kuwatawala.

(2) Kanuni zinazotoa mwongozo wa uongozi na maadili ni –

(a) uteuzi kwa misingi ya uadilifu, ustadi wa kufanya kazi, kufaa kwake, au uchaguzi huru na wa haki;

(b) kutopendelea katika maamuzi na katika kuhakikisha kwamba maamuzi hayo hayatokani na mapendeleo ya kindugu au nia zingine zozote mbaya au vitendo vya ufisadi;

(c) huduma za kujitolea kwa misingi hasa ya manufaa ya umma, ikidhihirishwa na –

(i) uaminifu katika utekelezaji wa wajibu kwa umma; na;

(ii) kutangaza maslahi ya kibinafsi yanayoweza kugongana na wajibu wake kwa umma;

(d) uwajibikaji kwa umma kuhusu maamuzi na hatua zinazochukuliwa; na

(e) nidhamu na kujitolea katika kuhudumia watu.

**Kiapo cha uaminifu kwa Maafisa wa Serikali**

**74.** Kabla ya kuhudumu katika afisi ya serikali , au kutekeleza majukumu yoyote ya afisi, kila mtu aliyechaguliwa au kuteuliwa katika afisi ya Serikali ataapa au kukiri kuwajibikia afisi hiyo katika njia na hali itakayopendekezwa na Mpangilio wa Tatu, au na Sheria ya Bunge.

Draft for approval

**Mienendo ya Maafisa wa Serikali**

**75.** (1) Afisa wa Serikali atakuwa na mienendo iliyonyooka, iwe katika maisha yake ya kuhudumia umma na afisi, katika maisha ya kibinafsi, au katika kuingiliana na watu wengine, yeye atapaswa kudumisha mienendo itakayomwepusha na-

(a) mgongano wowote kati ya maslahi ya kibinafsi na wajibu wake wa kuhudumia umma au afisi;

(b) ukiukaji wa maslahi yoyote ya umma au kiafisi kwa ajili ya maslahi yake ya kibinafsi; au

(c) kudhalilisha afisi au cheo anachoshikilia afisa huyo.

(2) Afisa wa Serikali anayetenda kinyume na ibara ya (1), au Kifungu cha 76, 77 au 78 (2)–

(a) atawekwa chini ya taratibu za kinidhamu zinazotumika kwa afisi inayohusika;

(b) kulingana na taratibu za kinidhamu zilizotajwa katika aya ya (a), anaweza kuachishwa kazi au vinginevyo, kuondolewa afisini.

(3) Mtu ambaye ameachishwa kazi au vinginevyo kutolewa afisini kwa kukiuka vipengele vilivyotajwa katika ibara ya (2) atapigwa marufuku kushikilia afisi yoyote nyingine ya Serikali.

Draft for approval

**Uadilifu wa kifedha kwa Maafisa wa Serikali**

**76.** (1) Zawadi au mchango wowote kwa afisa wa Serikali katika shughuli za umma au rasmi, itakuwa zawadi kwa Jamhuri na itakabidhiwa Serikali isipokuwa ikiidhinishwa na au chini ya Sheria ya Bunge.

(2) Afisa wa Serikali –

(a) hatamiliki akaunti ya benki nje ya Kenya isipokuwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge; au

(b) hataomba au kukubali mkopo au manufaa ya kibinafsi katika hali zinazotatiza uadilifu wake.

**Vizuizi katika shughuli za maafisa wa serikali**

**77.** (1) Afisa wa Serikali ambaye ni mtumishi wa kudumu hatashiriki kazi nyingine yoyote ya kulipwa.

(2) Afisa yeyote wa Serikali wa kuteuliwa hatashikilia afisi ya chama cha kisiasa.

(3) Afisa wa Serikali aliyestaafu na anayepokea malipo ya uzeeni kutoka katika fedha za umma, hatakubali zaidi ya nyadhifa mbili za kulipwa mshahara kwa wakati mmoja kama mwenyekiti, mkurugenzi au mwajiriwa wa-

(a) kampuni inayomilikiwa au kudhibitiwa na Serikali; na

(b) idara ya Serikali.

(4) Afisa wa Serikali aliyestaafu hatapokea mshahara kutoka katika fedha za umma isipokuwa kama inavyoelezwa katika ibara ya (3).

**Uraia na uongozi**

**78**. (1) Hakuna mtu anayepaswa kuchaguliwa au kuteuliwa katika afisi ya Serikali ikiwa si raia wa Kenya.

(2) Afisa wa Serikali au afisa mlinda usalama hatakuwa na uraia mara mbili.

(3) Ibara za (1) na (2) hazitatumika kwa-

(a) Majaji na wanachama wa tume; au

(b) mtu yeyote ambaye amekuwa raia wa nchi nyingine na kwa utekelezaji wa sheria ya nchi hiyo, hana uwezo wa kutoka.

**Sheria ya kuundwa kwa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi**

**79.** Bunge litatunga sheria ya kubuniwa kwa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi, ambayo itakuwa na hadhi na mamlaka sawa na tume iliyo chini ya Sura ya Kumi na Tano, kwa nia ya kuhakikisha utimizaji na utekelezaji wa masharti ya Sura hii.

**Sheria kuhusu uongozi**

**80.** Bunge litatunga sheria –

(a) kubuni taratibu na mikakati ya kutekeleza sura hii kwa njia ifaayo;

(b) kupendekeza adhabu zaidi ya zile zinazotajwa katika Kifungu cha 75, ambazo zinaweza kuamriwa kwa sababu ya kutofuata maagizo ya Sura hii;

(c) kusaidia katika utekelezaji wa Sura hii pakiwa na marekebisho yanayofaa kwa maafisa wa umma; na

(d) kuunda masharti mengine yoyote katika kuhakikisha udumishaji wa kanuni za uongozi na uadilifu ambayo yametajwa katika Sura hii, na utekelezaji wa masharti ya Sura hii.

Draft for approval

## SURA YA SABA

## UWAKILISHI WA WATU

**Sehemu ya 1 – Mfumo na utaratibu wa uchaguzi**

**Kanuni za jumla za mfumo wa uchaguzi**

**81.** Mfumo wa uchaguzi utazingatia kanuni zifuatazo-

(a) uhuru wa raia wa kutekeleza haki zao za kisiasa chini ya Ibara ya 38;

(b) sio zaidi ya thuluthi mbili ya wanachama wa mashirika ya umma yatakayoshiriki uchaguzi wa wanachama watakuwa ya jinsia sawa;

(c) uwakilishi wenye usawa wa watu walio na ulemavu;

(d) haki ya kupiga kura kwa wote katika misingi ya haki ya uwakilishwaji na usawa wa kura; na

(e) chaguzi za haki na usawa, ambazo ni -

(i) za kura ya siri;

(ii) huru na zisizo na ghasia, vitisho, ushawishi usiofaa, au ufisadi;

(iii) zinazoendeshwa na halmashauri huru;

(iv) wazi; na

(v) zinazofanywa kwa njia zisizopendelea upande wowote, katikati, bora, kamilifu na zilizo na uwajibikaji.

Draft for approval

**Sheria kuhusu uchaguzi**

**82.** (1) Bunge litatunga sheria ya kutoa nafasi ya-

(a) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kuamua idadi ya maeneo-bunge kuhusu maeneo ya uchaguzi kwa wanachama wa Baraza la Kitaifa na mabaraza ya kaunti;

(b) uteuzi wa wagombeaji;

(c) usajili wa mara kwa mara wa raia kama wapiga kura;

(d) hali ya chaguzi na kura za maamuzi. Uendeshaji na usimamizi bora wa chaguzi na kura za maamuzi ikiwa ni pamoja na uteuzi wa wagombeaji wa uchaguzi; na

(e) usajili wa mara kwa mara wa raia wanaoishi nje ya Kenya, kama wapiga kura na kuzifahamu haki zao za kupiga kura.

(2) Sheria inayotakikana na ibara ya (1) (d) itahakikisha kwamba upigaji kura katika kila uchaguzi ni-

(a) rahisi;

(b) wazi; na

(c) inazingatia mahitaji maalumu ya-

(i) watu wenye ulemavu; na

(ii) watu wengine ama vikundi vya watu walio na mahitaji maalumu.

**Kusajiliwa kama mpiga kura**

**83.** (1) Mtu anastahili kusajiliwa kama mpiga kura katika chaguzi au kura za maamuzi kama mtu huyo ni raia mtu mzima; hajatangazwa kuwa na akili punguwani; na hajapatikana na hatia ya uchaguzi katika kipindi cha miaka mitano iliyotangulia.

(2) raia anayestahili kusajiliwa kama mpigakura atasajiliwa kwenye kituo kimoja tu cha usajili wa kupigia kura.

(3) mipango ya kiusimamizi ya usajili wa wapiga kura na uendeshaji wa chaguzi, itapangwa ili kurahisisha, na haitamnyima raia yeyote anayestahili haki ya kupiga kura au kugombea uchaguzi.

Draft for approval

**Wagombea uchaguzi na vyama vya kisiasa kuzingatia kanuni za upigaji kura**

**84.** Katika kila uchaguzi, wagombea uchaguzi wote na vyama vyote vya kisiasa vitazingatia kanuni za upigaji kura zilizowekwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

**Ustahili wa kusimama kama mgombea wa kibinafsi**

**85.** Mtu yeyote anastahili kusimama kama mgombea uchaguzi wa kujitegemea, ikiwa mtu huyo-

(a) si mwanachama wa chama cha kisiasa kilichosajiliwa na hajakuwa mwanachama kwa angalau kwa kipindi cha miezi mitatu kabla ya tarehe ya uchaguzi; na

(b) anatimiza masharti ya-

(i) Kifungu cha 99 (1) (c) (i) au (ii), kwa mgombeaji wa uchaguzi wa Baraza la Kitaifa au Seneti, mtawalia; au

(ii) Kifungu cha sheria cha 193 (1) (c) (ii), kwa mgombeaji wa uchaguzi wa bunge la kaunti.

**Upigaji kura**

**86.** Katika kila uchaguzi, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itahakikisha kwamba-

(a) katika njia yoyote ya upigaji kura itakayotumiwa, mfumo unakuwa rahisi, sahihi, wa kuthibitika, salama, unaowajibika na ulio na uwazi;

(b) kura zinazopigwa zinahesabiwa, kuorodheshwa na matokeo kutangazwa moja kwa moja na afisa msimamizi wa kituo cha upigaji kura hapo kituoni;

(c) matokeo kutoka kwa vituo vingine vya upigaji kura yanajumlishwa kwa uwazi na kutangazwa moja kwa moja na afisa msimamizi wa kituo cha upigaji kura; na miundo na taratibu mwafaka zimewekwa ili kuondoa uwezekano wa kuhusishwa kwa mienendo yoyote mibaya, ukiwemo uhifadhi salama wa vifaa vya uchaguzi.

**Mizozo ya uchaguzi**

**87.** (1) Bunge litatunga sheria ya kubuniwa kwa mifumo ya kusuluhishwa kwa haraka mizozo ya uchaguzi.

(2) Malalamiko kuhusu uchaguzi, isipokuwa uchaguzi wa urais, yatawasilishwa katika kipindi cha siku ishirini na nane baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

(3) Kukabidhiwa kwa mashtaka hayo kunaweza kuwa kwa moja kwa moja au kupitia kwa tangazo katika gazeti linalosambazwa kote nchini.

Draft for approval

**Sehemu ya 2 - Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka**

**Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka**

**88.** (1) Kutabuniwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

(2) Mtu hastahili kuteuliwa kama mwachama wa Tume, ikiwa mtu huyo-

(a) ashawahi kushikilia afisi au kugombea uchaguzi katika kipindi cha miaka mitano iliyotangulia kama -

(i) mbunge katika ama mbunge kwenye bunge la kaunti; au

(ii) mwanachama wa taasisi ya kiserikali inayosimamia chama cha kisiasa; au

(b) anashikilia afisi yoyote ya taifa.

(3) Mwanachama wa Tume hatashikilia afisi nyingine ya umma.

(4) Tume inawajibika kuendesha na kusimamia kura za maamuzi na chaguzi katika taasisi zote zinazofanya uchaguzi au afisi zilizobuniwa na Katiba hii, na chaguzi nyingine zozote kama zilivyoagizwa na kifungu cha Sheria ya Bunge na hususan, katika-

(a) usajili wa mara kwa mara wa raia kama wapiga kura;

(b) usahihishaji wa mara kwa mara kwa kitabu cha usajili ya wapiga kura;

(c) kuweka mipaka ya maeneobunge na wadi;

(d) kudhibiti taratibu ambazo vyama hutumia kuteua wagombea uchaguzi;

(e) kusuluhisha mizozo ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na mizozo inayohusiana na au kutokana na uteuzi lakini isiyohusisha malalamiko ya uchaguzi na mizozo inayotokana na kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi;

(f) kusajili wagombea uchaguzi;

(g) elimu ya mpigakura;

(h) kuwezesha uchunguzi, usimamizi na tathmini ya chaguzi;

(i) kudhibiti kiwango cha fedha zinazoweza kutumiwa na au kwa niaba ya mgombea au chama katika uchaguzi wowote;

(j) kujenga kanuni za uchaguzi kwa wagombea na vyama vinavyogombea uchaguzi katika uchaguzi; na

(k) kuchunguza utimizaji wa sheria inayotakikana chini ya Kifungu cha 82 (1)

(l) kuhusiana na uteuzi wa wagombea wa vyama.

(5) Tume itatumia mamlaka yake kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba hii na sheria ya kitaifa iliyotungwa bungeni.

**Kuwekea mipaka maeneo ya uchaguzi**

**89.** (1) Kutakuwa na maeneobunge mia mbili tisini kwa lengo la uchaguzi wa wabunge wa Baraza la Kitaifa kama ilivyotajwa katika Kifungu cha 97 (1) (a).

(2) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itarekebisha upya majina na mipaka ya maeneobunge kila baada ya muda usiopungua miaka minane na usiozidi miaka kumi na miwili, lakini marekebisho yoyote lazima yakamilishwe angalau miezi kumi na miwili kabla ya uchaguzi mkuu wa wabunge.

(3) Tume itarekebisha upya mara kwa mara idadi, majina na mipaka ya wadi.

(4) Ikiwa uchaguzi mkuu utafanyika katika kipindji cha miezi kumi na miwili baada ya kukamilika kwa marekebisho yatakayoendeshwa na Tume, mipaka hiyo mipya haitatekelezeka kwa ajili ya uchaguzi huo.

(5) Mipaka ya kila eneobunge italinganishwa kwa, inakaribiana sana, sawa na idadi ya wakazi katika eneobunge hilo, lakini idadi ya wakazi wa eneobunge inaweza kuwa kubwa au ndogo kuliko idadi ya kiasi cha watu kwa namna ambayo imetajwa katika Ibara ya (6) ili kuzingatia-

Draft for approval

(a) hali ya kijiografia na maeneo ya miji;

(b) jamii ya eneo lile, kihistoria, kiuchumi na mshikamano wake wa kitamaduni; na

(c) mbinu za mawasiliano.

(6) Idadi ya wakazi wa eneobunge au wadi inaweza kuwa kubwa au ndogo zaidi ya idadi ya watu kwenye eneo hilo kwa kiwango kisichozidi-

(a) asilimia arubaini kwa majiji na maeneo yaliyo na idadi ya watu iliyotawanyika; na

(b) asilimia thelathini kwa sehemu nyingine.

(7) Katika kurekebisha mipaka ya maeneobunge na wadi, Tume-

(a) itashauriana na makundi yote husika; na

(b) itandelea kufanya kazi kwa lengo la kuhakikisha kwamba idadi ya watu katika kila eneobunge na wadi, inakaribiana, sawa na idadi ya watu wa eneo hilo iliyokadiriwa.

(8) Ikiwezekana, Tume hii itabadilisha majina na mipaka ya maeneobunge na wadi, na idadi, majina na mipaka ya wadi.

(9) Kulingana na Ibara ya (1) (2),(3) na (4), majina na maelezo ya kina kuhusu mipaka ya maeneobunge na wadi iliyobuniwa na Tume, itachapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali, na itatekelezwa baada ya kuvunjwa kwanza kwa Bunge, kufuatia kuchapishwa kwake.

(10) Mtu anaweza kutuma maombi kwa Mahakama Kuu ili kubatilisha maamuzi yaliyo chini ya kifungu hiki na yaliyotolewa na Tume.

Draft for approval

(11) Ombi la kurekebisha maamuzi yaliyotolewa chini ya Kifungu hiki, litatumwa katika kipindi cha siku thelathini baada ya uchapishaji wa uamuzi uliopo kwenye Gazeti Rasmi la Serikali na litasikilizwa na kuamriwa katika kipindi cha miezi mitatu kutoka siku ya kuwasilishwa kwa ombi hilo.

(12) kwa sababu ya Kifungu hiki, ‘ idadi ya watu’ ina maana ya idadi inayopatikana baada ya kugawa idadi ya watu wanaoishi Kenya kwa idadi ya maeneobunge au wadi, ifaavyo, kwa namna ambayo, Kenya ilivyogawanywa chini ya Kifungu hiki.

**Ugawaji wa orodha ya viti vya chama**

**90**. (1) Uchaguzi wa viti bungeni uliotolewa chini ya Kifungu cha 97 (1) (c) na 98 (1) (b), (c) na (d), na wanachama wa baraza la kaunti chini ya kifungu cha 177 (1) (b) na (c),utakuwa kwa misingi ya ushirikishwaji sawa kwa kutumia orodha za vyama.

(2) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itawajibika katika kuendesha na kusimamia chaguzi za viti vilivyotolewa chini ya Ibara ya (1) na itahakikisha kwamba-

(a) kila chama cha kisiasa kinachoshiriki katika uchaguzi mkuu kitateua na kuwasilisha orodha ya majina ya watu wote ambao wangalichaguliwa iwapo chama hicho kingalipewa viti vyote kama ilivyo chini ya Ibara ya (1), kwa wakati ulioagizwa kupitia sheria ya kitaifa;

(b) isipokuwa kwenye viti vilivyoelezewa chini ya Kifungu cha cha 98 (1) (b), kila orodha ya vyama ina idadi kamilifu ya wagombeaji wanaostahili na hubadilishana kati ya wagombeaji wanaume na wanawake kulingana na jinsi walivyoorodheshwa ; na

(c) isipokuwa kwenye viti vya baraza la kaunti, kila orodha ya chama inaakisi tofauti za kimaeneo na uanuwai wa kikabila wa Wakenya.

(3) Viti vilivyotajwa katika ibara ya (1) vitagawiwa vyama vya kisiasa kwa kulingana na idadi ya jumla ya viti walivyoshinda wagombeaji wa chama cha kisiasa katika uchaguzi mkuu.

**Sehemu ya 3- Vyama vya Kisiasa**

**Kanuni za kimsingi kwa vyama vya kisiasa**

**91.** (1) Kila chama cha kisiasa-

(a) kitakuwa na sifa za kitaifa kama inavyopendekezwa na Sheria ya Bunge;

(b) kiwe na taasisi ya kiutawala iliyochaguliwa kidemokrasia;

(c) kitadumisha na kukuza umoja wa kitaifa;

(d) kitazingatia kanuni za kidemokrasia za utawala bora, kudumisha na kuendeleza demokrasia kupitia kwa uchaguzi wa mara kwa mara, ulio na haki na huru katika chama;

(e) kitaheshimu haki za kila mtu ili kushiriki katika harakati za kisiasa, yakiwemo makundi ya walio wachache na wale waliotengwa;

(f) kitaheshimu na kudumisha haki za binadamu na uhuru wa kimsingi, na usawa wa kijinsia na usawazishaji;

(g) kitadumisha malengo na kanuni za Katiba hii na utawala wa sheria; na

(h) kitazingatia kanuni za maadili ya vyama vya kisiasa.

(2) Chama cha kisiasa –

(a) hakitabuniwa kwa misingi ya kidini, lugha, mbari, kabila, jinsia au kwa misingi ya kimaeneo au kujihusisha katika kampeni za kusambaza chuki na shihata katika misingi ya masuala mengine kama hayo;

Draft for approval

(b) hakitajihusisha na au kuchochea ghasia kwa, au vitisho kwa, wanachama wake, wafuasi, wapinzani au mtu mwingine yeyote;

(c) hakitaanzisha au kufadhili vikosi vya jeshi la wanamgambo wa kuvizia, makundi haramu au mashirika mengine kama hayo;

(d) hakitajihusisha katika utoaji hongo au aina nyingine za ufisadi; au

(e) isipokuwa kwa jinsi ilivyoelezwa katika Sura hii au kwa mujibu wa Sheria ya Bunge, kukubali au kutumia rasilimali ya umma ili kuimarisha maslahi yake au wagombeaji wake katika uchaguzi.

**Sheria ya vyama vya kisiasa**

**92.** Bunge litatunga sheria ambayo itatoa -

(a) nafasi sawa ya kutengewa muda katika vyombo vya habari, vinavyomilikiwa na Serikali au aina ya vyombo vinginevyo vya utangazaji, kwa vyama vya kisiasa wakati wowote au wakati wa kampeni za uchaguzi; na

(b) udhibiti wa uhuru wa kutangaza ili kuhakikisha kampeni zilizo na haki wakati wa uchaguzi;

(c) udhibiti wa vyama vya kisiasa;

(d) majukumu na utendakazi wa vyama vya kisiasa;

(e) usajili na usimamizi wa vyama vya kisiasa;

(f) uundwaji na uongozi wa hazina ya vyama vya kisiasa;

(g) akaunti na ukaguzi wa hesabu za vyama vya kisiasa;

(h) masharti kuhusu matumizi ya rasilimali ya umma ili kuendeleza maslahi ya vyama vya kisiasa; na

(h) masuala mengine muhimu ya kuongoza vyama vya kisiasa.

Draft for approval

Draft for approval

## SURA YA NANE

## BUNGE

### Sehemu ya 1 – Kuundwa na jukumu la Bunge

**Kuundwa kwa Bunge**

**93.** (1) Kutaundwa Bunge Kenya, litakalohusisha Seneti na Baraza la Kitaifa.

(2) Baraza la Kitaifa na Seneti zitatekeleza majukumu yao mahususi kwa mujibu wa Katiba hii.

**Jukumu la Bunge**

**94.** (1) Mamlaka ya utungaji wa sheria ya Jamhuri hii inatokana na wananchi na katika kiwango cha kitaifa, yamekabidhiwa kwa na kutekelezwa na Bunge.

(2) Bunge hufuatilia uanuwai wa taifa, huwakilisha nia ya wananchi, na hutekeleza Mamlaka yao.

(3) Bunge linaweza kukubali na kupitisha marekebisho kwenye Katiba hii na kubadilisha mipaka ya kaunti kama inavyoagizwa katika Katiba hii;

(4) Bunge litalinda Katiba hii na kudumisha utawala wa kidemokrasia katika Jamhuri hii.

(5) Hakuna mtu yeyote au asasi yoyote, isipokuwa Bunge, itakayokuwa na mamlaka ya kuunda masharti yatakayokuwa na nguvu za kisheria nchini Kenya isipokuwa kwa amri ya Katiba hii iliyokabidhiwa Bunge au kwa Sheria ya Bunge.

(6) Sheria ya Bunge, au sheria ya kaunti, inayoipatia asasi yoyote ya Serikali, afisa wa Serikali, au mtu yeyote mamlaka ya kutunga masharti au sheria na kuipatia nguvu za kisheria nchini Kenya, kama inavyokusudiwa katika Ibara ya (5), itaeleza bayana na kwa hakika shabaha na malengo ya kukabidhiwa mamlaka haya, viwango vya mamlaka, hali na upeo wa sheria zitakavyotungwa, na kanuni na viwango vya ubora vinavyotumika kisheria na vilivyobuniwa chini ya mamlaka haya.

**Majukumu ya Baraza la Kitaifa**

**95.** (1) Baraza la Kitaifa linawakilisha watu wa maeneobunge na walio na maslahi maalumu katika Baraza la Kitaifa.

(2) Baraza la Kitaifa hushauriana kuhusu na kusuluhisha masuala yenye umuhimu mkubwa kwa watu.

(3) Baraza la Kitaifa linatunga sheria kwa kuzingatia Sehemu ya 4 ya Sura hii.

(4) Baraza la Kitaifa -

(a) hubainisha ugavi wa mapato ya kitaifa kati ya ngazi za Serikali, kama inavyoagizwa katika Sehemu ya 4 ya Sura ya Kumi na Mbili;

(b) hugawa hazina ya fedha kwa matumizi ya Serikali ya kitaifa na asasi nyingine za Serikali ya kitaifa; na

(c) hutekeleza usimamizi wa jumla wa mapato ya kitaifa pamoja na matumizi yake.

(5) Baraza la Kitaifa-

(a) linachunguza utendakazi wa Rais afisini, Naibu wa rais na maafisa wengine wa Serikali na ikiwezekana kuchukua hatua za kuwatoa afisini; na

(b) litasimamia asasi za Serikali;

(6) Baraza la Kitaifa litaidhinisha tangazo la vita na kutathmini ongezeko la hali ya hatari nchini.

**Jukumu la Seneti**

**96.** (1) Seneti inawakilisha kaunti na inatumika kulinda maslahi ya kaunti na serikali zake;

(2) Seneti inashiriki katika jukumu la Bunge la uundaji wa sheria kwa kuamua, kujadiliana, kuidhinisha miswada inayohusu kaunti kama ilivyo katika Kifungu cha 109 hadi 113.

(3) Seneti ndio huamua ugavi wa mapato ya kitaifa miongoni mwa kaunti kama ilivyo katika Kifungu cha 217, na kutekeleza usimamizi jumla wa mapato ya kitaifa iliyotengewa kwa serikali za kaunti.

(4) Seneti inashiriki katika usimamizi wa maafisa wa Serikali na kutathmini na kutoa maamuzi kuhusu hoja ya kumuondoa Rais au Naibu wa rais kutoka kwenye wadhifa wake kwa mujibu wa Kifungu cha 145.

**Sehemu ya 2 – Uhusika na Uanachama wa Bunge**

**Uanachama wa Baraza la Kitaifa**

**97.** (1) Baraza la Kitaifa litajumuisha –

(a) wanachama mia mbili tisini waliochaguliwa na wapigakura, kila mmoja wao akiwa amechaguliwa na wapigakura waliosajiliwa kwa eneobunge moja lililo mwanachama;

(b) wanawake arobaini na saba, kila mmoja wao akiwa amachaguliwa na wapigakura waliosajiliwa kwenye kaunti, kila kaunti ikihusisha mwanachama mmoja wa eneobunge;

(c) wanachama kumi na wawili walioteuliwa na vyama vya kisiasa vya bunge kulingana na usawa wa wanachama wa Baraza la Kitaifa kwa mujibu wa Kifungu

Draft for approval

cha 90, kuwakilisha maslahi ya watu maalumu ikiwa ni pamoja na vijana, watu wenye ulemavu na wafanyakazi; na

(d) Spika, ambaye ni mwanachama m'badala .

(2) Hakuna kifungu chochote katika Kifungu hiki kinachoweza kufasiriwa kama kumuondoa mtu yeyote katika ugombea uchaguzi chini ya ibara ya (1) (a).

**Uanachama wa Seneti**

**98.** (1) Seneti itajumuisha-

(a) wanachama arobaini na saba, kila mmoja wao akiwa amechaguliwa na wapigakura waliosajiliwa kwenye kaunti, na kila kaunti ikiwa ni eneowakilishi la mwanachama mmoja;

(b) wanachama wanawake kumi na sita watakaoteuliwa na vyama vya kisiasa kulingana na usawa wao wa wanachama kwenye Seneti waliochaguliwa chini ya ibara ya (a) kwa mujibu wa Kifungu cha 90;

(c) wanachama wawili wakiwa mwanamume mmoja na mwanamke mmoja ili kuwakilisha vijana;

(d) wanachama wawili wakiwa mwanamume mmoja na mwanamke mmoja wakiwakilisha watu wenye ulemavu; na

(e) Spika atakayekuwa mwanachama m'badala kwa mujibu wa wadhifa wake.

(2) Wanachama waliotajwa katika ibara ya (1) (c) na (d) watachaguliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 90.

(3) Hakuna chochote katika Kifungu hiki kitafasiriwa kama kinachomuondoa mtu yeyote katika ugombeaji wa uchaguzi chini ya ibara ya (1) (a).

Draft for approval

**Sifa za kufaa na kutofaa katika kuchaguliwa kama Mbunge**

**99.** (1) Isipokuwa wakati mtu amepigwa marufuku katika ugombeaji chini ya Ibara ya (2), mtu anaweza kuchaguliwa kama mbunge iwapo mtu huyo-

(a) amesajiliwa kama mpigakura;

(b) anaafiki kiwango chochote cha kielimu, kimaadili na ana uadilifu kama inavyoagizwa kwenye Katiba hii au na Sheria ya Bunge; na

(c) ameteuliwa na chama cha kisiasa au mgombeaji wa kujitegemea anayedhaminiwa -

(i) na angalau wapigakura elfu moja waliosajiliwa katika eneobunge katika uchaguzi wa Baraza la Kitaifa; na

(ii) na angalau wapigakura elfu mbili waliosajiliwa katika kaunti kwa uchaguzi

wa Seneti.

(2) Mtu hastahili kuchaguliwa kama mbunge ikiwa mtu huyo-

(a) anashikilia jukumu lolote la Serikali au afisi mwingine wa umma, licha ya kuwa Mbunge;

(b) amekuwa, katika kipindi cha miaka mitano inanayotangulia taratibu za uchaguzi, ameshawahi kushikilia afisi kama mwanachama wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka;

(a) hakuwa raia wa Kenya kwa angalau miaka kumi inayotangulia tarehe ya uchaguzi;

(b) ni mwanachama wa Baraza la Kaunti;

(c) hana akili timamu;

(d) mufilisi ;

(e) anakabiliwa na hukumu ya kifungo cha miezi sita gerezani, kuanzia siku ya kujiandikisha kama mgombeaji, au katika tarehe ya uchaguzi; au

(f) amepatikana, kwa mujibu wa sheria yoyote, kutumia vibaya afisi ya Serikali au ya umma ama kwa njia yoyote alikiuka kanuni za Sura ya Sita.

(3) Mtu hazuiliwi chini ya ibara ya (2) isipokuwa tu pale ambapo uwezekano wote wa rufaa au kubadilishwa kwa kifungo kinachofaa ama pamekosekana maamuzi mengine.

Draft for approval

**Kukuza uwakilishi wa makundi yaliyotengwa**

**100.** Bunge litatunga sheria kuimarisha uwakilishwaji Bungeni wa-

(a) wanawake;

(b) watu wenye ulemavu;

(c) vijana;

(d) makabila na wengine walio wachace; na

(e) jamii iliyotengwa.

**Uchaguzi wa Wabunge**

**101.** (1) Uchaguzi mkuu wa wabunge utafanyika Jumanne ya pili ya mwezi wa Agosti katika kila mwaka wa tano.

(2) panapotokea nafasi katika afisi ya mbunge wa Baraza la Kitaifa, lililotajwa chini ya Kifungu cha 97 (1) (c), au katika Seneti chini ya Kifungu cha 98 (1) (b), (c) ama

(d), Spika mhusika, katika kipindi cha siku ishirini na moja za kutokea nafasi hiyo ya kazi, atatoa notisi kwa maandishi kuhusu nafasi hiyo ya kazi kwa-

(a) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka; na

(b) chama cha kisiasa ambacho kupitia kwa orodha yake ya chama ndipo mwanachama huyo alipokuwa amechaguliwa au kuteuliwa.

(3) Nafasi hiyo iliyotajwa katika Ibara ya (2) kwa, kuambatana na Ibara ya (5), itajazwa kwa namna iliyoagizwa na Sheria ya Bunge ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya kutangazwa na Spika mhusika.

(4) Panapotokea nafasi ya kazi katika afisi ya mwanachama wa Baraza la Kitaifa aliyechaguliwa chini ya Kifungu cha 97 (1) (a) au (b), au wa Seneti aliyechaguliwa chini ya Kifungu cha 98 (1) (a)-

(a) Spika mhusika, kwa muda wa siku ishirini na moja baada ya kutokea kwa nafasi hii, atatoa notisi kuhusu nafasi hii kwa kuiandikia Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka; na

(b) uchaguzi mdogo utafanyika katika muda wa siku tisini baada ya kutokea kwa nafasi hiyo ya kazi, kuambatana na ibara ya (5).

(5) Nafasi iliyotajwa katika ibara ya (4) haitajazwa katika kipindi cha miezi mitatu inayotangulia uchaguzi mkuu.

Draft for approval

**Muhula wa Bunge**

**102.** (1) Muhula wa kila Bunge humalizika mnamo tarehe ya uchaguzi mkuu unaofuata.

(2) Wakati Kenya iko kwenye vita, mara kwa mara Bunge, kwa maamuzi yalioungwa mkono na angalau wabunge wasiopungua thuluthi mbili ya wabunge wote katika kila kitengo cha bunge, linaweza kuongeza kipindi cha Bunge kwa muda usiozidi miezi sita kwa wakati huo.

(3) muhula wa bunge hautaongezwa chini ya ibara ya (2) kwa jumla ya zaidi ya miezi kumi na miwili.

**Kuondoka afisini kwa Mbunge**

**103.** (1) Afisi ya mbunge itakuwa wazi-

(a) ikiwa mbunge huyo amefariki;

(b) ikiwa, katika kipindi cha mbunge huyo anakosekana katika vikao vinane mfululizo vya bunge husika, bila ruhusa ya Spika wa kitengo chake cha bunge kwa maandishi, na hatoi sababu ya kuridhisha ya kutohudhuria kwake kwa kamati husika;

(c) ikiwa kwa vinginevyo mbunge huyo ataondolewa afisini chini ya Katiba hii au

sheria iliyotungwa chini ya Kifungu cha 80;

(d) ikiwa mbunge huyo atajiuzulu kwa kumwandikia barua Spika;

(e) ikiwa, ameshachaguliwa katika Bunge-

(i) kama mwanachama wa chama cha kisiasa, mwanachama huyu anajiuzulu kutoka kwa chama au angefaa kujiuzulu kutoka kwa chama kama inavyoamriwa kwa mujibu wa sheria inayozingatiwa na ibara ya (2); au

(ii) kama mgombea uchaguzi wa kibinafsi, anajiunga na chama cha kisiasa.

(f) baada ya kukamilika kwa muhula wa Bunge husika;

(g) ikiwa mbunge huyo ataondolewa katika ugombeaji wa kuchaguliwa Bungeni chini ya Kifungu cha 99 (2) (d) hadi (h).

(2) Bunge litatunga sheria ili kuruhusu hali ambazo mwanachama wa chama cha kisiasa atachukuliwa kama, kwa makusudi ya ibara ya (1) (e), aliyejiuzulu kutoka kwa chama.

Draft for approval

**Haki ya kumwondoa mamlakani mbunge**

**104.** (1) Wapiga kura chini ya Vifungu vya 97 na 98, wana haki ya kumuondoa mamlakani mbunge waliyemchagua ili kuwakilisha eneobunge kabla ya kukamilika kwa kipindi cha Bunge.

(2) Bunge litatunga sheria inayoorodhesha sababu za kufaa na taratibu zitakazofuatwa za kumuondoa mbunge mamlakani.

**Kutathmini maswali kuhusu ubunge**

**105.** (1) Mahakama Kuu itasikiliza na kuamua kuhusu lalamiko lolote la iwapo-

(a) mtu amechaguliwa kama mbunge kwa njia halali; au

(b) iwapo kiti cha mbunge kimekuwa wazi.

(2) Malalamiko yaliyotajwa katika ibara ya (1) yatasikilizwa na kuamuliwa katika muda wa miezi sita kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa malalamiko.

(3) Bunge litatunga sheria kutoa utekelezaji kamili wa Kifungu cha hiki.

**Sehemu ya 3 - Afisi za Bunge**

**Maspika na Manaibu Spika wa Bunge**

**106.** (1) Kutakuwa na-

(a) Spika wa kila kitengo cha Bunge, atakayechaguliwa na kitengo hicho kulingana na Kanuni za Kuendesha Bunge, kutoka miongoni mwa watu walio na sifa zinazostahili kuchaguliwa kama wabunge na ambao si wabunge; na

(b) Naibu Spika wa kila Bunge, atakayechaguliwa na Bunge hilo kwa mujibu wa Kanuni za Kuendesha Bunge, kutoka miongoni mwa wabunge.

(2) Afisi ya Spika au Naibu wa Spika itakuwa wazi-

(a) wakati Bunge litakapokutana kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi;

(b) iwapo anayeshikilia afisi, kama mwanachama wa Bunge husika, anaondoka afisini chini ya Kifungu cha 103;

(c) iwapo Bunge husika linaamua kwa uamuzi ulioungwa mkono na angalau wabunge wasiopungua thuluthi mbili; ama

(d) iwapo anayeshikilia afisi hiyo atajiuzulu kutoka kwa afisi hiyo kwa kuandika barua kwa Bunge husika.

**Kuongoza vikao Bungeni**

**107.** (1) Katika kikao chochote cha Bunge-

(a) Spika ndiye kiongozi;

(b) Ikiwa Spika hayupo, Naibu wa Spika ataongoza; na

(c) Spika na Naibu wake wasipokuwepo, mbunge mwingine yeyote atakayechaguliwa na Bunge ataongoza;

(2) Katika kikao cha pamoja kati ya Mabunge, Spika wa Baraza la Kitaifa litaongoza likisaidiwa na Spika wa Seneti.

**Viongozi wa vyama**

**108.** (1) Kutakuwa na Kiongozi wa chama kilicho na idadi kubwa ya wabunge na kiongozi wa chama cha walio wachache Bungeni.

(2) Kiongozi wa chama kilicho na wabunge wengi ndiye atakayekuwa kiongozi katika Baraza la Kitaifa la chama kilicho na idadi kubwa ya wabunge au muungano wa vyama;

(3) Kiongozi wa chama cha walio wachache ni kiongozi katika Baraza la Kitaifa la chama kilicho cha pili kwa idadi ya wabunge au muungano wa vyama;

(4) Mpangilio ufuatao wa kupewa umuhimu wa kwanza utafuatwa katika Baraza la Kitaifa –

(a) Spika wa Baraza la Kitaifa;

Draft for approval

(b) Kiogozi wa chama cha wabunge walio wengi;

(c) Kiongozi wa chama cha wabunge walio wachache.

**Sehemu ya 4 – Taratibu za Kutunga sheria Bungeni**

**Matumizi ya Mamlaka ya kutunga sheria**

**109.** (1) Bunge litatumia mamlaka yake ya kutunga sheria kupitia kwa Miswada itakayopitishwa Bungeni na kutiwa saini na Rais.

(2) Mswada wowote unaweza kutoka kwa Baraza la Kitaifa;

(3) Mswada usiohusu serikali za kaunti utashughulikiwa tu katika Baraza la Kitaifa, na kupitishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 122 na kanuni za Kuendesha Bunge.

(4) Mswada unaohusu serikali za kaunti unaweza kutoka kwa Baraza la Kitaifa au Seneti, na kupitishwa kwa mujibu wa Vifungu vya 109 hadi 113, Vifungu vya 122 hadi 123 na Kanuni za Kuendesha Bunge.

(5) Mswada unaweza kuwasilishwa na mwanachama wowote wa kamati ya Bunge husika, lakini Mswada wa Fedha unaweza kuwasilishwa tu kwa Baraza la Kitaifa kwa mujibu wa Kifungu cha 114.

**Miswada kuhusu Serikali za Kaunti**

**110.** (1) Katika Katiba hii, 'Mswada unaohusu serikali ya kaunti unamaanisha'-

(a) mswada ulio na masharti yanayoathiri majukumu na mamlaka ya serikali za kaunti zilizotajwa katika Mpangilio wa Nne; na

(b) Mswada unaohusiana na uchaguzi wa mwanachama wa bunge la kaunti au serikali za kaunti.

(c ) mswada uliotajwa katika Sura ya Kumi na mbili unaoathiri fedha za serikali za kaunti.

(2) Mswada unaohusu serikali za kaunti ni-

(a) mswada maalumu ambao utashughulikiwa chini ya Kifungu cha 111, iwapo-

(i) unahusiana na uchaguzi wa wabunge wa bunge la kaunti au serikali ya kaunti; au

(ii) ni Mswada wa Mgao wa Mapato ya Kaunti wa kila mwaka uliotajwa katika Kifungu cha 218; au

(iii) mswada wa kawaida ambao utashughulikiwa chini ya Kifungu cha 112 katika hali yoyote.

Draft for approval

(3) Kabla ya mojawapo ya vitengo vya Bunge kutathmini mswada, Maspika wa Baraza la Kitaifa na Seneti kwa pamoja wataamua suala lolote kuhusu kama Mswada huo unahusu kaunti na iwapo ni hivyo, kama ni mswada maalumu au wa kawaida.

(4) Wakati Mswada unahusu serikali za kaunti umepitishwa na Bunge moja, Spika wa Bunge hilo ataupeleka kwa Spika wa Bunge hilo jingine.

(5) Iwapo Mabunge yote mawili yatapitisha Mswada katika mfumo uleule, Spika wa Bunge ulikotoka mswada huo, ataupeleka kwa Rais katika muda wa siku saba ili uidhinishwe.

**Miswada maalumu inayohusu serikali za kaunti**

**111.** (1) Mswada maalumu unaohusu serikali za kaunti utashughulikiwa kwa namna moja kama mswada wa kawaida unaohusu serikali za kaunti kuambatana na ibara ya ya (2) na (3).

(2) Baraza la Kitaifa linaweza kurekebisha au kupiga marufuku mswada maalum uliopitishwa na Seneti kwa uamuzi tu ulioungwa mkono na angalau thuluthi mbili ya wabunge.

(3) Iwapo uamuzi katika Baraza la Kitaifa wa kurekebisha au kupiga marufuku mswada maalum utaangushwa, Spika wa Bunge ataupeleka mswada kwa hali iliyokubaliwa na Seneti kwa Rais katika muda wa siku saba ili kuidhinishwa.

**Miswada ya kawaida inayohusu serikali za kaunti**

**112.** (1) Iwapo Bunge moja linapitisha mswada wa kawaida kuhusu kaunti, na Bunge la pili-

(a) likaukataa Mswada huo, basi utapelekwa kwa kamati ya upatanisho chini ya Kifungu cha 113; au

(b) linapitisha Mswada uliorekebishwa, utarejeshwa kwa lile Bunge ulikotoka mwanzoni, ili kutathminiwa tena.

(2) Ikiwa, baada ya Bunge asili lililoleta Mswada limeushughulikia upya Mswada uliorejeshwa kwake chini ya ibara ya (1) (b), basi Bunge hilo-

(a) litaupitisha Mswada kama ulivyorekebishwa, Spika wa Bunge hilo ataupeleka kwa Rais katika muda wa siku saba ili kuidhinishwa.

(b) linaukataa Mswada kama ulivyorekebishwa, Mswada huo unapelekwa kwa kamati ya upatanishi chini ya Kifungu cha 113.

**Kamati za Upatanishi**

**113.** (1) Iwapo Mswada utapelekwa kwa kamati ya upatanishi chini ya Kifungu cha 112, Maspika wa Mabunge yote mawili watateua kamati ya upatanishi itakayohusisha

Draft for approval

idadi sawa ya wanachama wa Mabunge yote mawili ili kujaribu kutengeneza toleo jingine la Mswada litakalokubalika na Mabunge yote mawili.

(2) Iwapo kamati ya upatanishi itakubaliana na toleo hilo la Mswada, basi kila Bunge litapiga kura ili kupitisha au kukataa toleo hilo la Mswada.

(3) Iwapo Mabunge yote mawili yanakubali ttole hilo la Mswada kama ilivyopendekezwa na kamati ya upatanishi, Spika wa Baraza la Kitaifa atamkabidhi Rais ili kuidhinishwa.

(4) Iwapo kamati ya upatanishi itakosa kuafikiana kuhusu toleo hilo la Mswada kwa kipindi cha muda wa siku thelathini, au iwapo toleo hilo lililopendekezwa na kamati litakataliwa na na mojawapo ya Mabunge, basi Mswada huo utakuwa umeshindwa.

Draft for approval

**Miswada ya Fedha**

**114.** (1) Mswada wa fedha hauwezi kushughulikia suala jingine lolote isipokuwa tu lile ambalo limeorodheshwa katika fasiri ya 'Mswada wa fedha' kwenye ibara ya (3).

(2) iwapo, kwa maoni ya Spika wa Baraza la Kitaifa, mjadala unatoa vifungu kwa suala lililotajwa katika fasiri ya Mswada wa fedha, Bunge linaweza kuendelea tu kwa mujibu wa mapendekezo ya kamati husika ya Bunge baada ya kutilia maanani maoni ya Waziri anayehusika na fedha.

(3) Katika Katiba hii, 'Mswada wa fedha' unamaanisha, Mswada, tofauti na Mswada uliotajwa katika Kifungu cha 218 kilicho na masharti yanayoshughulikia-

(a) ushuru;

(b) kutoza malipo kwa hazina ya umma au kubadili au kuondolewa kwa mojawapo wa malipo hayo;

(c) kugawa, kupokea, kutunza, kuwekeza au kutoa pesa za umma;

(d) kudhamini mkopo wowote au ulipwaji wake; ama

(e) masuala mengineyo yanayotokana na masuala hayo.

(4) Katika ibara ya (3), "ushuru", "fedha za umma", na "mkopo", hazijumuishi ushuru wowote, fedha za umma au mkopo uliopatwa na kaunti.

**Idhini ya Rais na urejeshaji**

**115.** (1) Katika kipindi cha muda wa siku kumi na nne baada ya kupokea Mswada, Rais-

(a) ataweka saini; au

(b) ataurejesha Mswada Bungeni ili kuchunguzwa upya na Bunge huku likitilia maanani sababu alizo nazo Rais za kutouidhinisha mswada huo.

(2) Iwapo Rais ataurejesha Mswada bungeni kuchunguzwa upya, Bunge kwa kuzingatia taratibu zinazofaa kama zilivyotajwa katika sehemu hii, linaweza-

(a) kuurekebisha Mswada huo kwa kuangazia sababu muhimu alizotoa Rais; au

(b) kuupitisha Mswada huo kwa mara ya pili bila kufanya marekebisho.

(3) Iwapo Bunge limerekebisha Mswada huo huku likitilia maanani kikamilifu hoja za Rais, Spika anayehusika atampelekea Rais tena ili aweke sahihi.

(4) Bunge, baada ya kutilia maanani sababu za Rais,linaweza kuupitisha Mswada huo kwa mara ya pili bila marekebisho au ukiwa na marekebisho ambayo hayakuyapa nafasi kwa kikamilifu hoja za Rais kwa kura ambayo itaungwa mkono na-

(a) Thuluthi mbili ya wabunge wa Baraza la Kitaifa; na

(b) Thuluthi mbili ya uwakilishi katika Seneti, iwapo ni Mswada unaohitaji idhini ya Seneti.

(5) Iwapo Bunge litapitisha Mswada chini ya ibara ya (4)-

(a) Spika wa Bunge husika atahitajika baada ya siku saba auwakilishe tena mswada huo kwa Rais; na

(b) Rais atauwekea sahihi Mswada huo katika muda wa siku saba.

(6) Iwapo Rais hatauwekea sahihi Mswada huo au kuurejesha kwa wakati unaopendekezwa katika Ibara ya (1), au au aweke sahihi chini ya ibara ya (5) (b), mswada huo utachukuliwa kama ulioidhinishwa kufikia kumalizika kwa kipindi hicho.

Draft for approval

**Kutekelezeka kwa sheria**

**116.** (1) Mswada unaopitishwa na Bunge na kuidhinishwa na Rais, utachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kama Sheria ya Bunge katika muda wa siku saba baada ya kuidhinishwa; na

(2) Kwa kuzingatia ibara ya (3), Sheria ya Bunge inaanza kutekelezwa baada ya siku ya kumi na nne za kuchapishwa kwake katika Gazeti Rasmi la Serikali isipokuwa pale ambapo Sheria yenyewe inapendekeza tarehe au wakati wa kuanza kutekelezwa kwake.

(3) Sheria ya Bunge ambayo moja kwa moja inatunukia maslahi ya kifedha kwa wabunge, haitaidhinishwa hadi baada ya uchaguzi mkuu wa wabunge unaofuatia.

(4) ibara ya (3) haitatumika kwa maslahi walionayo wabunge wakiwa kama wananchi.

**Sehemu ya 5 – Taratibu za jumla na sheria za Bunge**

**Mamlaka, haki na kinga za Bunge**

**117.** (1) Kutakuwa na uhuru wa kujieleza na kujadili Bungeni**.**

(2) Bunge linaweza, kwa lengo la kupangilia vyema shughuli za bunge, kutoa mamlaka, marupurupu na kinga ya Bunge, kamati zake, kiongozi wa chama cha kisiasa cha wabunge walio wengi, kiongozi wa chama cha kisiasa cha wabunge walio wachache,vinara na wanachama wa kamati.

**Kufikiwa na kushiriki wa umma**

**118.** (1) Bunge-

(a) litafanya shughuli zake kwa njia ya uwazi, na kufanya vikao vyake na vile vya kamati zake mbele ya umma; na

(b) litarahisisha kushiriki na kuhusishwa kwa umma katika shughuli za kutunga sheria na shughuli nyingine za Bunge na kamati zake.

(2) Bunge halitazuia umma au chombo chochote cha habari dhidi ya kuhudhuria vikao isipokuwa katika hali mahususi ambazo Spika husika ataamua kwamba kuna sababu za kuridhisha kufanya hivyo.

**Haki ya kulalamikia Bunge**

**119.** (1) Kila mtu ana haki ya kulalamikia Bunge ili lishughulikie suala lolote lililo katika mamlaka yake ikiwa ni pamoja na, kurekebisha au kutoa sheria yoyote.

(2) Bunge litaweka Vifungu vya muhimu kuhusu utaratibu wa kutekeleza haki hii.

**Lugha rasmi za Bunge**

**120.** (1) Lugha rasmi za Bunge zitakuwa Kiswahili, Kiingereza na lugha ya ishara na shughuli za Bunge zinaweza kuendelezwa kwa Kiingereza, Kiswahili na lugha ya ishara ya Kenya.

(2) iwapo patatokea mgogoro kati ya tafsiri za matoleo tofauti ya lugha za Sheria ya Bunge, toleo la tafsiri iliyotiwa saini na Rais ndiyo itakayotumika.

**Idadi ya wabunge katika vikao**

**121.** Idadi katika Bunge itakuwa-

(a) wabunge hamsini katika Baraza la Kitaifa;

Draft for approval

(b) wabunge kumi na tano katika Seneti.

**Kupiga kura Bungeni**

**122.** (1) Ila tu, kulingana na maagizo katika Katiba hii, Suala lolote litakalopendekezwa kuamuliwa katika mojawapo wa Bunge, litaamuliwa kwa kupigiwa kura na wingi wa wabunge waliopo.

(2) Katika swali linalopendekezwa kuamuliwa katika mojawapo wa Bunge-

(a) Spika hatapiga kura; na

(b) Iwapo kura zitakuwa sawa pande zote, swali hilo litakuwa limeshindwa.

(3) Mbunge hatapigia kura suala ambalo yeye mwenyewe ana maslahi ya kifedha.

(4) Katika kujumlisha idadi ya wabunge kwenye Bunge kwa kusudi lolote la kupiga kura katika Bunge hilo, Spika wa bunge hilo hatahesabiwa.

**Maamuzi ya Seneti**

**123.** (1) Kwa uchaguzi, wanachama wote wa Seneti ambao walikuwa wameandikishwa kama wapigakura katika kaunti fulani, kwa pamoja wataunda ujumbe mmoja kwa lengo la Ibara ya (4) na mwanachama aliyechaguliwa chini ya Kifungu cha (98) (1) (a) atakuwa ndiye kiongozi wa ujumbe huo.

(2) Wakati Seneti itakapopigia kura kuhusiana na suala lolote isipokowa Mswada, Spika ataamua iwapo suala hilo linaathiri au kutoathiri kaunti.

(3) Seneti inapopiga kura kuhusu suala ambalo haliathiri kaunti, kila Seneta atakuwa na kura moja.

(4) Isipokuwa iwe vinginevyo, kama inavyoagizwa na Katiba hii, kwa suala lolote katika Seneti linaloathiri kaunti-

(a) kila ujumbe wa kaunti utakuwa na kura moja itakayopigwa na kiongozi wa ujumbe wa kaunti kwa niaba ya kaunti au, endapo hakuna kiongozi wa ujumbe huo, basi ipigwe na mwanachama mmoja wa ujumbe huo aliyeteuliwa na kiongozi wa ujumbe huo.

(b) mtu ambaye anapiga kura kwa niaba ya ujumbe ataamua iwapo apige kura kwa kuunga mkono au kinyume cha suala hilo, baada ya kushauriana na wajumbe; au

(c) suala hilo litaendelezwa iwapo litaungwa mkono na wajumbe walio wengi.

Draft for approval

**Kamati na Kanuni za Kuendesha Bunge**

**124.** (1) Kila Bunge linaweza kubuni kamati, na kuweka kanuni za kuendesha Bunge ili kusimamia shughuli zake ikiwa ni pamoja na shughuli za kamati zake.

(2) Bunge linaweza kubuni kamati za pamoja zinazojumuisha wabunge kutoka Mabunge yote mawili na kwa pamoja kudhibiti utaratibu wa kamati hizo.

(3) Shughuli za kila mojawapo ya Mabunge hayo hazitaharamishwa eti kwa sababu ya-

(a) nafasi katika uanachama wake; au

(b) kuwepo au kushiriki kwa mtu yeyote asiyepaswa kuwepo au kushiriki katika shughuli za bunge hilo.

(4) Wakati Bunge litakaposhughulikia kuhusu uteuzi wowote pale ambapo idhini inahitajika kama inavyotakikana na Katiba hii au Sheria ya Bunge-

(a) uteuzi huo utashughulikiwa na kamati husika ya Bunge;

(b) mapendekezo ya kamati yatawasilishwa Bungeni ili kuidhinishwa; na

(c) shughuli za kamati na za Bunge zitakuwa wazi kwa umma.

Draft for approval

**Uwezo wa kuitisha ushahidi**

**125.** (1) Bunge lolote na kamati yoyote yake, lina uwezo wa kumuita mtu yeyote kwa kusudi la kutoa ushahidi mbele yake;

(2) Kwa lengo la ibara ya (1), Bunge na kamati yake nyingineyo ina uwezo sawa na Mahakama Kuu-

(a) kuhakikisha kuhudhuria kwa mashahidi na kuwahoji chini ya kiapo, kuthibitisha au vinginevyo;

(b) kushurutisha utoaji wa nyaraka; na

(c) kutoa agizo au ombi la kuwahoji mashahidi walio katika mataifa ya nje.

**Sehemu ya 6 – Vipengee vya ziada**

**Eneo la Vikao vya Bunge**

**126.** (1) Vikao vya Bunge lolote vinaweza kufanyiwa sehemu yoyote nchini Kenya, na kuanza wakati wowote utakaoteuliwa na Bunge.

(2) Kila kutakapochaguliwa Bunge jipya, Rais, kwa kupitia notisi ya Gazeti Rasmi la Serikali, atateua mahali na tarehe ya kikao cha kwanza cha Bunge jipya, ambayo haitakuwa zaidi ya siku thelathini baada ya uchaguzi.

**Tume ya Huduma za Bunge**

**127.** (1) Kutabuniwa Tume ya Huduma ya Bunge.

(2) Tume hii itawahusisha-

(a) Spika wa Baraza la Kitaifa kama mwenyekiti;

(b) Naibu mwenyekiti aliyechaguliwa na Tume kutoka kwa wanachama walioteuliwa kwa mujibu wa aya (c);

(c) wanachama saba walioteuliwa na Bunge kutoka miongoni mwa wabunge ambao-

(i) wanne watateuliwa kwa usawa kutoka Mabunge yote mawili na chama au washirika katika muungano unaobuni Serikali ya kitaifa na ambao wawili kati yao watakuwa wanawake; na

(ii) watatu watakuwa wameteuliwa na vyama visivyo kwenye Serikali ya taifa, angalau mmoja wao atateuliwa kutoka kila Bunge, na angalau mmoja wao atakuwa mwanamke; na

(d) mwanamume na mwanamke walioteuliwa na Bunge kutoka miongoni mwa watu ambao si wabunge lakini wana uzoefu mkubwa katika masuala yanayohusu umma.

(3) Karani wa Seneti atakuwa katibu wa Tume hiyo.

(4) Mwanachama wa Tume atatoka afisini-

(a) iwapo mtu huyo ni Mbunge-

(i) baada ya kukamilika kwa kipindi cha Bunge ambacho mtu huyo alikuwa mbuge;

(ii) iwapo mtu huyo anakoma kuwa Mbunge; au

(b) iwapo mtu huyo ni mbunge mteule, baada ya kufutiliwa mbali kwa uteuzi wake na Bunge.

(5) licha yai Ibara ya (3), baada ya kumalizika kwa kipindi cha Bunge, mwanachama wa Tume aliyeteuliwa kwa mujibu wa ibara ya (2) (c) ataendelea kuwa afisini hadi mwanachama mwingine atakapoteuliwa na Bunge ili kuchukua nafasi yake.

(6) Tume ina jukumu la-

(a) kutoa huduma na kusaidia ili kufanikisha utendakazi bora wa Bunge;

(b) kubuni afisi katika huduma ya Bunge, na kuteua na kuwasimamia wanaoshikilia nyadhifa afisini humo;

(c) kutayarisha makadirio ya matumizi ya fedha za kila mwaka katika huduma za Baraza la Kitaifa na kudhibiti bajeti yake;

(d) kuanzisha ama kibinafsi au kwa pamoja na mashirika husika, mipango ya kukuza maadili ya demokrasia ya Bunge; na

Draft for approval

(e) kutekeleza majukumu mengine-

(i) muhimu kwa manufaa ya wabunge na wafanyakazi wa Bunge; au

(ii) yatakayopendekezwa na sheria ya kitaifa.

**Makarani na wafanyakazi wa Bunge**

**128.** (1) Kutakuwa na Karani wa kila bunge atakayeteuliwa na Tume ya Huduma za Bunge kwa idhini la Bunge husika.

(2) Afisi za makarani na afisi za wahudumu katika afisi hizo zitakuwa afisi katika huduma ya Bunge.

Draft for approval

## SURA YA TISA

## MAMLAKA KUU YA SERIKALI

### Sehemu ya 1- Kanuni na Muundo wa Mamlaka Kuu ya Kitaifa

**Kanuni za mamlaka kuu**

**129.** (1) Mamlaka kuu ya Serikali yanatokana na Wakenya na yatatekelezwa kwa mujibu wa Katiba hii.

(2) Mamlaka kuu ya serikali yanapaswa kutekelezwa kwa namna ambayo inachukuana na kanuni ya huduma kwa watu wa Kenya, na kwa ustawi na manufaa yao.

**Mamlaka Kuu ya Kitaifa**

**130.** (1) Mamlaka kuu ya kitaifa ya Jamhuri ya Kenya inamhusisha Rais, Naibu wa Rais na Baraza lote la Mawaziri.

(2) Muundo wa mamlaka kuu ya kitaifa utaakisi tofauti za kimaeneo na kikabila za watu wa Kenya

### Sehemu ya 2- Rais na Naibu wa Rais

**Mamlaka ya Rais**

**131.** (1) Rais -

(a) ndiye Kiongozi wa Taifa na Serikali;

(b) anatekeleza mamlaka makuu ya Jamhuri kwa usaidizi wa Naibu wa Rais na Mawaziri;

(c) ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya Kenya;

(d) ndiye mwenyekiti wa Baraza la Kitaifa la Usalama

(e) ni ishara ya umoja wa kitaifa.

(2) Rais -

(a) ataiheshimu, kuifuata na kuilinda Katiba;

(b) ataulinda uhuru wa Jamhuri ya Kenya.

(c) atakuza na kudumisha umoja wa taifa.

(d) atakuza heshima ya uanuwai wa watu wa Kenya; na

(e) kuhakikisha ulinzi wa uhuru na haki za kimsingi za raia na utawala wa sheria.

(3) Rais hatasimamia afisi nyingine yoyote ya Serikali au ya umma.

Draft for approval

**Majukumu ya Rais**

**132**. (1) Rais ata-

(a) toa hotuba katika ufunguzi wa kila Bunge jipya lililoteuliwa;

(b) toa hotuba katika kikao maalumu cha Bunge mara moja kwa mwaka na anaweza kuhutubia Bunge wakati mwingine wowote.

(c) Mara moja kila mwaka-

(i) atoe ripoti, kupitia kwa hotuba kwa taifa, kuhusu hatua ambazo zimechukuliwa na maendeleo ambayo yamepatikana ili kufikia uadilifu wa kitaifa uliotajwa katika Kifungu cha cha 10;

(ii) kuchapisha katika Gazeti Rasmi la Serikali, yaliyomo katika hatua na maendeleo yaliyoelezewa katika sehemu ya aya (i); na

(iii) kuwasilisha ripoti kwa Baraza la Kitaifa ili kujadiliwa kuhusu mafanikio ambayo yamepatika katika utimizaji wa majukumu ya kimataifa ya Jamhuri.

(2) Rais atapendekeza na kwa idhini ya Baraza la Kitaifa, ateue na anaweza kuwaachisha kazi-

(a) Mawaziri kwa mujibu wa Kifungu cha 152;

(b) Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa Kifungu cha 156;

(c) Katibu wa Baraza la Mawaziri kwa mujibu wa Kifungu cha 154;

(d) Makatibu wakuu kwa mujibu wa Kifungu cha 155;

(e) Mabalozi, wanadiplomasia, maafisa wa balozi na wawakilishi wengine wa nchi; na

(f) Kwa mujibu wa Katiba hii, afisa yeyote mwingine wa taifa au wa umma ambaye Katiba hii inamtaka au kumpa Rais uwezo wa kumteua au kumwachisha kazi.

(3) Rais-

(a) ataongoza mikutano ya Baraza la Mawaziri;

(b) ataelekeza na kuratibu majukumu ya wizara na idara za serikali; na

(c) kwa uamuzi uliochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, atagawa majukumu kwa Mawaziri ili kutekeleza na kutawala Sheria yoyote ya Bunge na si kwa kiasi ambacho hakiambatani na Sheria yoyote ya Bunge.

(4) Rais anaweza-

(a) kutekeleza jukumu lololote la kiserikali lililoelekezwa katika Katiba hii au katika sheria ya kitaifa na, isipokuwa vinginevyo, kama ilivyoelekezwa katika, Katiba hii kubuni afisi katika huduma ya umma kwa mapendekezo ya Tume ya Huduma ya Umma;

Draft for approval

(b) kupokea mabalozi na wawakilishi wa balozi za nchi za nje;

(c) kutunukia heshima kwa jina la watu na Jamhuri;

(d) kulingana na Kifungu cha 58, kutangaza hali ya hatari; na

(e) kwa idhini ya Bunge, anaweza kurangaza vita.

(5) Rais atahakikisha kwamba majukumu ya kimataifa kwa Jamhuri yanatimizwa kupitia kwa utendaji wa Mawaziri husika.

**Mamlaka ya Huruma ya Rais**

**133.** (1) Kwa ombi la mtu yeyote, Rais anaweza kutekeleza mamlaka yake ya msamaha kwa mujibu wa ushauri kutoka kwa Kamati ya Ushauri iliyoundwa katika Kifungu cha (2) , kwa-

(a) Kumsamehe kabisa au kwa masharti mtu ambaye amepatikana na hatia;

(b) kuahirisha utekelezaji wa adhabu kwa muda uliowekwa au kwa muda usiojulikana;

(c) Kubadili adhabu isiwe kali; au

(d) Kusamehe sehemu ya adhabu au adhabu yote.

(2) Kutakuwepo na Kamati ya Ushauri kuhusu Mamlaka ya Msamaha wa Rais, itakayowahusisha-

(a) Mwanasheria Mkuu;

(b) Waziri anayehusika na Huduma za Urekebishaji; na

(c) Angalau watu wengine watano,na wasiwe watu walio kwenye huduma ya umma au afisi za Serikali kama inavyoidhinishwa na Sheria ya Bunge.

(3) Bunge litatunga Sheria ili kubainisha-

(a) hatamu ya wanachama wa Kamati ya Ushauri;

(b) Taratibu za Kamati ya Ushauri; na

(c) Kigezo ambacho kitatumiwa na Kamati ya Ushauri katika kuunda ushauri wake.

(4) Kamati ya Ushauri inaweza kutilia maanani maoni ya waathiriwa wa hatia kuhusu yale inayompendekezea Rais.

**Matumizi ya mamlaka ya Urais kwa Rais wa muda**

**134.** (1) Yeyote anayeshikilia afisi ya Rais au yule ambaye anayeidhinishwa kwa mujibu wa Katiba hii kutumia mamlaka ya Rais-

Draft for approval

(a) Katika kipindi kinachoanzia mnamo tarehe ya kwanza kwenye uchaguzi wa Rais, na kukamilika wakati Rais mpya anapochukua hatamu za afisi; au

(b) wakati Rais hayupo au, hawezi kutekeleza mamlaka yake au wakati mwingine kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 147 (3), hawezi kutekeleza mamlaka ya Rais yaliyotajwa katika ibara ya  ya (2).

(2) Mamlaka hayo yaliyotajwa katika ibara ya (1) ni-

(a) kuteua na kuwaandika kazi majaji wa mahakama yenye mamlaka makuu;

(b) kuteua na kuandika kazi afisa yeyote wa umma ambaye Katiba au sheria hii inamhitaji  Rais kumteua;

(c) kuwaandika kazi au kuwateua au kuwaachiza kazi mawaziri na maafisa wengine wa umma au wa Serikali;

(d) Kuandika kazi au kuteu  au kuwaachisha kazi mabalozi au wawakilishi wa mabalozi, wanadiplomasia na wawakilishi wengine;

(e) Mamlaka ya msamaha wa Rais;

(f) Mamlaka ya kutuza heshima kwa jina la wananchi na Jamhuri.

Draft for approval

**Maamuzi ya Rais**

**135.** Uamuzi wa Rais katika utekelezaji wa jukumu lolote la Rais chini ya Katiba hii utakuwa kwa maandishi  na itahitajika kuwa na muhuri na saini ya Rais.

**Uchaguzi wa Rais**

**136**. (1) Rais atachaguliwa na wapigakura waliosajiliwa katika uchaguzi wa kitaifa utakaoendeshwa kwa mujibu wa Katiba hii na Sheria nyingine yoyote ya Bunge inayothibiti uchaguzi wa Rais.

(2) Uchaguzi wa Rais utafanyika-

(a) siku moja na ile ya uchaguzi mkuu wa Wabunge, ikiwa ni siku ya Jumanne ya pili ya mwezi Agosti ya kila mwaka wa tano; au

(b) katika hali ambazo zinatajwa  kwenye ibara ya 146.

**Sifa za kimsingi za kuchaguliwa na kutochaguliwa kwa  Rais**

**137.** (1) mtu anastahili kupendekezwa kuwa mgombeaji wa urais iwapo-

(a) ni raia kwa kuzaliwa;

(b) amehitimu kugombea uchaguzi kama mbunge;

(c) ameteuliwa na chama cha kisiasa au ni mgombeaji wa kujitegemea; na

(d) ameteuliwa na wapigakura wasiopungua elfu mbili kutoka kwa kila kaunti zilizo nyingi.

(2) mtu hastahili kuteuliwa kuwa mgombea urais iwapo-

(a) anawajibikia taifa la kigeni;

(b) ni afisa wa umma, anayeshikilia afisi yoyote ya Serikali au nyingine ya umma; au

(3) ibara ya (2) (b) haitatumika kwa-

(a) Rais;

(b) Naibu wa Rais; au

(c) mbunge

Draft for approval

**Tararatibu katika uchaguzi wa Rais**

**138.** (1) iwapo ni mgombea urais mmoja tu atateuliwa, mgombeaji huyo atatangazwa kuwa ameteuliwa.

(2) iwapo wagombeaji wa urais wawili au zaidi watateuliwa, uchaguzi wa urais utafanyika katika kila eneobunge.

(3) Katika uchaguzi wa urais-

(a) wapigakura wote waliosajiliwa kama wapigakura kwa kusudi la uchaguzi wa wabunge wana haki ya kupiga kura.

(b) uchaguzi utakuwa kwa njia ya siri katika siku ambayo imeelezewa kwenye ibara ya 101(1) na kwa wakati, mahali na kwa njia ambayo imeamriwa chini ya Sheria ya Bunge; na

(c) baada ya kuhesabiwa kwa kura katika vituo vya kupigia kura, Tume Huru ya Uchaguzi na mipaka itahesabu na kuhakikisha hesabu ya kura na kutangaza matokeo.

(4) Mgombea urais atatangazwa kuwa Rais iwapo atapokea-

(a) zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa katika uchaguzi; na

(b) angalau asilimia ishirini na tano ya kura zilizopigwa katika kila kaunti na kaunti ziwe zaidi ya nusu ya kaunti zote kwa jumla.

(5) Iwapo hakuna mgombeaji amechaguliwa, uchaguzi mwingine utafanyika upya katika kipindi cha siku thelathini baada ya uchaguzi uliopita, na katika uchaguzi huo mpya, wagombeji watakuwa-

(a) mgombeaji au wagombeaji ambao walipata kura nyingi zaidi; na

(b) mgombeaji au wagombeaji ambao walipata idadi ya pili ya wingi wa kura.

(6) pale ambapo wagombeaji zaidi ya mmoja wamepata idadi kubwa zaidi ya kura, ibara ya (5) (b) haitatumika na wagombeaji pekee katika uchaguzi mpya watakuwa wale ambao wameelezewa katika Ibara ya (5) (a).

(7) mgombeaji ambaye atapata idadi kubwa zaidi ya kura kwenye uchaguzi mpya, atatangazwa kuwa Rais.

(8) uchaguzi wa urais utafutiliwa mbali na uchaguzi mwingine mpya kufanyika iwapo-

(a) hakuna mtu ambaye ameteuliwa kama mgombea uchaguzi kabla ya kumalizika kwa kipindi kilichowekwa cha kuwasilisha watakaoteuliwa;

(b) mgombea uchaguzi wa urais au naibu wa Rais ataaga dunia mnamo au kabla ya tarehe iliyopangiwa kufanyika uchaguzi; au

(c) mgombea uchaguzi ambaye alistahili kutangazwa kuwa Rais, kuaga dunia kabla ya kutangazwa kama Rais.

(9) uchaguzi mpya wa urais chini ya ibara ya (8) utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya tarehe iliyokuwa imewekwa ya uchaguzi uliotangulia.

(10) Katika muda wa siku saba baada uchaguzi wa urais, mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka-

(a) atangaza matokeo ya uchaguzi; na

(b) atawasilisha ripoti iliyoandikwa ya matokeo ya uchaguzi kwa Jaji Mkuu na Rais aliye mamlakani.

Draft for approval

**Kifo kabla ya kuchukua mamlaka**

**139.** (1) Iwapo aliyetangazwa kuwa Rais-mteule atafariki kabla ya kuchukua hatamu za uongozi-

(a) Naibu wa rais-mteule ataapishwa kama kaimu Rais siku ileile tu ambayo Rais mteule angeapishwa; na

(b) uchaguzi mpya wa Rais utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya kifo cha Rais -Mteule.

(2) Iwapo Naibu wa rais-mteule atafariki kabla ya kuchukua hatamu za uongozi, afisi ya Naibu wa rais itatangazwa kuwa wazi baada ya Rais-mteule kuchukua mamlaka.

(3) Iwapo Rais mteule pamoja na Naibu wa rais watafariki kabla ya kuchukua mamlaka-

(a) Spika wa Baraza la Kitaifa atakuwa kaimu Rais kuanzia siku ambayo Rais mteule angeapishwa;na

(b) uchaguzi mpya utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya kifo cha pili.

**Maswali kuhusu uhalali wa uchaguzi wa urais**

**140.** (1) Mtu anaweza kuwasilisha malalamiko katika Mahakama ya Juu kupinga uchaguzi wa Rais mteule katika muda wa siku saba baada ya tarehe ya kutangaza matokeo ya uchaguzi wa urais.

(2) katika muda wa siku kumi na nne baada ya kuwasilishwa kwa malalamiko, Mahakaya ya Juu itasikiza na kuamua kesi hiyo na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(3) Iwapo Mahakama ya Juu itaamua kuwa uchaguzi wa Rais Mteule si halali, uchaguzi mpya utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya uamuzi huo.

**Kuchukua hatamu za Urais**

**141.** (1) kuapishwa kwa Rais Mteule kutafanyika wazi na mbele ya Jaji Mkuu na ikiwa Jaji Mkuu hayupo, basi mbele ya Naibu jaji mkuu.

(2) Rais Mteule ataapishwa Jumanne ya kwanza itakayofuata-

(a) siku kumi na nne baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Urais isipokuwa matangazo hayo yawe yamepingwa kulingana na Kifungu cha 140; ama

(b) siku ya saba kufuatia tarehe ambayo mahakama inatoa uamuzi na kutangaza kuwa uchaguzi ulikuwa halali, ikiwa malalamiko yoyote yalikuwa yamewasilishwa chini ya Kifungu cha 140.

(3) Rais Mteule anachukua hatamu za Urais kwa kuchukua na kutia sahihi kiapo cha uaminifu; na kiapo cha kutekeleza majukumu ya Urais kama ilivyoamriwa katika Ratiba ya Tatu.

(4) Bunge kupitia kwa sheria itatoa taratibu za sherehe za kuapishwa kwa Rais-mteule.

**Muhula wa Afisi ya Rais**

**142.** (1) Rais atachukua mamlaka ya afisi yake kuanzia tarehe aliyoapishwa, na kukamika wakati ambapo Rais mpya mteule atakapoapishwa kwa mujibu wa Kifungu cha (136) (2) (a).

(2) Hakuna Rais atakayeongoza kwa muhula wa zaidi ya vipindi viwili.

**Kulindwa dhidi ya kufunguliwa mashtaka**.

**143**. (1) mashtaka yoyote ya jinai hayatafunguliwa au kuendeshwa katika mahakama yoyote dhidi ya Rais au yeyote ambaye anashikilia afisi ya Rais wakati wa hatamu ya uongozi wake.

Draft for approval

(2) Mashtaka ya kesi za madai hayatawasilishwa katika mahakama yoyote dhidi ya Rais au yeyote anayetekeleza majukumu ya afisi hiyo wakati wa hatamu yake kutokana na chochote anachokifanya au kutofanya katika kutekeleza mamlaka yake yaliyo kwenye Katiba hii.

(3) Pale ambapo masharti katika sheria yanawekewa mipaka ya wakati ambao mashtaka haya yanaweza kuwasilishwa dhidi ya mtu huyu kwa mujibu wa Ibara ya (1) au (2), wakati ambapo mtu huyu anashikilia au kutekeleza majukumu ya afisi ya Rais hakitazingatiwa katika kuhesabu wakati ambao unaelezewa na sheria hii.

(4) Kinga dhidi ya kushtakiwa kwa Rais iliyo katika Kifungu cha hiki, haitatumika kwa hatia ambazo Rais anaweza kushtakiwa chini ya mkataba wowote ambao Kenya ni mshiriki na ambao unapinga kinga kama hii.

**Kuondolewa kwa Rais kwa misingi ya kukosa uwezo.**

**144.** (1) mwanachama wa Baraza la Kitaifa akiungwa mkono na robo ya idadi ya Wabunge wote anaweza kuwasilisha hoja Bungeni ya kuchunguzwa kwa uwezo wa afya ya kiakili au kimwili ya Rais katika kutekeleza majukumu ya afisi yake.

(2) Iwapo hoja iliyo kwenye ibara ya (1) itaungwa mkono na Wabunge walio wengi wa Bunge la Kitaifa-

(a) Spika wa Bunge atamjulisha Jaji Mkuu kuhusu uamuzi huu katika kipindi cha siku mbili; na

(b) Rais ataendelea kutekeleza majukumu ya afisi ikisubiriwa matokeo ya mashauri yanayohitajika katika Kifungu cha hiki.

(3) Jaji Mkuu katika kipindi cha siku saba, baada ya kupokea notisi ya uamuzi huu kutoka kwa Spika,atateua tume itakayokuwa na -

(a) watu watatu ambao ni wataalamu katika kuendesha masuala ya matibabu chini ya sheria za Kenya, walioteuliwa na taasisi ambayo kwa kisheria inawajibika kuthibiti matendo ya taaluma ya tiba;

(b) wakili mmoja wa Mahakama Kuu aliyeteuliwa na taasisi ambayo kisheria inawajibika kuthibiti matendo ya taaluma ya uwakili; na

(c) mtu mmoja atakayeteuliwa na Rais.

(4) Iwapo Jaji Mkuu atashindwa kuteua tume chini ya ibara ya (3), Naibu Jaji Mkuu atateua tume kama hii.

(5) Iwapo Rais atashindwa kumteua mtu wa tano, mtu huyu atateuliwa na-

(i) mmoja wa familia ya Rais; au

(ii) pale ambapo hakuna yeyote wa familia anataka au kuweza kufanya uteuzi huo, ufanywe na mmoja aliye na uhusiano wa karibu na wa kidugu na Rais.

(6) Tume itachunguza suala hili na kuripoti kwa Jaji Mkuu na Spika wa Baraza la

Draft for approval

Kitaifa katika muda wa siku kumi na nne baada ya uteuzi.

(7) Spika wa Bunge atawasilisha ripoti hiyo ya tume kwa Baraza la Kitaifa katika kipindi cha muda wa siku saba baada ya kuipokea.

(8) Ripoti hiyo ya tume itakuwa ya mwisho na hakutakuwa na rufaa na ikiwa tume itaripoti kwamba Rais anaweza kutekeleza majukumu yake ya afisi, Spika wa Baraza la Kitaifa atatangaza katika Baraza la Kitaifa.

(9) Iwapo tume itatangaza kuwa Rais hawezi kutekeleleza majukumu ya afisi, Baraza la Kitaifa litapiga kura kuidhinisha ripoti hiyo.

(10) Iwapo wabunge walio wengi kati ya wabunge wote wa Baraza la Kitaifa watapiga kura kuunga mkono kuidhinisha ripoti hii, basi Rais wa ataondolewa mamlakani.

**Kuondolewa kwa Rais kupitia kwa kura ya kutokuwa na imani**

**145.** (1) Mwanachama wa Baraza la Kitaifa, iwapo ataungwa mkono na thuluthi moja ya Wabunge wote, anaweza kuwasilisha hoja ya kutokuwa na imani na Rais-

(a) kwa misingi ya ukiukaji mkubwa wa Vifungu vya vya Katiba hii na na sheria nyingine yoyote.

(b) ikiwa pana sababu kubwa za kuamini kwamba Rais amehusika katika uhalifu kulingana na sheria za kitaifa au kimataifa;au

(c) utovu mkubwa wa nidhamu.

(2) Iwapo thuluthi mbili ya Wabunge wote wataunga mkono hoja chini ya ibara ya (1),

(a) Spika atamuarifu Spika wa Seneti kuhusu uamuzi huo katika muda wa siku mbili; na

(b) Rais ataendelea kutekeleza majukumu ya afisi ikisubiriwa matokeo ya mashauri yanayohitajika katika Kifungu cha hiki.

(3) kwa kipindi cha siku saba baada ya kupokea maamuzi kutoka kwa Spika wa Baraza la Kitaifa-

(a) Spika wa Seneti ataandaa mkutano wa Seneti ili kusikia mashtaka dhidi ya Rais;

(b) Baraza la Seneti, kwa uamuzi wake, linaweza kuteua kamati maalum itakayohusisha watu kumi na moja kati yao ili kuchunguza suala hili.

(4) Tume hii maalum iliyochaguliwa chini ya ibara ya (3) (b) –

(a) itachunguza suala hilo; na

(b) kisha kwa muda wa siku kumi kuripoti kwa Seneti ikiwa imepata tuhuma dhidi ya Rais ambazo zinaweza kuthibitishwa.

(5) Rais wa ana haki ya kwenda au kuwakilishwa mbele ya tume hii maalum wakati wa

Draft for approval

uchunguzi .

(6) Iwapo kamati maalum itaripoti kuwa yale yaliyomo katika tuhuma dhidi ya Rais -

(a) hayajathibitishwa, hakuna mashtaka zaidi yatayowasilishwa chini ya Kifungu cha hiki yanayohusiana na tuhuma hizi.

(b) yamethibitishwa, basi baraza la Seneti, baada ya kumpa Rais nafasi ya kusikilizwa, litapigia kura mashtaka ya kutokuwa na imani.

(7) na iwapo theluthi mbili ya wanachama wa Seneti watapiga kura kushikilia mashtaka ya kutokuwa na imani na Rais, basi atakoma kushikilia mamlaka ya afisi yake kama Rais wa nchi.

Draft for approval

**Nafasi ya kazi katika afisi ya Rais**

**146.** (1) Afisi ya Rais itakuwa wazi iwapo mwenye afisi hiyo-

(a) Amefariki;

(b) amejiuzulu kwa kumwandikia barua Spika wa Baraza la Kitaifa; au

(c) ama anawacha kuwa mamlakani kwa mujibu wa Kifungu cha 144 au 145, au masharti mengineyo ya Katiba hii.

(2) Pale ambapo nafasi ya kazi katika afisi ya Rais itakapotokea-

(a) Naibu wa rais atachukua mamlaka kama Rais kwa muda uliosalia wa kipindi cha Rais; au

(b) iwapo afisi ya Naibu wa rais ni wazi au Naibu wa rais hawezi kuchukua mamlaka ya Rais, Spika wa Baraza la Kitaifa atakuwa kaimu wa Rais na uchaguzi utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya nafasi hiyo kutokea katika afisi ya Rais.

(3) Mtu anayechukua hatamu za uongozi kama Rais chini ya ibara ya (2) (a) au kufuatia uchaguzi unaoidhinishwa na ibara ya (2) (b), isipokuwa aondolewe mamlakani kwa mujibu wa Katiba hii, ataendelea na wadhifa huo mpaka uchaguzi mpya ufanyike na Rais aliyechaguliwa upya kuapishwa kufuatia uchaguzi unaofuatia kwa wakati uliowekwa wa kawaida ulio chini ya Kifungu cha 136 (1).

(4) Iwapo Naibu wa rais atachukua mamlaka kama Rais chini ya ibara ya (2) (a) au mtu anachaguliwa kwa afisi ya Rais chini ya Ibara ya (2) (b), Naibu wa rais au mtu yule aliyechaguliwa watachukuliwa kufuatia kifungu cha 142 (2) kuwa-

(a) wamehudumu kipindi kizima kama Rais, iwapo kufikia tarehe ya kuchukua mamlaka ya afisi, kumesalia muda wa zaidi ya miaka miwili unusu kabla ya tarehe ya uchaguzi utakaofuata ambao umeratibiwa chini ya Kifungu cha 136 (2) (a); au

(b) hawajahudumu kipindi kizima kama Rais kwa hali nyingine yoyote.

**Majukumu ya Naibu wa rais**

**147.** (1) Naibu wa rais atakuwa msaidizi mkuu wa Rais na atakuwa kaimu Rais katika utekelezaji wa majukumu ya Rais.

(2) Naibu wa rais atatekeleza majukumu yaliyotunukiwa kwake na Katiba hii na majukumu mengine yoyote ya Rais anayoweza kupewa na Rais mwenyewe.

(3) kwa kutegemea Kifungu cha 134, wakati Rais hayupo au hawezi kutekeleza majukumu yake kwa muda mfupi na katika kipindi kingine chochote ambacho Rais anaweza kuamua, Naibu wa rais atakuwa kaimu wa Rais.

(4) Naibu hatashikilia mamlaka ya afisi nyingine ya Serikali au umma.

**Kuchaguliwa na kuapishwa kwa Naibu wa rais**

**148**. (1) Kila mgombea uchaguzi wa Urais atateua mtu ambaye amehitimu kuchaguliwa kama Rais, kama mgombeaji wa Naibu wa Rais.

(2) Kwa sababu ya ibara ya (1), hakutakuwa na utaratibu tofauti wa uteuzi wa Naibu wa Rais na kifungu cha 137 (1) (d) hakitatumika kwa mgombeaji kiti cha Naibu wa Rais.

(3) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itatangaza yule ambaye ameteuliwa na Rais mteule kuwa ndiye Naibu wa Rais.

(4) Kuapishwa kwa Naibu wa Rais mteule kutafanyika mbele ya Jaji Mkuu au iwapo Jaji Mkuu hayupo, mbele ya Naibu wa Jaji Mkuu na wananchi.

(5) Naibu wa rais mteule atachukua hatamu za afisi kwa-

(a) Kula kiapo cha uaminifu; na

(b) Kiapo cha kutekeleza majukumu ya afisi kama ilivyoidhinishwa katika Ratiba ya Tatu.

Kipindi cha afisi ya Naibu wa rais kitaanza kutumika kutoka siku ya kuapishwa kwa Naibu wa rais na kukoma-

Wakati mtu atakayechaguliwa kama Rais anayefuata katika uchaguzi chini ya Kifungu cha (136) (2) (a) ataapishwa;

Wakati Naibu wa rais atachukua mamlaka ya Rais; au

Katika kijiuzulu , kifo au kuachishwa kazi kwa Naibu wa rais.

Naibu wa rais anaweza, kwa wakati wowote, kujiuzulu kwa kumwandikiia barua Rais na kujiuzulu huku kutaanza kutekelezwa saa na tarehe iliyobainishwa katika barua hiyo au iwapo tarehe haijabainishwa, adhuhuri ya siku ya kupokelewa kwa barua hiyo.

Hakuna mtu yoyote atakayehudumu kwa zaidi ya vipindi viwili kama Naibu wa rais.

Draft for approval

**Nafasi ya kazi katika afisi ya Naibu wa rais**

**149.** (1) katika muda wa siku kumi na nne baada ya kutokea nafasi ya kazi katika afisi ya Naibu wa rais, Rais atamteua mtu mwingine kujaza nafasi hiyo, nalo Baraza la Kitaifa litapiga kura ya uamuzi wa uteuzi huo katika muda wa siku sitini baada ya kuupokea.

(2) Iwapo mtu atachukua mamlaka ya Naibu wa rais chini ya ibara ya (1), basi kwa kusudi la Kifungu cha 148 (8), mtu huyo atachukuliwa-

(a) kama aliyehudumu kipindi chote cha Naibu wa rais, iwapo mnamo tarehe ya kuchukua mamlaka, zaidi ya miaka miwili na nusu inasalia kabla ya uchaguzi unaofuatia ulioratibiwa chini ya Kifungu 136 (2); au

(b) hajahudumu katika kipindi cha afisi ya Naibu wa rais katika hali yoyote nyingine.

**Kuondolewa kwa Naibu wa rais**

**150**. (1) Naibu wa rais anaweza kuondolewa mamlakani-

(a) kwa misingi ya kutokuwa na uwezo wa kiakili na kimwili wa kutekeleza majukumu ya kiafisi;

(b) kwa kura ya kutokuwa na imani-

(i) kwa misingi ya kukosa uwezo wa kimwili na kiakili wa kutekeleza majukumu ya afisi;

(ii) kwa sababu ya kuwa kuna sababu kubwa sana za kuamini kuwa Naibu Rais amefanya uhalifu wa jinai chini ya sheria za kitaifa ama kimataifa

(iii) utovu mkubwa wa nidhamu.

(2) Sheria katika Vifungu vya 144 na 145 vinavyohusiana na kuondolewa mamlakani kwa Rais, kukiwa na mabadiliko yanayostahili, itatumika katika kumuondoa Naibu wa rais.

**Malipo na marupurupu ya Rais na Naibu wa Rais**

**151.** (1) Mshahara na marupurupu yatakayolipwa Rais na Naibu wa rais yatatoka kwa Mfuko wa Jumla wa fedha.

(2) Malipo na marupurupu ya Rais na Naibu wa rais hayatabadilishwa kwa lengo la kutowanufaisha wakiwa afisini.

(3) Malipo ya uzeeni yanayopaswa kulipwa Rais mstaafu na Naibu wa rais mstaafu pamoja na marupurupu mengine wanayostahili hayatabadilishwa ili kutowanufaisha katika maisha yao yote.

Draft for approval

**Sehemu ya 3- Baraza la Mawaziri**

**Baraza la Mawaziri**

**152**. (1) Baraza la Mawaziri litakuwa na-

(a) Rais;

(b) Naibu wa rais;

(c) Mwanasheria Mkuu;

(d) Mawaziri wasiopungua kumi na wanne au kuzidi ishirini na wawili;

(2) Rais atawapendekeza na kwa idhini ya Baraza la Kitaifa kuwateua Mawaziri.

(3) Waziri hatakuwa Mbunge.

(4) Kila mtu atakayeteuliwa kama waziri- atachukua mamlaka kwa kuapa au kukiri kwa watu na Jamhuri ya Kenya na kutii Katiba, mbele ya Rais na kwa mujibu wa Ratiba ya Nne; na anaweza kujiuzulu kwa kuwasilisha kwa Rais taarifa iliyoandikwa ya kujiuzulu kwake.

(5) Rais –

(a) anaweza kubadilisha kazi ya Waziri;

(b) anaweza kumwachiza kazicWaziri; na

(c) atamwachisha kazi waziri iwapo itahitajika kufanya hivyo, kwa uamuzi unaochukuliwa chini ya ibara ya (6) hadi (10).

(6) Mwanachama wa Baraza la Kitaifa anayeungwa mkono na angalau robo moja ya wabunge wote, anaweza kupendekeza mjadala wa kumtaka Rais amwachishe kazi waziri-

(a) kwa misingi ya kukiuka kwa hali ya juu Vifungu vya Katiba hii au sheria nyingine yoyote;

(b) kwa kuwa kuna sababu kali za kuamini kwamba Waziri amefanya kosa la jinai chini ya sheria za kitaifa na kimataifa; au

(c) kwa kuwa na utovu wa nidhamu wa hali ya juu;

(7) Iwapo mjadala chini ya ibara ya (5) utaungwa mkono na angalau thuluthi moja ya wabunge wote wa Baraza la Kitaifa-

(a) Bunge litateua kamati maalumu itakayokuwa na wanachama kumi na mmoja kuchunguza suala hili; na

(b) katika muda wa siku kumi, kamati hii maalumu itaripoti kwa Baraza la kitaifa ikiwa limepata iwapo madai dhidi ya Waziri ni ya kuthibitika.

(8) Waziri ana haki ya kwenda au kuwakilishwa mbele ya kamati maalumu wakati wa uchunguzi wake.

Draft for approval

(9) Iwapo kamati maalumu itaripoti kwamba imepata madai-

(a) hayathibitiki, hakuna taratibu nyingine zitakazochukuliwa; ama

(b) yamethibitika, Baraza la Kitaifa-

(i) litampa Waziri nafasi ya kusikizwa; na

(ii) litapiga kura kama litaidhinisha uamuzi unaomtaka Waziri kuachishwa kazi.

Iwapo uamuzi ulio chini ya ibara ya (8) unaomtaka Rais kumwachiza kazi Waziri, utaungwa mkono na wingi wa wabunge wa Baraza la Kitaifa-

(a) Spika kwa haraka atawasilisha uamuzi huu kwa Rais; na

(b) Rais atamwachisha kazi waziri.

**Maamuzi, majukumu na kuwajibika kwa Baraza la Mawaziri**

**153**. (1) Uamuzi wa Baraza la Mawaziri utakuwa kwa maandishi.

(2) Mawaziri wanawajibika kwa pamoja na kibinafsi kwa Rais katika kutekeleza mamlaka na utendaji wa majukumu yao.

(3) Waziri atahudhuria kikao cha kamati maalumu ya Baraza la Kitaifa anapohitajika na kamati ili kujibu swali lolote kuhusu suala linalomhusu.

(4) Mawaziri-

(a) wataendesha shughuli za kulingana na Katiba hii; na

(b) watawasilisha kwa Bunge ripoti kamili na za mara kwa mara kuhusu masuala yaliyo chini ya udhibiti wao.

**Katibu wa Baraza la Mawaziri**

**154.** (1) Kuna afisi teule ya Katibu katika Baraza la Mawaziri ambayo ni afisi katika huduma za umma.

(2) Katibu katika Baraza la Mawaziri-

(a) atapendekezwa na Rais na kwa idhini ya Baraza la Kitaifa kuteuliwa na Rais; na

(b) anaweza kuachishwa kazi na Rais.

(3) Katibu katika Baraza la Mawaziri-

(a) atakuwa na madaraka ya afisi ya Baraza la Mawaziri;

(b) atawajibika kulingana na maelekezo ya Baraza la Mawaziri, kwa kupanga shughuli na kuweka kumbukumbu za mikutano ya Baraza la Mawaziri;

Draft for approval

(c) atawasilisha uamuzi wa Baraza la Mawaziri kwa watu au mamlaka zinazofaa; na

(c) atakuwa na majukumu kama itakavyoagizwa na Baraza la Mawaziri.

(4) Katibu katika Baraza la Mawaziri anaweza kujiuzulu kwa kutoa notisi ya maandishi kwa Rais.

**Makatibu Wakuu**

**155.** (1) Kutabuniwa afisi ya Katibu Mkuu ambayo ni afisi katika huduma ya umma.

(2) Kila Wizara au idara ya Serikali itakuwa chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu.

(3) Rais -

(a) atapendekeza mtu ili kuteuliwa kama Katibu Mkuu kutoka miongoni mwa wale waliopendekezwa na Tume ya Huduma za Umma; na

(b) atamteua Katibu Mkuu kwa idhini ya Baraza la Kitaifa.

(4) Rais anaweza kubadilisha au kumhamisha kazi Katibu Mkuu.

(5) Katibu Mkuu anaweza kujiuzulu kwa kumuandikia Rais notisi.

**Sehemu ya 4- Afisi nyinginezo**

**Mwanasheria Mkuu**

**156.** (1) Kutabuniwa afisi ya Mwanasheria Mkuu

(2) Mwanasheria Mkuu atapendekezwa na Rais na kwa idhini ya Baraza la Kitaifa, kuteuliwa na Rais.

(3) Sifa za kuteuliwa kwa Mwanasheria Mkuu ni sawa na zile za uteuzi wa Jaji Mkuu.

(4) Mwanasheria Mkuu-

(a) ndiye mshauri mkuu kisheria kwa Serikali;

(b) atawakilisha Serikali ya taifa mahakamani au katika kesi nyingine za kisheria ambazo Serikali ya Kitaifa inahusika, isipokuwa kesi za jinai; na

(c) atatekeleza jukumu lingine lolote litakalotunukiwa afisi yake na kifungu cha Sheria ya Bunge au na Rais.

(5) Mwanasheria Mkuu atakuwa na mamlaka, kwa ruhusa ya mahakama, kuwa kama rafiki wa mahakama katika kesi za umma zile ambazo Serikali si mhusika.

(6) Mwanasheria Mkuu atakuza, kuhifadhi na kutetea utawala wa sheria na kulinda maslahi ya Jamhuri.

Draft for approval

(7) Mamlaka ya Mwanasheria Mkuu yanaweza kutekelezwa na yeye mwenyewe au na wasaidizi katika afisi yake wakitekeleza majukumu hayo kulingana na maagizo maalum au ya kijumla.

**Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma**

**157**. (1) Kutabuniwa afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atapendekezwa na Rais, na kwa idhini ya Baraza la Kitaifa, atateuliwa na Rais.

(3) Sifa za uteuzi wa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma zitakuwa sawa na zile za uteuzi wa Jaji wa Mahakama Kuu.

(4) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atakuwa na mamlaka ya kumwagiza Inspekta Mkuu wa Huduma ya Polisi ya Kenya kuchunguza habari yoyote au madai ya vitendo vya jinai, naye Inspekta Mkuu wa Huduma ya Polisi ya Kenya atatii maagizo hayo.

(5) Mkurugenzi wa mashtaka ya Umma atashikilia hatamu ya afisi yake kwa kipindi cha miaka nane na hatakuwa na nafasi ya kuteuliwa tena.

(6) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atatekeleza mamlaka ya Taifa ya kuongoza mashtaka na anaweza-

(a) Kuwasilisha na kuendeleza mashtaka ya kesi za uhalifu dhidi ya mtu yeyote katika mahakama yoyote (isipokuwa mahakama ya kijeshi) kutokana na kosa linalotuhumiwa kuwa limefanywa;

(b) Kuchukua na kuendeleza kesi zozote ya uhalifu zilizowasilishwa katika mahakama yoyote (isipokuwa katika mahakama ya kijeshi) zilizowasilishwa na kuendelezwa na mtu mwingine au mamlaka; na

(c) Kwa kutegemea ibara ya (7) na (8), kukomesha katika hatua yoyote, kabla ya hukumu kutolewa, kesi yoyote ya uhalifu iliyowasilishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ya Umma au kuchukuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ya umma kulingana na aya (b)

(7) Pale ambapo kukomeshwa kwa kesi kunakorejelewa katika ibara ya (6) (c) kunapotekelezwa baada ya mshitakiwa kukamilisha kujitetea, mshitakiwa ataachiliwa huru.

(8) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma hawezi kukomesha shitaka lolote bila ya idhini ya mahakama.

(9) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anaweza kuyaendesha yeye mwenyewe ama kumuagiza afisa wa afisi yake kulingana na masharti maalum au ya jumla.

(10) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma hatahitaji idhini ya mtu au mamlaka yoyote kuwasilisha kesi za kijinai, na katika kutekeleza mamlaka au majukumu yake hataelekezwa au kudhibitiwa na mtu au mamlaka yoyote.

Draft for approval

(11) Katika kutekeleza mamlaka yaliyotunukiwa na Kifungu hiki, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atazingatia maslahi ya taifa, maslahi ya utekelezaji wa haki na haja ya kuzuia na kuepuka matumizi mabaya ya utaratibu wa sheria.

(12) Bunge linaweza kutunga sheria ya kutunukia taasisi nyingine uwezo wa kuongoza mashtaka kuliko ile ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

**Kuondolewa na Kujiuzulu kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma**

**158.** (1) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anaweza kuachishwa kazi tu kwa misingi ya-

(a) kutoweza kutekeleza majukumu ya afisi kutokana na kukosa uwezo wa kiakili au wa kimwili;

(b) kutozingatia Sura ya Sita.

(c) kufilisika

(d) kutokuwa na umilisi.

(e) utovu wa nidhamu na tabia mbaya

(2) Mtu anayetaka kuondolewa mamlakani kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umm, anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Tume ya Huduma ya Umma ambayo, itakuwa kwa maandishi yakidhihirisha uhakika wa madai yanayounda msingi wa kuondolewa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

(3) Tume ya Huduma ya Umma itaangalia malalamiko haya na, ikiridhika kwamba yanafichua kwa msingi wa malalamiko chini ya Ibara ya (1), itapeleka malalamiko haya kwa Rais.

(4) Baada ya kuyapokea na kuyachunguza malalamiko haya, Rais, kwa muda wa siku kumi na nne, atamsimamisha kazi Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma ikisubiriwa uamuzi wa Rais kulingana na ibara ya (5) na atatekeleza haya kulingana na ushauri wa Tume ya Huduma ya Umma, atateua tume maalum itakayokuwa na-

(a) wanachama wanne kutoka miongoni mwa wale ambao wanashikilia au wameshawahi kushikilia afisi kama jaji wa mahakama yenye mamlaka makuu, au wale ambao wamehitimu kuweza kuteuliwa kwa afisi kama hii ;

(b) wakili mmoja ambaye amehudumu kwa angalau miaka kumi na mitano na atakayeteuliwa na taasisi ya kisheria inayowajibika kuthibiti taaluma ya uwakili; na

(c) watu wengine wawili walio na uzoefu wa masuala ya umma.

(5) Kamati itachunguza suala hilo kikamilifu na kuripoti kuhusu ukweli huo na kutoa mapendekezo kwa Rais ambaye atachukua hatua kulingana na mapendekezo hayo ya tume maalum.

(6) Mkurugezi wa Mashtaka ya Umma, ambaye amesimamishwa kazi kulingana na ibara ya (4) atapokea nusu ya mshahara hadi wakati wa kuachishwa kazi au kurudishwa kazini.

Draft for approval

(7) Tume Maalum iliyoteuliwa kulingana na ibara ya (4) itamchagua mwenyekiti miongoni mwao.

(8) Tume Maalum iliyochaguliwa kulingana na ibara ya (4) itawajibika kuthibiti taratibu zake.

(9) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anaweza kujiuzulu kwa kumuandikia barua Rais.

Draft for approval

## SURA YA KUMI

## MAHAKAMA

### Sehemu ya 1 – Mamlaka ya Mahakama na Mfumo wa Kisheria

### Mamlaka ya Mahakama

**159**. (1) Mamlaka ya Mahakama yanatokana na watu, yanajikita katika mahakama na mahakama maalum zinazobuniwa kulingana na Katiba hii.

(2) Katika kutekeleza majukumu ya kimahakama, mahakama na mahakama maalum zitaongozwa na kanuni zifuatazo-

(a) haki itatendwa kwa kila mtu bila kuzingatia hadhi ;

(b) Haki haitacheleweshwa;

(c) njia m'badala za kusuluhisha kesi zikiwemo msamaha, mashauriano, na maridhiano na njia za kitamaduni za kusuluhisha migogoro zitaimarishwa, kwa mujibu wa ibara ya (3);

(d) haki itatolewa kwa kuzingatia matatizo yaliyopo ya utaratibu wa kitaalamu; na

(e) lengo na kanuni za Katiba hii zitatunzwa na kuendelezwa.

(3) Mbinu za kitamaduni za utatuaji wa migogoro hazitatumiwa kwa njia ambayo-

(a) itakiuka Sheria za Haki;

(b) itagongana na haki na maadili au kusababisha matokeo yatakayogongana na haki na maadili;

(c) haiambatani na Katiba hii au sheria yoyote iliyoandikwa.

Draft for approval

### Uhuru wa Mahakama

**160**. (1) Katika utekelezaji wa mamlaka ya mahakama, Mahakama kama ilivyoundwa chini ya kifungu cha 161, itazingatia Katiba hii pamoja na sheria na haitadhibitiwa wala kuelekezwa na mtu yeyote mwingine au halmashauri.

(2) Afisi ya jaji wa mahakama ya Mamlaka Kuu haitafutiliwa mbali wakati ambapo kuna afisa anayeshikilia wadhifa huo.

(3) Mishahara na marupurupu yanayofaa kulipwa, au kuhusiana na, majaji yatatoka kwa Mfuko wa Jumla wa Serikali.

(4) Kulingana na Kifungu cha 168 (6), mishahara na marupurupu inayofaa kulipwa, au kuhusiana na majaji haitabadilishwa kwa njia itakayowaathiri, na marupurupu ya kustaafu ya jaji hayatabadilishwa ili kumuathiri jaji mstaafu katika maisha yake ya uhai.

(5) Mwanachama wa mahakama hatawajibika katika hatua au kesi kuhusiana na

chochote watakachofanya au watakachokosa kufanya kwa nia njema katika utendaji kazi wa kisheria kwa kutekeleza majukumu ya mahakama.

**Afisi na Maafisa wa Mahakama**

**161**. (1) Mahakama inahusisha majaji wa mahakama za mamlaka ya juu, mahakimu na maafisa wengine wa idara ya Mahakama.

(2) Kutabuniwa afisi ya-

(a) Jaji Mkuu, atakayekuwa Mkuu wa Mahakama;

(b) Naibu Jaji Mkuu, atakayekuwa Naibu Mkuu wa Mahakama;

(c) Msajili Mkuu wa Idara ya Mahakama ambaye ni msimamizi mkuu wa kiutawala na afisa wa uhasibu wa Idara ya Mahakama.

(3) Tume ya Huduma za Mahakama inaweza kuunda afisi nyingine za masjala ikiwa pana haja ya kufanya hivyo.

**Mfumo wa mahakama**

**162**. (1) Mahakama za mamlaka ya juu ni Mahakama ya Juu, Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu na mahakama nyingine zilizotajwa katika Kifungu cha (2).

(2) Bunge litabuni mahakama zenye hadhi ya Mahakama Kuu ili kusikiliza na kuamua mizozo inayohusu –

(a) kuandikwa kazi na masuala yanayohusiana na ajira; na

(b) Mazingira na utumiaji wa ardhi, na hatimiliki ya, umiliki wa ardhi.

(3) Bunge litaamua mipaka na majukumu ya mahakama yanayofafanuliwa katika ibara ya (2).

(4) Mahakama za chini ni mahakama zinazobuniwa chini ya Kifungu cha 169, au na Bunge kulingana na Kifungu hicho.

**Sehemu ya 2- Mahakama za Mamlaka Kuu**

**Mahakama ya Juu**

**163**. (1) Kutabuniwa Mahakama ya Juu itakayojumuisha –

(a) Jaji Mkuu, ambaye atakuwa rais wa mahakama hiyo;

(b) Naibu Jaji Mkuu, ambaye –

(i) atakuwa naibu wa Jaji Mkuu; na

Draft for approval

(ii) atakuwa Naibu wa rais wa mahakama hiyo; na

(c) majaji wengine watano.

(2) Mahakama ya Juu itakuwa imebuniwa kisawasawa kwa minajili ya kesi zake iwapo itakuwa na majaji watano.

(3) Mahakama ya Juu-

(a) itakuwa na mamlaka ya kipekee ya kusikiliza na kuamua kesi zinazohusu kura za afisi ya Rais zinazotokana na Kifungu cha 140; na

(b) kulingana na ibara ya (4) na (5), mamlaka ya rufaa ya kusikiza na kuamua rufani kutoka -

(i) Mahakama ya Rufaa; na

(ii) mahakama yoyote nyingine au mahakama maalum kama inavyoidhinishwa na sheria ya kitaifa.

(4) Rufaa zitakatwa kutoka kwa Mahakama ya Rufaa -

(a) Kwa misingi ya haki katika kesi yoyote inayohusisha ufasiri na utekelezaji wa Katiba hii; na

(b) katika kesi nyingine yoyote ambapo Mahakama ya Juu au Mahakama ya Rufaa inathibitisha kwamba suala muhimu kwa umma linahusika, kwa mujibu wa Ibara ya (5).

(5) Uamuzi wa Mahakama ya Rufaa chini ya ibara ya (4) (b) unaweza kuangaliwa upya na Mahakama ya Juu, kuukubali, kuurekebisha au kubadilishwa ama kubatilishwa.

(6) Mahakama ya Juu inaweza kutoa maoni ya ushauri kwa serikali ya taifa, taasisi yoyote ya serikali, au idara yeyote ya serikali ya kaunti iwapo itaombwa kufanya hivyo.

(7) Mahakama nyingine zote, isipokuwa Mahakama ya Juu, zitafuata maamuzi ya Mahakama ya Juu.

(8) Mahakama ya Juu itatunga sheria zitakazoongoza utekelezaji wa majukumu yake.

(9) Sheria ya Bunge inaweza kutoa masharti zaidi kuhusu majukumu ya Mahakama ya Juu.

**Mahakama ya Rufani**

**164**. (1) Kutabuniwa Mahakama ya Rufaa, ambayo –

(a) itakuwa na idadi ya majaji ambao hawatapungua kumi na wawili kulingana na sheria za bunge; na

(b) inaundwa na kusimamiwa kulingana na ufafanuzi wa Sheria ya Bunge.

Draft for approval

(2) Kutakuwa na Rais wa Mahakama ya Rufaa ambaye atachaguliwa na majaji wa mahakama ya Rufaa kutoka miongoni mwao.

(3) Mahakama ya Rufaa ina mamlaka ya kusikiza rufaa kutoka –

(a) Mahakama Kuu; na

(b) mahakama nyingine au mahakama maalum kulingana na Sheria ya Bunge.

**Mahakama Kuu**

**165**. (1) Kutabuniwa Mahakama Kuu ambayo -

(a) inajumuisha idadi ya majaji kama itakavyobainishwa na Sheria ya Bunge; na

(b) imeundwa na kusimamiwa kulingana na Sheria ya Bunge.

(2) Kutakuwa na Jaji Kinara wa Mahakama Kuu ambaye atachaguliwa na majaji wa mahakama ya Juu kutoka miongoni mwao.

(3) Kulingana na ibara ya (5), Mahakama Kuu ina –

(a) mamlaka asilia yasiyokuwa na mpaka katika masuala ya uhalifu na masuala ya kiraia;

(b) mamlaka ya kubaini iwapo haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria ya Haki imenyimwa, kukiukwa, kuingiliwa au kutishiwa; au

(c) mamlaka ya kusikiliza rufaa ya uamuzi wa mahakama maalum iliyoteuliwa chini ya Katiba hii kuchunguza kuondolewa kwa mtu kutoka afisini, tofauti na Tume iliyoteuliwa chini ya Kifungu cha 144;

(d) mamlaka ya kusikiliza swala lolote kuhusu kufasiriwa kwa Katiba hii pamoja na kutoa uamuzi wa-

(i) swali iwapo sheria yoyote inakiuka au kwenda kinyume na Katiba hii;

(ii) swali iwapo chochote kinachosemwa kutekelezwa chini ya mamlaka ya Katiba hii au sheria yoyote, kinakiuka au kutekelezwa kinyume na Katiba hii;

(iii) suala lolote linalohusu mamlaka ya kikatiba ya taasisi za serikali kwa mujibu wa serikali za kaunti na suala linalohusu uhusiano wa kikatiba kati ya viwango vya serikali; na

(iv) swali linalohusu mkinzano wa sheria chini ya Kifungu cha 191.

(4) suala lolote linalothibitishwa na mahakama kuwa linazua utata mkubwa kisheria chini ya ibara ya (3) (b) au (d) litatasikilizwa na idadi isiyo shufwa ya majaji, wasiopungua watatu , watakaoteuliwa na Jaji Mkuu.

(5) Mahakama Kuu haina mamlaka kuhusiana na masuala –

(a) yaliyotengewa mamlaka ya kipekee ya Mahakama ya Juu chini ya Katiba hii; au

Draft for approval

(b) yaliyo chini ya mamlaka ya mahakama yaliyotajwa katika Kifungu cha 162(2).

(6) Mahakama Kuu ina mamlaka ya kusimamia mahakama ndogo na mtu yeyote, asasi au halmashauri, inayotekeleza jukumu la kimahakama au jukumu la mahakama ya kubuni, lakini siyo mahakama ya juu.

(7) Kwa malengo ya ibara ya (6), Mahakama Kuu inaweza kuitisha rekodi za kesi yoyote iliyoko katika mahakama ndogo, au mtu, asasi au halmashauri kama ambavyo imetajwa katika ibara ya (6) na inaweza kutoa maagizo yoyote na kutoa maelekezo inayochukulia kuwa yanafaa ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

**Uteuzi wa Jaji Mkuu, Naibu wa Jaji Mkuu na Majaji wengine**

**166**. (1) Rais atateua-

(a) Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu kulingana na mapendekezo ya Tume ya Huduma ya Mahakama na kwa idhini ya Bunge; na

(b) majaji wengine wote, kwa mujibu wa mapendekezo ya Tume ya Huduma za Mahakama.

(2) Majaji wa mahakama za mamlaka ya juu watateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao –

(a) wana shahada katika taaluma ya sheria kutoka chuo kinachotambulika, au ni mawakili wa Mahakama Kuu, au wana hitimu sawa na hizo katika masuala ya kawaida ya kisheria;

(b) wana tajriba inayohitajika ambayo wameipata nchini Kenya na taasisi nyingine za mataifa yanayotumia mamlaka ya sheria ya Jumuia ya Madola kama zinazotajwa katika ibara ya (3) hadi (6); na

(c) wana mienendo na maadili mema na hawabagui.

(3) Jaji Mkuu na majaji wa Mahakama ya Juu watateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao wana –

(a) tajriba ya miaka kumi na mitano kama jaji katika mahakama ya mamlaka ya juu; au

(b) tajriba ya miaka isiyopungua kumi na mitano kama msomi anayeheshimika, afisa katika idara ya mahakama, uanasheria au tajriba kama hiyo katika maeneo mengine ya taaluma ya uanasheria; au

(c) amehitimu kwa viwango vilivyotajwa katika aya (a) na (b) kwa jumla ya miaka kumi na mitano;

(4) Kila jaji wa Mahakama ya Rufaa atateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao wana–

(a) tajriba ya miaka isiyopungua kumi kama jaji wa Mahakama ya kiwango cha juu; au

Draft for approval

(b) tajriba ya miaka isiyopungua kumi kama msomi anayeheshimika au mwanasheria au tajriba kama hiyo katika nyanja nyingine husika ya kisheria; au

(c) amehitimu kwa viwango vilivyotajwa katika aya (a) na (b) kwa muda wa jumla ya miaka kumi.

(5) Kila jaji wa Mahakama Kuu atateuliwa kutoka miongoni mwa watu walio na –

(a) tajriba isiyopungua miaka kumi kama jaji katika mahakama ya kiwango cha juu; au

(b) tajriba ya miaka isiyopungua kumi kama msomi anayeheshimika au mwanasheria au tajriba kama hiyo katika nyanja nyingine husika ya kisheria; au

(c) amehitimu kwa viwango vilivyotajwa katika aya (a) na (b) kwa jumla ya muda wa miaka kumi.

Draft for approval

**Kipindi cha kudumu afisini kwa Jaji Mkuu na majaji wengine**

**167**. (1) Jaji atastaafu kutoka afisini atakapofikisha umri wa miaka sabini, lakini anaweza kuamua kustaafu wakati wowote baada ya kufikisha miaka sitini na tano.

(2) Jaji Mkuu atahudumu afisini kwa jumla ya miaka kumi au hadi wakati wa kustaafu chini ya Ibara ya (1), kutegemea itakayofika mwanzo.

(3) Iwapo kipindi cha Jaji Mkuu kuhudumu kitakamilika kabla ya kufikisha umri wa kustaafu chini ya ibara ya (1), Jaji Mkuu anaweza kuendelea kuhudumu kama jaji wa Mahakama ya Juu.

(4) Iwapo, wakati wa kukamilika kwa kipindi cha kuhudumu cha Jaji Mkuu, Jaji huyu ataamua kuendelea kuhudumu mahakamani chini ya ibara ya (3), mtu atakayeteuliwa kama Jaji Mkuu atateuliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 166(1) ingawa uteuzi huo utasababisha kuwepo kwa idadi inayozidi idadi inayokubalika ya majaji wa Mahakama ya Juu.

(5) Jaji Mkuu na jaji mwingine yeyote anaweza kujiuzulu kutoka afisini kwa kuandika barua kwa Rais.

**Kuondolewa kutoka afisini**

**168**. (1) Jaji wa mahakama yenye mamlaka ya juu anaweza kuondolewa tu kutoka afisini kwa misingi ya –

(a) kushindwa kutekeleza majukumu ya afisi kwa sababu ya ukosefu wa uwezo wa kimwili au kiakili;

(b) kukiuka kanuni za utendakazi zilizowekewa majaji wa Mahakama Makuu kupitia Sheria ya Bunge.

(c) kufilisika;

(d) kutokuwa na umilisi; au

(e) utovu wa nidhamu, ama katika utekelezaji wa majukumu ya jaji au vinginevyo.

(2) Hatua ya kumuondoa jaji kwenye wadhifa wake inaweza kuanzishwa na Tume ya Huduma za Mahakama itakayochukua hatua hiyo kivyake au kwa sababu ya malalamiko yatakayowasilishwa na mtu yeyote kwa Tume hii.

(3) Malalamiko ya mtu kwa Tume ya Huduma za Mahakama chini ya Ibara ya (2) yatawasilishwa kwa maandishi, yakionyesha ushahidi wa misingi ya madai ya kumuondoa jaji.

(4) Tume ya Huduma za Mahakama itaangalia malalamiko hayo na iwapo itaridhika kwamba ushahidi unaobainika wazi chini ya Ibara ya (1), na itatuma malamamiko hayo kwa Rais.

(5) Katika muda wa siku kumi na nne baada ya kupokea malalamiko hayo, Rais wa Taifa atamsimamisha kazi jaji huyo, na kwa kuzingatia ushauri wa Tume ya Huduma za Mahakama –

(a) iwapo itakuwa ni Jaji Mkuu, itateua mahakama maalum itakayowahusisha -

(i) Spika wa Baraza la Kitaifa kama mwenyekiti;

(ii) majaji watatu wa Mahakama ya Juu kutoka kwa mahakama zenye kutumia sheria ya kawaida;

(iii) wakili mmoja mwenye tajriba ya kazi ya miaka kumi na mitano;

(iv) watu wengine wawili wenye tajriba kuhusu masuala ya umma; au

(b) iwapo ni jaji mwingine asiye Jaji Mkuu, atateua mahakama maalum itakayohusisha -

(i) mwenyekiti na wanachama wengine watatu ambao wanahudumu au wamewahi kuhudumu kama jaji wa mahakama za mamlaka ya juu, au ambao wamehitimu kuteuliwa kuhudumu kwenye wadhifa huo, lakini katika kila moja ya hali hizo hawajakuwa, katika miaka mitatu inayotangulia, wamekuwa wanachama wa Tume ya Huduma ya Mahakama;

(ii) wakili mmoja mwenye tajriba ya kazi ya miaka kumi na mitano;

(iii) watu wengine wawili wenye tajriba kuhusu masuala ya umma.

(6) Licha ya kifungu cha (160) (4), mshahara na marupurupu ya jaji ambaye anasimamishwa kazi chini ya Ibara ya (5) utapunguzwa kwa nusu hadi wakati ambapo jaji huyo ataondolewa au kurudishwa kazini.

(7) Mahakama maalum inayobuniwa chini ya Ibara ya (5)-

(a) itatoa kanuni za kuongoza vikao vyake kwa mujibu wa sheria inayorejelewa katika Ibara ya (10); na

(b) kuchunguza suala hilo kwa haraka, kutoa ripoti ya matokeo na kuwasilisha

Draft for approval

mapendekezo ya kutiliwa maanani kwa Rais.

(8) Jaji ambaye haridhiki na uamuzi wa mahakama maalum chini ya kifungu hiki, anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwa Mahakama ya Juu, rufaa hii itakatwa kati ya siku kumi baada mahakama maalum kutoa mapendekezo yake.

(9) Rais atatoa maamuzi kwa mujibu wa mapendekezo yaliyotolewa na mahakama maalum kufikia mwisho wa-

(a) kuisha kwa muda uliotolewa wa kukata rufaa chini ya Ibara ya (8), iwapo rufaa kama hiyo haikukatwa; au

(b) baada ya kukamilika kwa hatua zote za kesi ya rufaa chini ya Ibara ya (8), iwapo rufaa kama hiyo imekatwa na uamuzi wa mwisho unaafikiana na mapendekezo ya mahakama hiyo maalum.

(10) Bunge litatunga sheria ya kutoa kanuni za kufuatwa na mahakama maalum itakayoteuliwa chini ya kifungu cha hiki.

**Sehemu ya 3 -Mahakama Ndogo**

**169**. (1) Mahakama saidizi ni –

(a) Mahakama za Mahakimu;

(b) Mahakama za Kadhi;

(c) Mahakama ya Kijeshi; na

(d) Mahakama yoyote nyingine au mahakama maalum kama inavyoweza kubuniwa kwa Sheria ya Bunge, isipokuwa mahakama zilizobuniwa kwa mujibu wa kifungu cha 162 (2).

(2) Bunge, kwa njia ya sheria litatoa mipaka, mamlaka na majukumu kwa mahakama ambazo zilizobuniwa chini ya ibara ya (1).

**Mahakama za Kadhi**

**170**. (1) Kutakuwa na Kadhi Mkuu na idadi kama hiyo, isiwe chini ya watatu, ya kadhi wengine kulingana na itakavyopendekezwa chini ya Sheria ya Bunge.

(2) Mtu hatahitimu kuteuliwa kushikilia au kuhudumu katika wadhifa wa Kadhi isipokuwa mtu huyo -

(a) anakiri kwa dini ya Uislamu; na

(b) ana maarifa ya sheria ya Uislamu kama inavyokubalika na madhehebu ya Waislamu, ambayo kwa mujibu wa Tume ya Huduma za Mahakama, amehitimu kuongoza vikao vya mahakama ya Kadhi.

Draft for approval

(3) Bunge litabuni mahakama za kadhi, na kila mahakama ya Kadhi itakuwa na mamlaka kulingana na jinsi itakavyoidhinishwa na sheria, kwa mujibu wa Ibara ya (5).

(4) Kadhi Mkuu na Kadhi wengine, au Kadhi Mkuu na Makadhi wengine kama hao (wasiopungua watatu) kama ilivyoidhinishwa na Sheria ya Bunge, watapewa uwezo kila mmoja wa kuhudumu kwa mahakama ya Kadhi iliyo na mamlaka nchini Kenya.

(5) Mamlaka ya mahakama ya Kadhi yatahusisha kubainisha maswali ya sheria ya Uislamu kuhusiana na hadhi ya kibinafsi, ndoa, talaka au urithi katika kesi ambazo pande husika zinakiri dini ya Uislamu na kutii mamlaka ya mahakama za kadhi.

**Sehemu ya 4 – Tume ya Huduma za Mahakama**

**Kuundwa kwa Tume ya Huduma za Mahakama**

**171.** (1) Tume ya Huduma za Mahakama imeundwa.

(2) Tume hii inajumuisha-

(a) Jaji Mkuu, atakayekuwa mwenyekiti wa Tume;

(b) Jaji mmoja wa Mahakama ya Juu aliyeteuliwa na majaji wa Mahakama ya Juu;

(c) Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufaa aliyeteuliwa na majaji wa mahakama ya Rufaa;

(d) Jaji mmoja wa Mahakama Kuu na hakimu mmoja, mwanamke mmoja na mwanamme mmoja, walioteuliwa na wanachama wa muungano wa majaji na mahakimu;

(e) Mwanasheria Mkuu;

(f) Mawakili wawili, mwanamke mmoja na mwanamme mmoja, kila mmoja awe na tajriba isiyopungua miaka kumi na tano, walioteuliwa na chama kilichokubaliwa kisheria kusimamia taaluma ya uwakili;

(g) mtu mmoja aliyeteuliwa na Tume ya Huduma ya Umma; na

(h) mwanamke mmoja na mwanamme mmoja kuwakilisha umma,wasiokuwa wanasheria, watakaoteuliwa na Rais kwa idhini ya Baraza la Kitaifa.

(3) Mkuu wa Masjala ya Mahakama atakuwa Katibu wa Tume.

(4) Wanachama wa Tume, isipokuwa Jaji Mkuu na Mwanasheria Mkuu watahudumu kwenye afisi, mradi tu wawe wamehitimu, kwa kipindi cha miaka mitano na wataweza kuteuliwa kuhudumu zaidi kwa kipindi kingine cha miaka mitano na cha mwisho.

Draft for approval

**Majukumu ya Tume ya Huduma za Mahakama**

**172**. (1) Tume ya Huduma za Mahakama itahakikisha na kuimarisha uhuru na uwajibikaji wa idara ya Mahakama na kuimarisha uhuru na uwazi wa mahakama na usimamizi bora na wenye uwazi na haki pamoja na –

(a) kupendekeza kwa Rais wa Taifa watu wa kuteuliwa kuwa majaji;

(b) kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masharti ya utendajikazi wa-

(i) majaji na maafisa wengine wa mahakama kando na mishahara; na

(ii) wafanyikazi wa mahakama;

(c) kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu hali na mazingira ya utendajikazi wa wafanyakazi katika idara ya mahakama;

(d) kuteua, kupokea malalamiko ya kupinga, kuchunguza na kuwafuta au hatua nyinginezo za kuwaadhibu, kuwasajili,mahakimu na maafisa wengine wa mahakama na wafanyakazi wengine wa mahakamani, kwa njia ambayo imetolewa na Sheria ya Bunge.

(e) Kuandaa na kutekeleza mipango ya kuendelea kwa elimu na mafunzo ya majaji, mahakimu, maafisa wengine wa idara ya mahakama na wafanyakazi wengine katika kazi hiyo; na

(f) kuishauri Serikali ya Kitaifa kuboresha utendakazi na utekelezaji wa haki na pamoja na kutoa huduma za ushauri wa kisheria.

(2) Katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume itaongozwa na yafuatayo –

(a) ushindani na utaratibu wenye uwazi katika kuwaajiri maafisa wa idara ya mahakama na wafanyakazi wengine katika idara hiyo.

(b) kukuza usawa wa kijinsia.

**Hazina ya Mahakama**

**173**. (1) Kutabuniwa hazina itakayojulikana kama Hazina ya Mahakama ambayo itaongozwa na Msajili Mkuu.

(2) Hazina hiyo itatumika kugharamia usimamizi wa Mahakama na majukumu mengine kama itakavyokuwa muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama.

(3) Kila mwaka wa kifedha, Mkuu wa Masjala ataandaa makadirio ya matumizi ya mwaka utakaofuata, na kuyawasilisha kwa Baraza la Kitaifa ili kuidhinishwa.

(4) Yakiidhinishwa na Baraza la Kitaifa, matumizi haya yatagharamiwa na Mfuko wa Jumla na fedha hizo zitalipwa moja kwa moja kwa Hazina ya Mahakama.

(5) Sheria ya Bunge itabainisha sheria na njia ya kusimamia Hazina hiyo.

Draft for approval

## SURA YA KUMI NA MOJA

## SERIKALI YA UGATUZI

**Sehemu ya 1- Malengo na kanuni za Serikali ya ugatuzi**

**Malengo ya ugatuzi**

**174.** Malengo ya Serikali ya ugatuzi ni-

(a) kuhakikisha kuwa kuna mamlaka ya kidemokrasia na uwajibikiaji wa Serikali ;

(b) kuhimiza umoja wa kitaifa kwa kutambua uanuwai wa jamii mbalimbali;

(c) kuwapa watu katika kila ngazi mamlaka ya kujitawala na kushiriki katika matumizi ya mamlaka ya Serikali katika kufanya maamuzi ya mambo yanyowaathiri;

(d) kutambua haki za jamii zote katika kusimamia masuala ya jamii zao na kujiendeleza zaidi;

(e) kulinda na kuhamasisha maslahi na haki za jamii za watu walio wachache na zile za watu waliotengwa;

(f) kustawisha miradi ya kijamii na kiuchumi na utoaji wa huduma za karibu na zilizo rahisi ili kumfikia kila mtu nchini Kenya;

(g) kuhakikisha kuna ugavi sawa wa rasilmali zote za kijamii na za kitaifa kote nchini.

(h) kufanikisha ugatuzi wa mamlaka ya taasisi za Serikali, uendeshaji wake wa shughuli ama huduma kutoka mji mkuu wa Kenya; na

(i) kuhakikisha kuna kudhibiti na kugawana mamlaka kwa njia iliyo sawa.

Draft for approval

**Kanuni za Serikali ya ugatuzi**

**175.** Serikali za kaunti zilizobuniwa chini ya Katiba hii zitazingatia kanuni zifuatazo-

(a) Serikali za kaunti zitazingatia misingi ya kidemokrasia na utengano wa mamlaka.

(b) Serikali za kaunti sharti ziwe na njia za kuaminika za kuzalisha mapato ili kuziwezesha kuendesha shughuli zao na kutoa huduma kwa njia bora; na

(c) isiyo zaidi ya theluthi mbili ya wanachama wawakilishi wa taasisi za umma katika Serikali za kaunti watakuwa wa jinsia moja.

**Sehemu ya 2 – Serikali za Kaunti**

**Serikali za Kaunti**

**176**. (1) Kila kaunti itakuwa na Serikali yake itakayokuwa na bunge na Baraza la Kaunti.

(2) Kila Serikali ya kaunti itagatua shughuli zake na utoaji wa huduma ili kuhakikisha kwamba imepata ufanisi wa kutekeleza majukumu yake kadiri iwezekanavyo.

**Wanachama wa baraza la kaunti**

**177.** (1) Baraza la kaunti lina wanachama wafuatao-

(a) wanachama waliochaguliwa na wapiga kura waliosajiliwa katika wadi, kila wadi ikijumuisha eneo moja la uwakilishi siku ile ya kupiga kura ya uchaguzi mkuu wa kuwachagua wabunge, itakayokuwa Jumanne ya pili ya mwezi Agosti baada ya kila miaka mitano

(b) idadi ya wabunge maalum ili kuhakikisha kuwa hakuna zaidi ya wabunge thuluthi mbili wa jinsia moja katika bunge hilo.

(c) idadi ya wanachama kutoka katika makundi yaliyotengwa, wakiwemo watu walemavu, jamii za watu wachache na vijana, kama inavyopendekezwa katika Sheria ya Bunge; na

(d) spika, asiye mwanachama rasmi.

(2) Wanachama wanaotajwa katika ibara ya (1) (b) na (c) watatateuliwa na vyama vya kisiasa kwa mgao wa kutegemea idadi ya viti chama cha kisiasa kilivyopata katika uchaguzi huo, katika kaunti hiyo chini ya Ibara ya (a) kulingana na kifungu cha 90.

(3) Kujaza viti maalum kwa mujibu wa ibara ya (1) (b) kutaamuliwa baada ya kutangazwa kwa wanachama waliochaguliwa katika kila wadi.

(4) Baraza la kaunti huchaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano.

Draft for approval

**Spika wa baraza la kaunti**

**178.** (1) Kila baraza la kaunti litakuwa na spika aliyechaguliwa na baraza la kaunti kutoka kwa watu wasio wanachama wa baraza hilo.

(2) Kinara wa kikao cha baraza la kaunti atakuwa-

(a) spika wa baraza hilo; au

(b) wakati spika hayupo, mwanachama mmoja aliyeteuliwa na baraza hilo.

(3) Baraza litatunga sheria itakayoruhusu kuchaguliwa na kuondolewa afisini kwa maspika wa mabaraza ya kaunti.

**Kamati za mamlaka kuu za Kaunti**

**179.** (1) Mamlaka kuu ya kaunti yamepewa, na yatatekelezwa, na kamati za mamlaka kuu za

Kaunti.

(2) Kamati ya mamlaka kuu ya Kaunti inajumuisha-

(a) gavana wa kaunti na naibu wake; na

(b) wanachama walioteuliwa na gavana wa kaunti, kwa idhini ya baraza, kutoka kwa watu wasio wanachama wa baraza.

(3) Idadi ya wanachama walioteuliwa kwa mujibu wa ibara ya (2)(b) haitazidi:

(a) thuluthi moja ya wanachama wa bunge la kaunti kama bunge hilo halina zaidi ya wanachama zaidi ya thelathini; au

(b) kumi; kama baraza lina wanachama thelathini au zaidi.

(4) gavana wa kaunti na naibu wake, watakuwa afisa mkuu na naibu wa afisa mkuu wa kaunti, mtawalia.

(5) Gavana wa kaunti asipokuwepo, naibu wake ana mamlaka ya kutosha ya kuendesha shughuli zote na majukumu ya gavana wa kaunti.

(6) Wanachama wa kamati kuu ya kaunti wanawajibikia gavana wa kaunti katika utekelezaji wa majukumu na mamlaka yao.

(7) Iwapo afisi ya gavana itakuwa wazi, wanachama wa mamlaka kuu ya kaunti walioteuliwa chini ya ibara ya (2) (b) watakuwa hawana kazi.

**Uchaguzi wa gavana wa kaunti na naibu wa gavana wa kaunti**

**180**. (1) Gavana wa kaunti atachaguliwa moja kwa moja na wapiga kura waliosajiliwa katika kaunti hiyo, siku ile ya uchaguzi mkuu wa wabunge, itakayokuwa Jumanne ya pili ya mwezi Agosti, baada ya kila miaka mitano.

(2) Kuhitimu kuchaguliwa kuwa gavana wa kaunti, mtu lazima awe amehitimu kuchaguliwa kuwa mwanachama katika baraza la kaunti.

(3) Ikiwa mgombea kiti cha gavana mmoja tu atateuliwa, mtu huyu atatangazwa kuwa amechaguliwa.

(4) Ikiwa wagombea kiti cha gavana wawili au zaidi watateuliwa, kura zitapigwa katika kaunti hiyo na mgombeaji atakayepata kura nyingi zaidi atatangazwa kuwa mshindi.

(5) Kila mgombea kiti cha gavana wa kaunti atamteua mtu mmoja ambaye amehitimu kuchaguliwa kama gavana wa kaunti kuwa mgombea kiti cha naibu gavana.

(6) Mtu hatahudumu afisini-

(a) kama gavana wa kaunti kwa vipindi zaidi ya viwili; au

(b) kama naibu gavana kwa vipindi zaidi ya viwili.

(7) Kwa mujibu wa ibara ya (7), mtu ambaye hajaingia afisi ya gavana wa kaunti

Draft for approval

atachukuliwa kuwa amehudumu kwa kipindi kizima, kwa mujibu wa kifungu cha 182 (3) (b).

**Kuondolewa kwa gavana wa kaunti**

**181.** (1) Gavana wa kaunti anaweza kuondolewa kutoka afisini katika msingi wowote kati ya misingi ifuatayo-

(a) ukiukaji wa katiba hii au sheria yoyote uliokithiri ;

(b) ikiwa pana sababu ya kutosha kuamini kuwa gavana huyo wa kaunti amefanya uhalifu chini ya sheria ya taifa au kimataifa;

(c) kutumia mamlaka ya afisi vibaya au utovu wa nidhamu uliokithiri;

(d) kukosa uwezo wa kimwili au kiakili kutekeleza majukumu ya afisi ya gavana.

(2) Bunge litatunga sheria ya kutoa kanuni za kufuatwa kumuondoa gavana afisini kwa msingi wowote uliotajwa katika ibara ya (1).

**Nafasi katika afisi ya gavana wa kaunti**

**182.** (1) Afisi ya gavana wa kaunti itaachwa wazi iwapo anayeshikilia afisi hiyo-

atafariki;

atajiuzulu kwa kumwandikia spika wa baraza la kaunti;

hafai kwa mujibu wa kifungu cha 180 (2);

atapokea kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake ni kufungwa gerezani kwa miezi isiyopungua kumi na miwili;

ataondolewa afisini kwa mujibu wa katiba hii.,

(2) Iwapo afisi ya gavana wa kaunti itakuwa wazi, naibu gavana atatekeleza majukumu ya gavana kwa kipindi kilichosalia cha gavana kuhudumu.

(3) Iwapo mtu ataikalia afisi kwa mujibu wa ibara ya (2), kwa minajili ya kifungu cha 180(7), mtu huyo atachukuliwa kuwa-

(a) amehudumu kipindi kizima cha gavana wa kaunti iwapo, kufikia tarehe mtu huyo alipoingia afisi hiyo, zaidi ya miaka miwili na nusu imesalia kabla ya tarehe ya uchaguzi mwingine ilivyo kawaida chini ya kifungu cha 180 (1); au

(b) hajahudumu afisini kama gavana wa kaunti iwapo ni hali nyingine yoyote.

(4) Iwapo nafasi itatokea katika afisi ya gavana wa kaunti na ile ya naibu gavana wa kaunti au iwapo naibu gavana wa kaunti hawezi kuishikilia kwa muda, spika wa baraza la kaunti atashikilia afisi hiyo kwa muda.

Draft for approval

(5) Iwapo nafasi itatokea katika hali inayotjwa katika ibara ya (4), uchaguzi wa gavana wa kaunti utafanywa kati ya siku sitini baada ya tarehe ya spika kuanza kushikilia afisi hiyo.

(6) Mtu atakeyechukua nafasi ya kuhudumu katika afisi ya gavana wa kaunti chini ya kifungu hiki, ila tu aondolewe afisini kwa mujibu wa Katiba hii, ataendelea kuhudumu hadi gavana mwingine atakapochaguliwa wakati wa uchaguzi unaofuata kwa mujibu wa kifungu cha 180 (1).

**Majukumu ya mamlaka kuu za kaunti**

**183**. (1) Kamati kuu ya kaunti ina majukumu yafuatayo:

(a) utekelezaji wa sheria za bunge la kaunti;

(b) utekelezaji, katika kaunti , sheria za taifa inavyohitajika kisheria;

(c) kusimamia shughuli za utawala wa kaunti na idara zake; na

(d) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa Katiba hii na sheria ya nchi.

(2) kamati kuu ya kaunti inaweza kuandaa sheria iliyopendekezwa na kuziwasilisha kwa bunge la kaunti.

(3) kamati kuu ya kaunti itatoa ripoti kamili za mara kwa mara kwa baraza la kaunti kuhusu masuala yaliyo chini ya udhibiti wa kamati hiyo.

**Maeneo ya miji na majiji**

**184.** (1) Sheria ya Kitaifa itaidhinisha utawala na usimamizi wa maeneo ya mijini na majiji na hususan ita-

(a) buni vigezo vya kuainisha maeneo kama miji na majiji;

(b) buni kanuni za utawala na usimamizi wa maeneo ya mijini na majiji; na

(c) ruhusu ushiriki wa umma katika utawala wa maeneo ya mijini na majiji.

(2) Sheria ya kitaifa inyorejelewa katika Ibara ya (1) inaweza kujumuisha njia za kutambua kategoria mbalimbali za maeneo ya mijini na majiji, na utawala wao.

**Mamlaka ya kisheria ya mabaraza ya kaunti**

**185.** (1) Mamlaka ya kutunga sheria ya kaunti yamepatiwa na yatatekelezwa na baraza la kaunti.

Draft for approval

(2) Baraza la kaunti, linaweza kutunga sheria zozote muhimu, zinazoshughulikia masuala yanayohusiana na, ufanikishaji wa mamlaka na majukumu yake, na utekelezaji wa mamlaka ya serikali ya kaunti kwa mujibu wa Mpangilio wa nne.

(3) Baraza la kaunti, likizingatia kanuni ya kugawana mamlaka, lina uwezo wa kusimamia kamati ya mamlaka kuu ya kaunti na idara nyingine za mamlaka katika kaunti.

(4) Baraza la kaunti laweza kupokea na kuidhinisha mipango na sera kwa-

(a) usimamizi na utumiaji wa rasilmali za kaunti; na

(b) kustawisha na kusimamia miundomsingi na idara zao.

**Sehemu ya 3– Mamlaka na shughuli za Serikali za kaunti**

**Mamlaka na Majukumu mahususi ya serikali za kaunti na kitaifa**

**186.** (1 ) Isipokuwa kama ilivyotajwa katika Katiba hii, mamlaka na majukumu ya Serikali ya taifa na zile za kaunti, mtawalia,ni kama yalivyoelezwa katika Mpangilio wa Nne

(2) Jukumu linalopatikana katika zaidi ya ngazi moja ya Serikali ni jukumu lililo katika eneo zaidi ya moja la utawala la ngazi hizo za Serikali.

(3) Jukumu ambalo halijatolewa na Katiba hii au na sheria ya taifa kwa kaunti, ni jukumu ya Serikali ya taifa.

(4) Kuwa yakini zaidi, bunge litatunga sheria ya Jamhuri katika suala lolote.

**Kuhamisha mamlaka na majukumu kati ya viwango vya serikali**

**187**. (1) Mamlaka au majukumu ya Serikali katika kiwango kimoja yaweza kuhamishwa hadi kiwango kingine cha Serikali kwa makubaliano kati ya Serikali hizo mbili kama-

(a) mamlaka au jukumu hilo litapata uzito zaidi likitekelezwa na Serikali hiyo itakayolichukua; na

(b) kuhamishwa kwa mamlaka au majukumu kunaafikiana na sheria ambazo zinafungamana na utekelezaji wake.

(2) Pale ambapo mamlaka au shughuli imehamishwa kutoka kiwango kimoja cha Serikali hadi kwa Serikali ya kiwango kingine-

(a) mipango itafanywa ili kuhakikisha kwamba gharama za utekelezaji wa mamlaka au shughuli hiyo iliyohamishwa imefanikishwa; na

(b) uwajibikaji wa kikatiba kwa shughuli au mamlaka utahifadhiwa na serikali iliyopangiwa kulingana na Mpangilio wa Nne.

Draft for approval

**Sehemu ya 4 – Mipaka ya kaunti**

**Mipaka ya kaunti**

**188.** (1) Mipaka ya kaunti inaweza kubadilishwa kwa pendekezo tu-

(a) lililopendekezwa na Tume huru iliyobuniwa na bunge kwa lengo hilo; na

(b) iliyoidhinishwa na-

(i) Baraza la Kitaifa likiungwa mkono na wabunge wasiopungua thuluthi mbili wa bunge hilo; na

(b) seneti ikiungwa mkono na angalau wawakilishi wa kaunti wasiopungua thuluthi mbili ya ujumbe wa kaunti.

(2) Mipaka ya kaunti inaweza kubadilishwa kwa kuzingatia-

(a) wingi wa watu na uongezekaji wao;

(b) miundomsingi na uhalisia wao;

(c) mshikamano wa kihistoria na misingi ya kitamaduni;

(d) gharama za usimamizi;

(e) maoni ya jamii zilizoathirika;

(f) malengo ya ugatuzi wa Serikali; na

(g) sifa za kijiografia.

Draft for approval

**Sehemu ya 5 – Mahusiano katika Serikali**

**Ushirikiano wa Serikali ya kitaifa na za kaunti**

**189.** (1) Serikali katika viwango vyovyote-

(a) itaendesha na kutumia mamlaka yake ikiheshimu utekelezaji na heshima za taasisi nyinginezo za viwango vingine za Serikali na kuheshimu hadhi ya kikatiba na taasisi za serikali katika viwango vingine, na kwa serikali ya kaunti, katika kiwango cha kaunti;

(b) kusaidia, kushirikiana na kushauriana na Serikali katika viwango vyote vifaavyo, kutekeleza sheria katika viwango vyote vya Serikali; na

(c) kushauriana na Serikali katika ngazi tofauti tofauti kwa minajili ya kubadilishana mawazo, kusimamia sera na utawala, huku uwezo ukikuzwa.

(2) Serikali katika viwango tofauti na serikali tofauti za kaunti zitashirikiana katika kutekeleza majukumu na mamlaka yao, kwa lengo hilo, zitaunda muungano wa kamati na mamlaka.

(3) Katika kutofautiana kokote kule kwa Serikali, Serikali inayohusika itafanya kila jitihada kutatua mzozo huo ikizingatia taratibu za kisheria kama zilivyo katika sheria ya taifa.

(4) Sheria ya kitaifa itatoa mwongozo na taratibu za kutatua mizozo kati ya Serikali kwa mbinu m'badala za kutatua mizozo zikiwemo kushauriana, kupatanisha na kusuluhisha.

**Usaidizi kwa serikali za kaunti**

**190.** (1) Bunge litatunga sheria ili kuhakikisha kwamba serikali za kaunti zimepokea usaidizi wa kutosha kuziwezesha kutekeleza majukumu yao.

(2) Serikali za kaunti zitaendesha mifumo ya usimamizi wa fedha inayoafikana na matakwa ya sheria ya kitaifa.

(3) Bunge litatunga sheria itakayoruhusu serikali ya kitaifa kuingilia serikali ya kaunti iwapo-

(a) imeshindwa kutekeleza majukumu yake; au

(b) haiendeshi mfumo wa usimamizi wa fedha unaoambatana na matakwa ya sheria ya kitaifa.

(4) Sheria inayotawa katika Ibara ya (3) inaweza, hasa, kuipa mamlaka serikali ya kitaifa-

(a) kuchukua hatua mwafaka ili kuhakikisha kuwa majukumu ya serikali ya kaunti yanatekelezwa na mfumo wa usimamizi wa fedha unaendeshwa inavyostahili; na

(b) kama pana haja, ichukue jukumu la kutekeleza majukumu hayo.

(5) Sheria inayotajwa katika Ibara ya (3)-

(a) itahitaji notisi kutolewa kwa serikali ya kaunti kuhusu hatua zozote serikali ya kitaifa inadhamiria kuchukua;

(b) itaruhusu serikali ya kitaifa kuchukua hatua zilizo muhimu pekee;

(c) itahitaji serikali ya kitaifa, wakati inaingilia kati, ichukue hatua ambazo zitaisaidia serikali ya kaunti kurejelea kikamilifu utekelezaji wa majukumu yake; na

(d) kutoa utaratibu utakaowezesha seneti kuhusika vyema ili kumaliza au kutoa suluhu kwa matatizo hayo.

**Mkinzano wa sheria**

**191.** (1) Kifungu hiki kinahusu mikinzano ya sheria kati ya sheria za kitaifa na zile za kaunti, kwa mujibu wa masuala yanayopatikana katika viwango vyote viwili vya Serikali.

Draft for approval

(2) Sheria ya kitaifa itakuwa na mamlaka juu ya ile sheria ya kaunti iwapo-

(a) sheria za kitaifa zitatumika kwa usawa katika Kenya nzima na masharti mengine yaliyomo katika ibara ya (3) yametoshelezwa; au

(b) sheria za kitaifa zinalenga kudhibiti maamuzi yasiyo ya busara ya kaunti ambayo-

(i) yanaweza kuwa na athari mbaya kiuchumi, kiafya ama maslahi ya usalama wa Kenya au kaunti nyingine; au

(ii) zitazuia utekelezaji wa sera za uchumi wa kitaifa.

(3) Masharti yanayotajwa katika ibara ya (2) (a) ni yafuatayo -

(a) sheria za kitaifa hushughulikia suala ambalo haliwezi kutatuliwa na sheria zilizotungwa na kaunti peke yake.

(b) sheria za kitaifa hushughulikia suala ambalo ili lishughulikiwe kikamilifu, linataka sheria ambazo ni sawa katika taifa zima. Hufanya hivi kwa kuwa na-

(i) Kanuni na viwango vya ubora; au

(ii) sera za kitaifa; au

(c) Sheria za kitaifa ni muhimu kwa-

(i) uhifadhi wa usalama wa kitaifa;

(ii) uhifadhi wa umoja wa kiuchumi;

(iii) kulinda masoko ya pamoja kulingana na uhamishaji wa bidhaa, huduma na ufanyaji kazi, mtaji na ajira;

(iv) kuhimiza shughuli za kiuchumi miongoni mwa mipaka ya kaunti;

(v) kuhimiza nafasi sawa au usawa katika kufikia huduma za serikali; au

(vi) kulinda mazingira.

(4) Sheria za kaunti huwa na mamlaka juu ya sheria za taifa kama mahitaji yoyote yanayorejelewa katika ibara ya (2) hayahusiki.

(5) Katika kushughulikia mzozo unaohusu sheria za viwango tofauti za serikali, mahakama yatapendelea ufasiri wa sheria ambao utazuia mzozo kuliko ufasiri ambao utaleta mzozo.

(6) uamuzi wa mahakama kwamba sheria ya kiwango kimoja cha Serikali kinakubalika kuliko kifungu kingine cha sheria ya kiwango kingine cha Serikali hakubatilishi kifungu cha sheria cha kiwango kile kingine, ila tu sheria hiyo nyingine inakuwa haifanyi kazi kwa kiasi kile inachotofautiana na hiyo nyingine.

Draft for approval

**Sehemu ya 6 – Kusimamishwa kwa muda kwa Serikali za kaunti**

**Kusimamishwa kwa muda kwa serikali ya kaunti**

**192.** (1) Rais anaweza kusimamisha serikali ya kaunti kwa muda-

(a) wakati wa dharura inayotokana na mizozo ya ndani au vita; au

(b) wakati wa hali za kipekee zinazohitaji kuchukuliwa kwa hatua kama hiyo.

(2) Serikali ya kaunti haitasimamishwa kwa muda kulingana na ibara ya (1) (b) hadi tume huru ifanye uchunguzi wa mashtaka yaliyowasilishwa dhidi yake, Rais wa taifa aridhike kwamba mashtaka ni ya haki na seneti imeyaidhinisha.

(3) wakati wa kusimamishwa kwa muda katika kifungu hiki, mipango itafanywa ya kutekeleza majukumu ya kaunti kulingana na Sheria za Bunge.

(4) Seneti yaweza, wakati wowote, kufutilia mbali kusimamishwa huko kwa muda.

(5) kusimamishwa kwa muda katika kifungu hiki hakuwezi kuwa kwa zaidi ya siku tisini.

(6) Muda uliotengwa kulingana na Ibara ya (5) unapomalizika uchaguzi wa Serikali mwafaka ya kaunti utafanyika.

**Sehemu ya 7 – Jumla**

**Sifa za wagombea uanachama wa baraza la kaunti**

**193.** (1) Labda azuiwe na ibara ya (2), mtu atahitimu kugombea uanachama katika baraza la kaunti kama-

(a) amesajiliwa kama mpiga kura;

(b) anatimiza mahitaji yote ya kielimu, tabia nzuri na maadili mema kama inavyotakikana kwa mujibu wa Katiba au Sheria ya Bunge; na

(c) ama-

(i) ameteuliwa na chama cha kisiasa; au

(ii) ni mgombeaji wa kujitegemea aliyeungwa mkono na watu mia tano waliosajiliwa kama wapiga kura katika wadi husika.

(2) Mtu hataruhusiwa kugombea kiti katika baraza la kaunti iwapo mtu huyo-

(a) ana cheo Serikalini au afisi ya umma, mbali na hiyo ya baraza la kaunti anayowania kiti;

(b) amekuwa na cheo katika Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka, wakati wowote ule

Draft for approval

katika miaka mitano iliyotangulia tarehe ya uchaguzi.

(c) hajakuwa raia wa Kenya kwa miaka isiyopungua kumi iliyotangulia tarehe ya uchaguzi;

(d) hana akili timamu;

(e) ni mufilisi;

(f) anatumikia kifungo gerezani cha miezi sita au zaidi; au

(g) amepatikana, kulingana na sheria yoyote, kwamba ametumia vibaya afisi ya umma ama kwa njia yoyote ile kukiuka kanuni za Sura ya sita.

(3) Mtu hatazuiwa kulingana na ibara ya (2) ila tu kama uwezekano wa kukata rufaa ama kesi yake kushughulikiwa upya kwa kifungo chake na mbinu zote za kujitetea zimekwisha.

**Kuondoka afisini kama mwanachama wa baraza la kaunti**

**194**. (1) Afisi ya mbunge wa baraza unge la kaunti huwa wazi kutokana na-

(a) iwapo mbunge atafariki;

(b) kama mbunge atakosa vikao vinane vya bunge bila idhini iliyoandikwa kwa spika wa bunge, na hawezi kutoa sababu za kutosha za kutohudhuria vikao hivyo;

(c) kama mtu huyo ataondolewa afisini kwa mujibu wa Katiba hii au kwa mujibu wa sheria ya kifungu cha 80.

(d) mbunge akijiuzulu kwa kumwandikia spika wa bunge;

(e) iwapo baada ya kuchaguliwa kuwa mbunge-

(i) kama mwanachama wa chama cha kisiasa atajiuzulu, ama ikichukuliwa amejiuzulu kutoka kwa chama kwa mujibu wa sheria inayotajwa katika Ibara ya (2); au

(ii) baada ya kuchaguliwa bungeni kama mgombea huru, anajiunga na chama cha kisiasa

(f) kukamilika kwa kipindi cha bunge; au

(g) kama mwanachama ataondolewa afisini kwa misingi ya uchaguzi ilivyowekwa katika Kifungu cha 193 (2).

(2) Bunge litatunga sheria itakayoonyesha hali ambapo mwanachama wa chama cha kisiasa, atachukuliwa kuwa amejiuzulu kutoka kwa chama, kwa mujibu wa Ibara ya (1) (e).

Draft for approval

**Uwezo wa baraza la kaunti kuita mashahidi**

**195**. (1) Baraza la kaunti ama kamati yake yoyote, lina uwezo wa kumwita mtu yeyote mbele yake ili kutoa ushahidi au habari zinazotakikana.

(2) Kwa sababu ya ibara ya (1), baraza lina mamlaka sawa na Mahakama kuu ya:

(a) kuhimiza mashahidi kuhudhuria na kuwahoji baada ya kula kiapo, kukiri au hali nyingine;

(b) kuwalazimisha mashahidi kuwasilisha nyaraka muhimu;

(c) kutafuta idhini ya kuwahoji mashahidi ng'ambo.

**Kushiriki kwa umma, mamlaka, haki na kinga kwa baraza la kaunti**

**196.** (1) Baraza la kaunti –

(a) litaendesha shughuli zake kwa uwazi, na kufanya vikao vyake na vile vya kamati zake mbele ya umma; na

(b) kuhimiza watu kushiriki katika kutunga sheria na katikacshughuli nyingine za baraza na kamati zake.

(2) Baraza la kaunti halitawaacha nje watu, au vyombo vya habari, katika kikao chochote ila katika hali ambapo spika wa bunge ametoa uamuzi na sababu za kutosha za kufanya hivyo.

(3) Baraza litatunga sheria itakayoonyesha mamlaka, haki, na kinga ya mabaraza ya kaunti, jamii na wanachama wake.

Draft for approval

**Usawa na tofauti za kijinsia katika baraza la kaunti**

**197.** (1) Wanachama wa baraza lolote la kaunti au wa kamati ya mamlaka kuu ya kaunti, wasiwe zaidi ya thuluthi mbili katika jinsia moja.

(2) Bunge litatunga sheria-

(a) kuhahakikisha kwamba tofauti za kijamii na za kitamaduni katika nchi zinaangaziwa kwenye mabaraza na kamati za mamlaka kuu za kaunti ; na

(b) kuweka mikakati ya kuwalinda walio wachache katika kaunti hizo.

**Serikali ya kaunti katika kipindi cha mpito**

**198.** Wakati uchaguzi unapoendelea ili kuunda bunge la kaunti kwa mujibu wa Sura hii, kamati kuu ya kaunti, ilivyoundwa mwisho bado inakuwa na umilisi na uwezo wa kuendesha shughuli za usimamizi hadi pale kamati kuu itakapoundwa upya baada ya uchaguzi.

**Kuchapishwa kwa sheria za kaunti**

**199**. (1) Sheria za kaunti hazitaanza kutekelezwa hadi zitangazwe katika Gazeti Rasmi la Serikali.

(2) Sheria za kitaifa, na zile za kaunti zinaweza kupendekeza masharti zaidi kuhusu uchapishaji wa sheria za Serikali ya kaunti..

**Sheria ya kuhusu Sura hii**

**200**. (1) Bunge litatunga sheria katika masuala yote muhimu au ya lazima kuidhinisha utekelazaji wa Sura hii.

(2) Hasa, sheria inaweza kubuniwa ili iangazie-

(a) usimamizi wa mji mkuu, majiji mengine na miji mingine;

(b) kuhamishwa kwa majukumu na mamlaka kutoka kwa kiwango kimoja cha Serikali hadi kingine, pamoja na kuhamisha uwezo wa kutunga sheria kutoka kwa Serikali ya kitaifa hadi Serikali za kaunti;

(c) taratibu za uchaguzi ama uteuzi wa watu, na kuwatoa mamlakani katika Serikali za kaunti, pamoja na kuhitimu kwa wapiga kura na wagombeaji wa viti.

(d) taratibu za mabaraza na kamati kuu pamoja na uenyekiti, mfululizo wa mikutano, uhudhuriaji na upigaji kura; na

(e) kusimamishwa kwa muda kwa mabaraza na kamati kuu.

Draft for approval

## SURA YA KUMI NA MBILI

## FEDHA ZA UMMA

### Sehemu ya I – Kanuni na utaratibu wa fedha za umma

### Kanuni za fedha za Umma

**201.** Kanuni zifuatazo zitaongoza Vifungu vyote vya fedha za umma katika taifa:-

(a) Kutakuwa na uwazi na uwajibikaji, ikiwa ni pamoja na kuhusika kwa umma katika masuala ya kifedha.

(a) Mfumo wa fedha za umma utakuza jamii yenye usawa, hasa:-

(i) Mzigo wa utozaji ushuru utasawazishwa;.

(ii) Mapato yanayopatikana katika kiwango cha kitaifa yatagawanywa sawa kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti;.

(iii) Matumizi yatachangia usawazishaji wa kimaendeleo nchini, ikiwa ni pamoja na mgao maalum kwa makundi ya watu kutoka maeneo yaliyotengwa; na

(b) Mizigo na faida za matumizi ya mapato na ukopaji wa umma itagawanywa sawa kwa kizazi hiki na vizazi vijavyo;

(c) fedha za umma lazima zitumiwe kwa busara na uwajibikaji; na

(d) Usimamizi wa fedha lazima uwajibikiwe vyema na ripoti ya hazina ya serikali iwe wazi.

Draft for approval

### Ugawaji sawa wa mapato ya kitaifa

**202.** (1) Mapato yanayozalishwa katika kiwango cha kitaifa yatagawanywa sawa kwa serikali ya kitaifa na serikali za kaunti;

(2) Serikali za kaunti zinaweza kupewa mgao wa ziada kutoka kwa sehemu ya mapato ya serikali ya kitaifa, kwa masharti au bila masharti.

### Ugavi sawa na sheria nyingine za kifedha

**203.** **(1)** Vigezo vifuatavyo vitatumiwa kutoa uamuzi kuhusu mgao sawa uliotajwa katika kifungu cha 202 na katika sheria zote za kitaifa kuhusu serikali za kaunti kama zilivyotungwa kwa mujibu wa masharti ya sura hii –

(a) masilahi ya kitaifa;

(b) kifungu kingine ambacho kinahitajika kwa mujibu wa deni la umma na mahitaji mengine ya kitaifa;

(c) mahitaji ya serikali ya kitaifa yatakayoamuliwa kwa misingi ya kigezo cha kutopendelea;

(d) haja ya kuhakikisha kuwa serikali za kaunti zina uwezo wa kutekeleza majukumu zilizopewa;

(e) uwezo wa kifedha na ufanisi wa serikali za kaunti;

(f) maendeleo na mahitaji mengine ya serikali za kaunti;

(g) tofauti za kiuchumi miongoni na kati ya kaunti na sababu ya kutatua matatizo hayo;

(h) haja ya kuchukua hatua kwa mujibu wa maeneo na makundi yaliyotengwa;

(i) haja ya kuboresha uchumi kwenye kila kaunti na kutoa motisha kwa kila kaunti kuboresha uwezo wake wa kuzalisha mapato;

(j) kutamani mgao wa mapato ulio thabiti na unaoweza kutabirika; na

(k) haja ya wepesi katika kukabiliana na majanga na mahitaji mengine ya muda katika misingi ya kigezo cha kutopendelea.

(2) Kwa kila mwaka wa fedha, mgao unaolingana wa mapato yanayozalishwa na taifa ambayo yatagawiwa serikali za kaunti hayatapungua asilimia kumi na tano ya mapato yote ambayo serikali ya kitaifa inayozalisha.

(3) Jumla ya fedha zilizotajwa katika Ibara ya (2) zitapigwa hesabu katika misingi ya ukaguzi wa juzi zaidi wa hesabu ya mapato yaliyokusanywa, kama itakavyoidhinishwa na Baraza  la Kitaifa.

Draft for approval

**Hazina ya Usawazishaji**

**204.** (1) Kutaundwa Hazina ya Usawazishaji ambayo itachukua asilimia moja unusu ya mapato yote yanayozalishwa na serikali ya kitaifa kila mwaka, katika misingi ya ukaguzi wa hesabu za mapato uliofanywa  karibuni zaidi, kama itakavyoidhinishwa na Baraza la Kitaifa.

(2) Serikali ya kitaifa itatumia hazina ya kusawazisha kutoa huduma za kimsingi zikiwa ni pamoja na maji, barabara, matibabu na umeme katika maeneo yaliyotengwa hadi kiwango kitakachoboresha huduma hizo katika maeneo hayo kiwe sawa na kiwango kilicho maeneo mengine, iwezakanavyo.

(3) Serikali ya kitaifa inaweza kutumiaHazina ya Kusawazisha:-

(a) iwapo matumizi ya fedha za hazina hiyo yameidhinishwa tu katika Mswada wa Matumizi ya Fedha uliopitishwa na Bunge; na

(b) ama kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja kupitia kwa misaada yenye masharti ambayo inahusisha makundi yaliyotengwa .

(4) Tume ya Ugavi wa Mapato itashauriwa na mapendekezo yake kutiliwa maanani mbele ya Bunge ili kupitisha mswada wa kuidhinisha matumizi ya fedha katika Hazina ya Usawazishaji.

(5) Fedha zozote ambazo hazitakuwa zimetumiwa katika Hazina ya Usawazishaji, zitasalia katika hazina hiyo kwa matumizi kwa mujibu wa ibara ya (2) na (3) katika mwaka wa fedha utakaofuata.

(6) Kifungu hiki kitaisha baada ya miaka ishirini kuanzia tarehe kitakapoanza kutekelezwa, kutegemea ibara ya (7).

(7) Bunge linaweza kupitisha sheria ya kuondoa utekelezaji wa ibara ya (6) kwa kipindi cha ziada cha miaka mahususi, kutegemea ibara ya (8).

(8) Kupitisha sheria katika ibara ya (7) lazima kuungwe mkono na zaidi ya nusu ya wabunge wote wa Baraza la Kitaifa, na zaidi ya nusu ya wajumbe wa serikali za kaunti katika Seneti.

(9) Fedha hazitaondolewa katika Hazina ya Usawazishaji hadi pale Msimamizi wa Bajeti atakapoidhinisha kutolewa kwake.

Draft for approval

**Mashauriano kuhusu sheria za Kifedha zinazoathiri Kaunti**

**205.** (1) Wakati mswada ambao unahusisha ugavi wa mapato, au suala lolote la kifedha linalohusu serikali za kaunti utakapochapishwa, Tume ya ugavi wa Mapato itachunguza mahitaji yake na kutoa mapendekezo kwa Baraza la Kitaifa na Seneti.

(2) Mapendekezo yoyote ya Tume hii yatawasiliswa Bungeni, na kila bunge litachunguza mapendekezo hayo kabla ya kupiga kura.

**Sehemu ya 2 – Fedha zingine za Umma**

**Mfuko wa Jumla na Mfuko wa Jumla na Fedha zingine za Umma.**

**206.** (1) Mfuko wa Jumla umeundwa, ambao utahifadhi fedha zilizozalishwa au kupokelewa kwa minajili ya serikali ya kitaifa, isipokuwa fedha ambazo –

(a) kwa sababu maalum zilizotengwa kutoka kwa Hazina hiyo na Sheria ya Bunge na ambazo zitawekwa kwa hazina tofauti ya umma iliyobuniwa kwa lengo maalum; au

(b) zinaweza, chini ya Sheria ya Bunge, kuhifadhiwa na taasisi ya serikali iliyozipokea kwa lengo la kugharamia mahitaji ya taasisi hiyo.

(2) Fedha zinaweza kutolewa kutoka kwa Mfuko wa Jumla iwapo tu –

(a) matumizi yake yameidhinishwa na Sheria ya Bunge;

(b) kwa mujibu wa kifungu cha 222 au 223; au

(c) kulipa madeni ya mfuko huo wa jumla kama ilivyoidhinishwa na Katiba hii au Sheria ya Bunge.

(3) Fedha hazitatolewa kwa hazina nyingine yoyote ya fedha za umma ila tu kutoka kwa Mfuko wa Jumla, isipokuwa tu ikiwa kutolewa kwa fedha hizo kumeidhinishwa na Sheria ya Bunge.

(4) Fedha hazitatolewa kwa Mfuko wa Jumla ila tu mpaka Msimamizi wa Bajeti atakapoidhinisha.

**Hazina za mapato za Serikali za Kaunti**

**207.** (1) Hazina ya Mapato ya kila serikali ya Kaunti imeundwa. Hazina hii italipwa pesa zote zilizozalishwa au kupokelewa na, au kwa niaba ya serikali ya kaunti, isipokuwa fedha ambazo kwa sababu maalum zimetengwa na Sheria ya Bunge.

(2) Fedha zinaweza kutolewa kutoka kwa Hazina ya Mapato ya serikali ya Kaunti kwa ajili :-

(a) Kama malipo dhidi ya Hazina ya Mapato ambayo yamekubaliwa na Sheria ya Bunge au sheria za serikali hiyo ya kaunti; au

(b) kama ilivyoidhinishwa na sheria ya matumizi ya fedha katika serikali hiyo ya kaunti.

(3) Fedha hazitatolewa kwa Hazina ya Mapato mpaka Msimamizi wa Bajeti atakapoidhinisha.

(4) Sheria ya Bunge inaweza –

(a) kutoa idhini zaidi ya kutoa fedha kutoka kwa Hazina ya Mapato ya Serikali ya Kaunti.

(b) kuruhusu serikali za kaunti kuanzisha hazina nyingine za mapato na usimamizi wa hazina kama hizo.

**Hazina ya Dharura**

**208.** (1) Kutabuniwa Hazina ya Dharura, ambayo shughuli zake zitaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge.

(2) Sheria ya Bunge itaruhusu kutolewa kwa fedha kutoka kwa Hazina ya Dharura iwapo waziri anayehusika na Fedha ameridhika kuwa pana jambo la dharura linalohitaji matumizi ambayo hayapo chini ya mamlaka yoyote.

Draft for approval

**Sehemu ya 3 – Nguvu za Kuzalisha Mapato na Deni la Umma**

**Mamlaka ya Kutoza Kodi na Ushuru**

**209.** (1) Ni serikali ya kitaifa pekee ambayo imepewa uwezo wa kutoza-

(a) kodi ya mapato;

(b) ushuru wa thamani;

(c) ushuru wa forodha na kodi nyingine katika bidhaa zinazoingizwa na kuuzwa nje ya nchi.; na

(d) mapato ya ushuru.

(2) Sheria ya Bunge inaweza kuipa mamlaka serikali ya kitaifa kutoza ushuru au kodi nyingine yoyote, isipokuwa ushuru uliotajwa katika ibara ya (3) (a) na (b).

(3) Serikali ya kaunti inaweza kutoza:-

(a) ushuru kwa mali;

(b) kodi za burudani; na

(c) na kodi nyingine yoyote ambayo imeruhusiwa na Sheria ya Bunge.

(4) Serikali ya kitaifa na serikali za kaunti zinaweza kutoza ushuru wa huduma.

(5) Utozaji ushuru na mamlaka mengine ya kuzalisha mapato ya serikali ya kaunti hautafanywa kwa njia ambayo inakiuka sera za kiuchumi za kitaifa, shughuli za kiuchumi zinazotekelezwa ndani ya mipaka ya kaunti au uzungushwaji wa bidhaa katika nchi nzima, huduma, mtaji au ajira.

Draft for approval

**Kutoza Ushuru**

**210.** (1) Hakuna kodi yoyote au malipo ya leseni yanayoweza kuondolewa au kubadilishwa ila kwa mujibu wa sheria.

(2) Iwapo sheria itaruhusu kufutiliwa mbali kwa ushuru au malipo ya leseni –

(a) rekodi ya kufutilia mbali itahifadhiwa kwa umma ambayo itaonyesha sababu za kila kufutilia mbali; na

(b) kila kufutiliwa mbali; pamoja na sababu zake lazima zifikishwe kwa Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu.

(3) Hakuna sheria ambayo itamwondolea au kuamrisha mhudumu yeyote wa umma kutolipa kodi kwa sababu za –

(a) mamlaka yanayoshikiliwa na afisa huyo; au

(b) aina ya kazi anayofanya afisa huyo.

**Ukopaji wa Serikali ya Kitaifa**

**211.** (1) Bunge kupitia kwa sheria, linaweza –

(a) kueleza hali ambazo serikali ya kitaifa inaweza kukopa; na

(b) kuweka kanuni za kutoa taarifa.

(2) Kati ya kipindi cha siku saba baada ya Bunge kutoa ombi, Waziri anayehusika na fedha atawasilisha habari kwa kamati husika kuhusu mkopo wowote au dhamana, pamoja na habari yote muhimu ili kuonyesha –

(a) kiwango cha madeni yote ikiwa ni pamoja na mtaji na jumla ya faida inayodaiwa;

(b) mkopo huo ulivyotumiwa au utakavyotumiwa;

(c) Mikakati iliyopo ya kulipa mkopo huo; na

(d) hatua zilizochukuliwa katika kulipa mkopo huo.

**Ukopaji wa kaunti**

**212.** Serikali ya kaunti inaweza kukopa iwapo:-

(a) Serikali ya kitaifa itadhamini mkopo huo; na

(b) baraza la serikali hiyo ya kaunti limeidhinisha.

**Udhamini wa Mikopo na Serikali ya Kitaifa.**

**213.** (1) Sheria ya Bunge itawekea kanuni na masharti ambayo kwayo serikali ya kitaifa inaweza kudhamini mikopo.

(2) Kati ya kipindi cha miezi miwili baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha, serikali ya taifa itachapisha ripoti itakayoonyesha dhamana zote ilizozitoa wakati wa kipindi cha mwaka huo.

**Deni la Umma**

**214.** (1) Deni la umma, ni deni linalohusishwa na Mfuko wa Jumla, lakini Sheria ya Bunge inaweza kuamuru deni hili au sehemu yake idaiwe hazina nyingine za umma.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “deni la umma” linamaanisha madeni yote yanayohusisha mikopo, dhamana na amana iliyotolewa au kudhaminiwa na serikali ya kitaifa.

Draft for approval

**Sehemu ya 4 – Ugavi wa Mapato**

**Tume ya Ugavi wa Mapato**

**215.** (1) Kutabuniwa Tume ya Ugavi wa Mapato.

(2) Tume hii itajumuisha watu wafuatao watakaoteuliwa na Rais-

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Baraza la Kitaifa;

(b) Watu wawili walioteuliwa na vyama vya kisiasa vinavyowakilishwa katika Baraza la Kitaifa kutegemea idadi ya wabunge wa chama bungeni;

(c) Watu watano walioteuliwa na vyama vya kisiasa vinavyowakilishwa katika seneti kwa kutegemea idadi yao ya uwakilishi katika seneti; na

(d) Katibu Mkuu katika wizara inayosimamia fedha.

(3) Watu watakaoteuliwa kwa mujibu wa ibara ya (2) hawatakuwa wabunge.

(4) Ili kuhitimu kuwa kamishna wa Tume hii chini ya ibara ya (2) (a), (b) au (c), mtu lazima awe na tajriba pana katika taaluma ya masuala ya kifedha na uchumi.

**Majukumu ya Tume ya Ugavi wa Mapato**

**216.** (1) Jukumu kuu la Tume ya Ugavi wa Mapato ni kutoa mapendekezo kuhusu ugavi unaozingatia usawa wa mapato yanayozalishwa na serikali ya kitaifa –

(a) kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti; na

(b) miongoni mwa serikali za kaunti.

(2) Tume hii pia itatoa mapendekezo kuhusu ufadhili wa serikali za kaunti na usimamizi wa fedha katika serikali hizi; kwa mujibu wa Katiba hii na sheria za kitaifa.

(3) Katika kutoa mapendekezo, Tume hii itahitaji:-

(a) kuinua na kudumisha kigezo kilichotajwa katika kifungu cha 203 (1);

(b) kwa wakati mwafaka, kueleza na kuwezesha njia za kuzalisha mapato za serikali ya kitaifa na serikali za kaunti ; na

(c) kuhimiza uwajibikaji wa kifedha.

(4) Tume itaamua, kuchapisha na kuchunguza kila mara sera ambayo itatoa kigezo cha kutambua maeneo yaliyotengwa katika kifungu cha 204 (2).

(5) Tume itawasilisha mapendekezo yake kwa Seneti, Baraza la Kitaifa, Serikaliya kitaifa, mabaraza ya kaunti na kamati kuu ya Kaunti.

Draft for approval

**Mgao Unaolingana wa Mapato**

**217.** (1) Mara moja baada ya kila miaka mitano, Baraza la Seneti litatoa mapendekezo kuhusu misingi ya kutumiwa katika ugavi wa mapato ya kitaifa yanayogawiwa kila serikali ya kaunti kila mwaka.

(2) Katika kutoa mapendekezo ya vigezo vya kutumiwa kugawa mapato yaliyotajwa katika ibara ya (1),Seneti:-

(a) itatilia maanani kigezo katika kifungu cha 203 (1);

(b) itaitisha na kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Ugavi wa Mapato;

(c) itawashauri Magavana wa serikali za kaunti, Waziri anayesimamia fedha na asasi nyingine yoyote ya serikali ya kaunti; na

(d) itawaalika watu, ikiwa ni pamoja na makundi ya wataalamu, kutoa mapendekezo yao.

(3) Katika kipindi cha kati ya siku kumi baada ya Seneti kuidhinisha pendekezo chini ya ibara ya (1), Spika wa Seneti atawasilisha pendekezo hilo kwa Spika wa Baraza la Kitaifa.

(4) Katika kipindi cha kati ya siku sitini baada ya maamuzi ya Seneti kuwasilishwa kama inavyotajwa katika ibara ya (3), Baraza la Kitaifa litachunguza pendekezo hilo na kulipigia kura ili kuliidhinisha kwa kulifanyia au kutolifanyia marekebisho, au kulikataa.

(5) kiwa Baraza la Kitaifa:-

(a) halitapiga kura kwa pendekezo hili kwa kipindi cha siku sitini, basi itachukuliwa kwamba pendekezo hili limeidhinishwa na Baraza la Kitaifa bila marekebisho;

(b) litapiga kura kwa pendekezo hili, pendekezo litakuwa:-

(c) limefanyiwa marekebisho iwapo wajumbe wasiopungua thuluthi mbili wataunga mkono marekebisho;

(i) litakatiliwa iwapo tu wajumbe wa bunge wasiopungua thuluthi mbili watalipigia kura ya kulikataa, bila kujali kama limefanyiwa marekebisho na Baraza la Kitaifa au la; au

(ii) kuidhinishwa, kwa njia yoyote ile.

(6) Iwapo Baraza la Kitaifa litaidhinisha pendekezo lililofanyiwa marekebisho au kulikataa pendekezo, basi Seneti itakuwa na uchaguzi wa:-

(a) kuchukua pendekezo jipya chini ya ibara ya (1), katika hali hii masharti ya ibara ya (4) na (5) yatatumiwa upya;

(b) kuomba suala hili liwasilishwe kwa kamati ya pamoja ya mabaraza yote mawili ya Bunge kwa upatanisho chini ya kifungu cha 113, utakaozingatia marekebisho muhimu.

Draft for approval

(7) Pendekezo hili chini ya kifungu hiki kitakachokuwa kimeidhinishwa chini ya ibara ya (5) basi kitaendelea kutekelezwa hadi wakati ambapo pendekezo jipya litakapoidhinishwa.

(8) Licha ya ibara ya (1), Seneti, kwa uamuzi ikiwa umeungwa mkono na wanachama wasiopungua thuluthi tatu, inaweza kulifanyia marekebisho pendekezo lililoidhinishwa.

(9) ibara ya (2) hadi (8), na marekebisho muhimu, zinataja pendekezo chini ya ibara ya (8).

Draft for approval

**Miswada ya Ugavi wa kila mwaka wa Mapato.**

**218.** (1) Kipindi kisichopungua miezi miwili baada ya kukamilika kwa mwaka wa kifedha, bungeni kutawasilishwa –

(a) mswada wa kugawa mapato, ambao utagawa mapato yaliyozalishwa na serikali ya kitaifa kwa serikali za kaunti kwa mujibu wa Katiba hii; na

(b) mswada wa kutenga mapato kwa serikali za kaunti, ambao utazigawia serikali za kaunti na mapato yaliyotengwa kwa serikali za kaunti katika misingi ya pendekezo lililoamuliwa chini ya kifungu cha 217.

(2) Kila mswada unaohitajika na ibara ya (2) utaambatanishwa na memoranda itakayoweka wazi –

(a) maelezo ya mgao wa mapato kama ilivyopendekezwa na mswada;

(b) utathmini wa mswada katika misingi ya kigezo kilichotajwa kwenye Kifungu cha 203 (1); na

(c) mukhtasari wa tofauti zozote muhimu kutoka kwa mapendekezo ya Tume, na maelezo kwa kila tofauti iliyopo.

**Uhamishaji wa Ugavi sawa**

**219.** Mgao wa mapato yaliyozalishwa na serikali ya kitaifa nchini utahamishwa kwa kaunti bila kucheleweshwa pasipo sababu na bila kupunguzwa, isipokuwa wakati uhamishaji huu umesimamishwa chini ya Kifungu cha 225.

**Sehemu ya 5 – Bajeti na Matumizi**

**Umbo, yaliyomo na wakati za bajeti.**

**220.** (1) Bajeti za serikali ya kitaifa na zile za serikali za kaunti zitajumuisha –

(a) makadirio ya mapato na matumizi, zikionyesha tofauti kati ya matumizi ya kawaida na yale ya kimaendeleo;

(b) mapendekezo ya kufadhili upungufu wowote unaotarajiwa kwa kipindi cha matumizi;

(c) Mapendekezo kuhusu kukopa na madeni yoyote ambayo yataongeza deni la umma katika kipindi cha mwaka utakaofuata.

(2) Sheria za kitaifa zitaonyesha –

(a) muundo wa mipango ya maendeleo na bajeti za nchi;

(b) wakati mipango na bajeti za serikali za kaunti zitawasilishwa kwa mabunge ya kaunti; na

(c) njia na jinsi ya kufanya mashauri kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti katika harakati za kutayarisha na mipango na bajeti.

**Mswada wa Makadirio ya Bajeti na Matumizi ya Mwaka**

**221.** (1) Kwa kipindi kisichopungua miezi miwili kabla ya kukamilika kwa kila mwaka wa kifedha, waziri anayehusika na fedha, atawasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka ufuatao wa fedha kwa Baraza la Kitaifa.

(2) Makadirio yaliyotajwa katika ibara ya (1) –

(a) yatajumlisha makadirio ya matumizi kutoka kwa Hazina ya Usawazishaji; na

(b) itakayokuwa kwa muundo, na kwa mujibu wa utaratibu ufaao na kuambatana na kanuni zilizoratibiwa na Sheria ya Bunge.

(3) Baraza la Kitaifa litazingatia makadirio yaliyowasilishwa chini ya kifungu cha (1) pamoja na makadirio yanayowasilishwa na Tume ya Huduma za Bunge na Msajili Mkuu wa Mahakama chini ya Kifungu cha 127 na 173, mtawalia.

(4) Kabla ya Baraza la Kitaifa kuzingatia makadirio ya mapato na matumizi; kamati ya Bunge itajadili na kuchunguza makadirio hayo na kutoa mapendekezo yake kwa Bunge.

(5) Katika kujadili na kuchunguza makadirio hayo, kamati itahusisha umma na mapendekezo yake yatatiliwa maanani wakati kamati hiyo itakapowasilisha mapendekezo hayo kwa Baraza la Kitaifa.

(6) Wakati makadirio ya matumizi ya serikali ya kitaifa, makadirio ya matumizi ya mahakama na Baraza la Kitaifa, yatakuwa yameidhinishwa na Baraza la Kitaifa, yatajumlishwa katika Mswada wa Matumizi ya Fedha, utakaowasilishwa kwa Baraza la Kitaifa ili kuidhinisha kutolewa kwa fedha za matumizi kutoka kwa Mfuko wa Jumla, na matumizi ya fedha hizo kwa madhumuni yaliyotajwa katika mswada.

(7) Mswada wa matumizi ya fedha uliotajwa katika ibara ya (6) hautajumlisha matumizi yanayodaiwa kutoka kwa Mfuko wa Jumla na Katiba hii au Sheria ya Bunge.

Draft for approval

**Matumizi Kabla ya Kuidhinishwa kwa Bajeti ya Mwaka**

**222.** (1) Iwapo sheria ya matumizi ya fedha haitakuwa imeidhinishwa kufikia mwanzo wa mwaka wa fedha, Baraza la Kitaifa linaweza kuamuru kutolewa kwa pesa kutoka Mfuko wa Jumla wa fedha.

(2) Fedha zitakazotolewa chini ya ibara ya (1) –

(a) zitatumiwa kwa minajili ya kuendesha shughuli muhimu za serikali ya kitaifa katika mwaka huo hadi wakati ambapo mswada wa matumizi ya fedha utakapoidhinishwa;

(b) kwa jumla zisizidi nusu ya fedha zilizopendekezwa katika makadirio ya matumizi ya mwaka huo yaliyowasilishwa bungeni; na

(c) ziwekwe katika vitengo tofauti vya matumizi kwa sababu ya huduma mbalimbali zilizokusudiwa katika mswada wa matumizi ya fedha.

**Matumizi ya Ziada**

**223.** (1) Kwa kuzingatia ibara ya (2) hadi (4), serikali ya kitaifa inaweza kutumia fedha ambazo hazijaidhinishwa iwapo –

(a) Fedha zilizotengwa kwa madhumuni fulani katika sheria ya matumizi hazikutosha au kumezuka haja ya matumizi ambayo hayakuwa na mgao katika sheria ya matumizi ya fedha; au

(b) fedha zimechukuliwa kutoka kwenye Hazina ya Ziada ya fedha.

(2) Idhini ya Bunge ya kutumia fedha chini ya kifungu hiki itahitajika kati ya miezi miwili baada ya fedha kuchukuliwa mara ya kwanza, kulingana na ibara ya (3).

(3) Iwapo Bunge litakuwa limevunjwa wakati wa kipindi kinachotajwa katika ibara ya (2), au vikao vya bunge vinaendelea na bunge kuvunjwa kabla ya idhini kutolewa, idhini lazima itolewe kati ya majuma mawili pindi tu vikao vingine vitakapoanza.

(4) Wakati Baraza la Kitaifa litakapokuwa limeidhinisha matumizi chini ya ibara ya (2), mswada na matumizi ya fedha utawasilishwa kwa mgao wa fedha zilizotumika.

(5) Katika mwaka wowote wa matumizi ya fedha za serikali, serikali ya kitaifa chini ya kifungu hiki haiwezi kutumia zaidi ya asilimia kumi ya fedha zilizotengewa bunge kwa mwaka huo, ila katika hali maalum Bunge limeidhisha kiasi cha juu .

**Miswada ya Matumizi ya fedha za Kaunti**

**224.** Katika misingi ya mswada wa mgao wa mapato uliopitishwa na Bunge chini ya kifungu cha 218, kila serikali ya kaunti itaandaa na kutumia bajeti yake ya mwaka wa matumizi ya fedha, jinsi ulivyoandikwa katika misingi na utaratibu uliowekwa na sheria ya Bunge.

Draft for approval

**Sehemu ya 6 – Udhibiti wa fedha za Umma.**

**Udhibiti wa fedha.**

**225.** (1) Sheria ya Bunge itaidhinisha kuanzishwa, na kuipa majukumu Hazina ya Kitaifa.

(2) Bunge litapitisha sheria itakayohakikisha usimamizi wa matumizi na uwajibikaji katika serikali zote na kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba zimetekelezwa.

(3) Sheria inayotajwa katika ibara ya (2) inaweza kuamuru waziri anayehusika na fedha kusimamisha uhamishaji wa fedha kwa kitengo fulani cha serikali au shirika lolote la serikali –

(a) iwapo tu kuna ukiukaji uliokithiri mipaka au ukiukaji wa kila mara wa hatua zilizowekwa na sheria; na

(b) kulingana na masharti ya ibara ya (4) na (7).

(4) Uamuzi wa kusimamia uhamishaji wa fedha kama ilivyoelezwa katika Ibara ya (3) haiwezi kusimamisha uhamishaji wa zaidi ya asilimia hamsini ya fedha zilizotengewa serikali ya kaunti.

(5) Uamuzi wa kusimamisha uhamishaji wa fedha kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha (3) –

(a) hauwezi kusimamisha uhamishaji kwa siku zaidi ya sitini; na

(b) unaweza kutekelezwa mara moja, lakini unaweza kufanya kinyume ila tu, kati ya siku thelathini baada ya tarehe ya maamuzi hayo, Bunge linauidhinisha kwa pendekezo linalopitishwa na viwango vyote mawili vya Bunge.

(6) Bunge linaweza kuweka upya uamuzi wa kusimamisha uhamishaji wa fedha lakini kwa siku zisizozidi sitini kwa wakati mmoja.

(7) Bunge linaweza kuidhinisha au kuweka upya uamuzi wa kusimamisha uhamishaji wa fedha isipokuwa –

(a) Msimamizi wa Bajeti amewasilisha ripoti kuhusu suala hili Bungeni; na

(b) shirika hilo la umma lipewe nafasi ya kujibu madai dhidi yake, na kujitetea mbele ya kamati husika ya Bunge.

**Akaunti na ukaguzi wa mashirika ya Umma.**

**226.** (1) Sheria ya Bunge itawezesha –

(a) kuhifadhi na kukaguliwa kwa rekodi za fedha za serikali na mashirika mengine ya umma, na kuweka hatua za kuhakikisha usimamizi wazi na madhubuti wa fedha; na

(b) kuweka Afisa wa Uhasibu katika kila shirika la umma kwenye kiwango cha kitaifa na katika serikali za kaunti.

Draft for approval

(2) Afisa wa Uhasibu wa shirika la umma katika kiwango cha kitaifa anawajibikia Baraza la Kitaifa kwa usimamizi fedha katika shirika hilo, na afisa wa uhasibu wa shirika la umma katika kiwango cha kaunti anawajibikia baraza la kaunti kwa usimamizi wa fedha.

(3) Kwa mujibu wa ibara ya (4), hesabu za vitengo vya serikali na nchi zitakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu.

(4) Hesabu za mkaguzi mkuu wa mahesabu zitakagulia na ripoti kutolewa na mhasibu atakayeteuliwa na Baraza la Kitaifa.

(5) Mhudumu wa Afisi ya Umma, ikiwa ni pamoja na afisi ya kisiasa, akiamuru au kuidhinisha matumizi ya fedha za umma kinyume na sheria au maagizo, mtu huyu atawajibikia hasara yoyote itakayotokana na matumizi hayo na atagharimia hasara hiyo, angali akiwa afisini au la.

**Ununuzi wa bidhaa na huduma za umma.**

**227.** (1) Wakati kitengo cha serikali au shirika lolote la umma linaponunua bidhaa au huduma, ununizi huo utafanywa kwa njia ya haki, usawa, uwazi, yenye ushindani na ya kupunguza gharama.

(2) Sheria ya Bunge itatoa mwongozo wa jinsi sera zinazohusishwa na ununuzi na uuzaji wa mali zitavyotekelezwa na itaamuru kuzingatiwa kwa suala mojawepo au masuala yote yafuatayo –

(a) vigezo vya kupewa kipaumbele wakati wa kutoa idhini za ununizi;

(b) kuwalinda na kuwatetea watu, au makundi ya watu ambao awali walinyanyaswa na ushindani usio na haki au uliowatenga;.

(c) kuweka vikwazo dhidi ya wanakandarasi ambao utendakazi wao hautimizi viwango vilivyokubaliwa kitaaluma, kimapatano au kisheria; na

(d) kuweka vikwazo dhidi ya watu wanaokiuka ulipaji kodi, au ambao wamehusika kwenye ufisadi au wenye makosa makubwa ya ukiukaji wa sheria za uajiri kwa haki.

**Sehemu ya 7 – Maafisa na kifedha na Taasisi**

**Msimamizi wa Bajeti**

**228.** (1) Kutakuwa na Msimamizi wa Bajeti atakayependekezwa na Rais, kuidhinishwa na Baraza la Kitaifa na kuteuliwa na Rais.

(2) Mtu atakayehitimu kuwa Msimamizi, lazima awe na ujuzi mkubwa wa masuala ya fedha za umma au tajriba isiyopungua ya miaka kumi katika ukaguzi na usimamizi wa fedha za umma.

(3) Msimamizi wa Bajeti, chini ya Kifungu cha 251, atahudumu kwa kipindi cha miaka nane na hataweza kuteuliwa tena.

Draft for approval

(4) Msimamizi wa Bajeti atasimamia utekelezaji wa bajeti ya kitaifa na bajeti za serikali za kaunti kwa kuagiza kutolewa kwa fedha kutoka kwa hazina za umma chini ya Kifungu cha 204, 206 na 207.

(5) Msimamizi huyu hataidhinisha kutolewa kwa fedha kutoka kwa hazina za umma mpaka aridhike kuwa utowaji huo umekubalika kisheria.

(6) Kila baada ya miezi minne, Msimamizi huyu atawasilisha kwa mabaraza yote ya Bunge ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya kitaifa na bajeti za serikali za kaunti.

**Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu**

**229.** (1) Kutakuwa na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu atakayependekezwa na Rais, kuidhinishwa na Baraza la Kitaifa na kuteuliwa na Rais.

(2) Kuhitimu kuwa Mkaguzi, mtu lazima awe na ujuzi mkubwa wa masuala ya fedha za umma au tajriba isiyopungua miaka kumi katika ukaguzi wa usimamizi wa fedha za umma.

(3) Msimamizi huyu atakuwa afisini kwa mujibu wa Kifungu cha 251, kwa kipindi cha miaka nane na hawezi tena kuteuliwa upya.

(4) Kati ya miezi sita baada ya kukamilika kwa kila mwaka wa fedha, Mkaguzi Mkuu atakagua na kutoa ripoti, kwa mujibu wa mwaka huo wa fedha, kuhusu –

(a) hesabu za serikali ya taifa na serikali za kaunti;

(b) hesabu za hazina zote na mashirika ya serikali ya kitaifa na ya serikali za kaunti;

(c) hesabu za mahakama zote;

(d) hesabu za kila Tume na Afisi huru zote zilizoundwa na Katiba hii;

(e) hesabu za Baraza la Kitaifa, Seneti na mabaraza ya kaunti;

(f) hesabu za fedha za vyama vya kisiasa zinazotoka kwenye hazina za umma.

(g) deni la umma; na

(h) hesabu za shirika lingine lolote ambalo linatakiwa kisheria kufanyiwa ukaguzi na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu.

(5) Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu anaweza kukagua na kutoa ripoti za hesabu za shirika lolote linalopokea fedha kutoka hazina za umma.

(6) Ripoti ya ukaguzi itathibitisha iwapo fedha za umma zimetumiwa kwa mujibu wa sheria au zilivyonuiwa.

(7) Ripoti za ukaguzi zitawasilishwa bungeni au kwenye mabaraza husika ya kaunti.

(8) Kati ya miezi mitatu baada ya kupokea ripoti ya ukaguzi, bunge au baraza la kaunti litazingatia na kujadili ripoti hizi na kuchukua hatua zifaazo.

Draft for approval

**Tume ya Mishahara na Kuzawidi**

**230.** (1) Tume ya mishahara na kuzawidi inajumlisha watu wafuatao walioteuliwa na Rais –

(a) Mwenyekiti

(b) Watu walioteuliwa na mashirika yafutayo, ambayo watu ambao si wanachama au waajiriwa wa mashirika hayo wameteuliwa.

(i) Tume ya Huduma za Bunge

(ii) Tume ya Huduma za Umma

(iii) Tume ya Huduma za Mahakama

(iv) Tume ya Kuwaajiri Walimu

(v) Tume ya Kitaifa ya Huduma za Polisi

(vi) Baraza la Ulinzi; na

(vii) Seneti, kwa niaba ya serikali za kaunti;

(c) Watu walioteuliwa, kila mmoja na –

(i) Shirika kuu linalowakilisha vyama vya wafanyakazi;

(ii) Shirika linalowakilisha waajiri; na

(iii) Jopo la Muungano linaloshirikisha makundi ya wataalamu yaliyokubaliwa kisheria.

(d) Watu walioteuliwa, kila mmoja na –

(i) waziri anayesimamia fedha;

(ii) Mwanasheria Mkuu; na

(e) Mtu aliye na tajriba katika usimamizi wa wafanyakazi katika huduma ya umma, aliyeteuliwa na katibu wa Waziri anayesimamia huduma ya umma.

(2) Makamishna waliotajwa katika ibara ya (1) (d) na (e) hawatakuwa na uwezo wa kupiga kura.

(3) Mamlaka na majukumu ya Tume ya Mishahara na Kuzawidi ni –

(a) Kuweka viwango na kudhibiti mishahara na marupurupu ya maafisa wote wa serikali; na

(b) Kushauri serikali ya kitaifa na serikali za kaunti kuhusu mishahara na marupurupu ya maafisa wote wa serikali.

(4) Katika kutekeleza majukumu yake, Tume hii itazingatia kanuni zifuatazo –

(a) Haja ya kuhakikisha kuwa mswada wa fidia wa umma unakuwa ni endelevu.

Draft for approval

(b) Haja ya kuhakikisha kuwa huduma ya umma ina uwezo wa kuvutia na kuweka wahudumu walio na ujuzi wanaohitajika kutekeleza majukumu yao.

(c) Haja ya kutambua uzalishaji na utendakazi; na

(d) Uwazi na haki.

**Benki Kuu ya Kenya**

**231.** (1) Benki Kuu ya Kenya imeundwa.

(2) Benki Kuu ya Kenya inawajibikia kuelekeza sera za kifedha, kudumisha udhabiti wa bei, kutoa sarafu na kutekeleza majukumu mengine kama yalivyotolewa na sheria ya Bunge.

(3) Benki Kuu ya Kenya haitakuwa chini ya mamlaka au kuelekezwa na mtu au shirika lolote inapokuwa inatumia mamlaka yake katika kutekeleza majukumu yake.

(4) Noti na sarafu zinazotolewa na Benki Kuu ya Kenya zinaweza kuwa na picha zinazoashiria Kenya au kifungu cha Kenya lakini zisiwe na picha ya mtu yeyote.

(5) Sheria ya Bunge itatoa mwongozo, wahusika, mamlaka, majukumu na utendakazi wa Benki Kuu ya Kenya.

Draft for approval

## SURA YA KUMI NA TATU

## HUDUMA ZA UMMA

### Sehemu 1- Maadili na Kanuni za Huduma za Umma

### Maadili na Kanuni za Huduma za Umma

**232.** (1) Maadili na Kanuni za Umma huhusisha–

(a) viwango vya juu vya maadili ya kitaaluma;

(b) matumizi bora ya rasilmali;

(c) utoaji wa haraka wa huduma za umma usio na upendeleo na unaozingatia usawa na haki;

(d) ushirikishwaji wa watu katika utaratibu wa kuunda Sera;

(e) uwajibikaji katika shughuli za kiusimamizi;

(f) uwazi na utoaji wa habari sahihi kwa umma bila kuchelewa;

(g) kwa kuzingatia ibara za (h) na (i), ustahili na ujuzi wa mtu ndio msingi wa kuteuliwa au kupandishwa cheo;

(h) uwakilishi wa jamii mbalimbali za Kenya; na

(i) kutoa nafasi sawa na za kutosha za kazi, katika kuteua, kutoa mafunzo na kupandishwa vyeo katika ngazi zote za huduma za umma, kwa-

(i) wanaume na wanawake;

(ii) watu wa jamii zote; na

(iii) watu wenye ulemavu.

(2) Maadili na Kanuni za Huduma za umma huhusisha huduma za umma kwa –

(a) idara zote za serikali katika viwango vyote viwili vya serikali; na

(b) mashirika yote ya serikali.

(3) Bunge litaunda sheria kukipa nguvu Kifungu hiki.

### Sehemu ya 2-Tume ya Huduma za Umma

### Tume ya Huduma za Umma

**233**. (1) Tume imeundwa ya Huduma za Umma.

(2) Tume ya Huduma za Umma inahusisha mwenyekiti, naibu wa mwenyekiti na wanachama wengine saba walioteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Baraza Kuu la

Draft for approval

Kitaifa.

(3) Kwa mujibu wa ibara ya (4), mtu hastahili kuteuliwa kama mwanachama wa Tume hii iwapo mtu huyo-

(a) kwa kipindi cha miaka mitano iliyotangulia alikuwa na afisi au amewania kiti katika uchaguzi kama-

(i) mwanachama wa bunge au wa baraza la kaunti; au

(ii) mwanachama katika bodi ya uongozi ya chama cha kisiasa;

au

(b) ana wadhifa katika afisi yoyote ya serikali;

(c) anagombea kiti, au kwa wakati wowote amewahi kugombea kiti cha ubunge au katika baraza la kaunti; au

(d) anashikilia, au kwa wakati wowote ule, amewahi kushikilia kiti cha afisi ya shirika la kisiasa linalofadhili au kuunga mkono mgombeaji wa ubunge au wa baraza la kaunti.

(4) ibara ya (3) (c) na (d) hazitatumika iwapo uchaguzi mkuu umefanywa mara mbili tangu mtu huyo alipogombea kiti au alipokuwa afisini.

(5) Kutakuwa na katibu wa Tume.

(6) Katibu wa Tume-

(i) ndiye afisa mkuu wa Tume; na

(ii) atateuliwa na Tume kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa upya mara moja tu.

Draft for approval

**Majukumu na Mamlaka ya Tume ya Huduma za Umma**

**234**. (1) Majukumu na mamlaka ya Tume ni kama yalivyofafanuliwa katika kifungu hiki .

(2) Tume-

(a) kwa mujibu wa Katiba hii na sheria-

(i) itaunda na kuvunja afisi katika huduma za umma;

(ii) itateua watu kuhudumu au kushikilia afisi pamoja na kuthibitisha uteuzi huo.

(b) itadumisha nidhamu na kuwaondoa kazini maafisa walio katika afisi hizo au wanaozishikilia kwa muda;

(c) itakuza maadili na kanuni zilizotajwa katika Vifungu vya 10 na 232 kote katika utoaji wa huduma za umma;

(d) itachunguza, kufuatilia, na kutathmini usimamizi na mienendo ya wafanyakazi katika utoaji wa huduma za umma;

(e) itahakikisha utendakazi bora katika huduma za umma;

(f) itakuza uajiri katika huduma za umma;

(g) itachunguza na kutoa mapendekezo kwa serikali ya kitaifa kuhusu hali za utendakazi, kanuni za utendakazi, na ustahili wa maafisa wanaotoa huduma za umma;

(h) itatathmini na kuripoti kwa Rais na Bunge kuhusu kiwango ambacho maadili na kanuni zilizotajwa katika Vifungu vya 10 na 232 zinazingatiwa katika huduma za umma;

(i) itasikiza na kuamua rufani kuhusu masuala yanayohusiana na huduma za umma katika serikali za kaunti;

(j) itatekeleza majukumu na mamlaka mengine yoyote kama ilivyopewa na sheria ya nchi.

(3) ibara ya (1) na (2) hazitatekelezwa katika afisi zozote zifuatazo za huduma za umma-

(a) afisi za Serikali;

(b) afisi ya Balozi wa nchi za Jumuia ya madola, balozi au mwakilishi yeyote katika afisi za kibalozi za Jamhuri;

(c) afisi au wadhifa kwa mujibu wa-

(i) Tume ya Huduma za Bunge;

(ii) Tume ya Huduma za Mahakama;

(iii) Tume ya kuwaajiri walimu; au

(iv) Tume ya Huduma za Polisi ya Kitaifa; au

(d) afisi inayohudumia serikali ya kaunti, isipokuwa ilivyofafanuliwa katika ibara ya (2) (i).

(4) Chini ya ibara ya (2), Tume haitamteua mtu kuchukua wadhifa au kushikilia afisi kama mfanyikazi katika afisi ya Rais au ya Rais mstaafu mpaka pawe na kibali kutoka kwa Rais au Rais mstaafu.

(5) Kupitia kwa maandishi, Tume inaweza, kwa masharti au bila ya masharti, kukabidhi majukumu na mamlaka yake yoyote chini ya Kifungu hiki kwa yeyote kati ya wanachama wake, au kwa afisa yeyote, bodi au idara katika huduma za umma.

**Kuajiri wafanyikazi wa serikali za kaunti**

**235.** (1) Chini ya utaratibu uliosawazishwa na kanuni zilizoidhinishwa na Sheria ya Bunge, serikali ya kaunti ina wajibu wa-

Draft for approval

(a) kuunda na kuvunja afisi katika huduma za umma;

(b) kuteua watu kuhudumu au kushikilia kwa muda afisi katika huduma za umma, kuidhinisha uteuzi ; na

(c) kudumisha nidhamu pamoja na kuwaachisha kazi watu wanaohudumu katika ofisi hizo au wanaozishikilia kwa muda.

(2) Ibara ya (1) haitazingatiwa katika afisi yoyote au wadhifa wowote unaohusu Tume ya Kuwaajiri Walimu.

**Kuwalinda wafanyikazi wa umma**

**236**. afisa wa umma hataweza–

(a) kuonewa au kubaguliwa kwa kutekeleza majukumu ya kiafisi kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyingine yoyote ; au

(b) kufutwa, kuondolewa afisini au kushushwa cheo au kuadhibiwa bila kufuata utaratibu wa sheria.

**Sehemu 3 – Tume ya Kuwaajiri Walimu**

**Tume ya Kuwaajiri Walimu**

**237**. (1) Tume ya Kuwaajiri Walimu imeundwa.

(2) Majukumu ya Tume ni –

(a) kusajili walimu waliohitimu;

(b) kuteua na kuajiri walimu waliosajiliwa;

(c) kuwapa kazi walimu walioajiriwa na Tume hii kuhudumu katika shule yoyote ya umma au taasisi;

(d) kuwapandisha vyeo na kuwahamisha walimu;

(e) kushughulikia masuala ya kinidhamu ya walimu; na

(f) kuwafuta kazi walimu.

(3) Tume -

(a) itachunguza viwango vya elimu na mafunzo kwa watu wanaojiunga na taaluma ya ualimu;

(b) itachunguza kuhitajika kwa walimu na upatikanaji wao; na

(c) itashauri serikali ya kitaifa kuhusu masuala yanayohusiana na taaluma ya ualimu.

Draft for approval

## SURA YA KUMI NA NNE

## USALAMA WA KITAIFA

### Sehemu 1- Idara za Usalama wa Kitaifa

### Kanuni za usalama wa kitaifa

**238.** (1) Usalama wa Kitaifa ni ulinzi kutokana na vitisho vya ndani na nje ya mipaka ya Kenya, watu wake, haki zao, uhuru, mali, amani, uthabiti na maendeleo na maslahi mengine ya kitaifa.

(2) Usalama wa kitaifa wa Kenya utaimarishwa na kuhakikishwa kwa mujibu wa kanuni zifuatazo –

(a) usalama wa kitaifa unaongozwa na mamlaka ya Katiba hii na Bunge;

(b) usalama wa kitaifa utatekelezwa kulingana na sheria, na kwa heshima ya utawala wa sheria, demokrasia, haki za binadamu na uhuru wa kimsingi;

(c) katika kutekeleza majukumu na mamlaka yao, idara za usalama wa kitaifa zitaheshimu uanuwai wa kitamaduni wa jamii nchini Kenya; na

(d) uajiri katika idara za usalama wa kitaifa utabainisha uanuwai wa watu wa Kenya katika viwango sawa.

### Idara za usalama wa kitaifa

**239.** (1) Idara za usalama wa kitaifa ni -

(a) Vikosi vya Ulinzi wa Kenya;

(b) Huduma za Upelelezi za kitaifa; na

(c) Huduma za Polisi za kitaifa.

(2) Lengo la kimsingi la idara za usalama wa kitaifa na utaratibu wa usalama ni kuendeleza na kuhakikisha kuwepo kwa usalama wa kitaifa kwa mujibu wa kanuni zilizotajwa katika Kifungu cha 238(2).

(3) Katika kutekeleza majukumu na mamlaka yao, idara za usalama wa kitaifa na kila mwanachama wa idara hizo hataruhusiwa -

(a) kuwa na upendeleo kwa njia yoyote,

(b) kuendeleza maslahi ya chama chochote cha kisiasa wala sera zake; au

(c) kuhujumu maslahi ya kisiasa au sera zake za kisiasa ambazo ni halali chini ya Katiba hii.

(4) Mtu hataruhusiwa kubuni kikosi cha kijeshi au kikosi chenye hadhi ya kijeshi au shirika linalodai kuendeleza na kuhakikisha usalama wa kitaifa isipokuwa inavyoruhusiwa na Katiba hii au Sheria ya Bunge.

Draft for approval

(5) Idara za uslama wa kitaifa zitakuwa chini ya mamlaka ya raia.

(6) Bunge litatunga sheria kushughulikia majukumu, utaratibu na usimamizi wa idara za usalama wa kitaifa.

**Kuundwa kwa Baraza la Usalama wa Kitaifa**

**240.** (1) Baraza la Usalama wa kitaifa limeundwa.

(2) Baraza hili linahusisha-

(a) Rais;

(b) Naibu wa Rais;

(c) Waziri anayehusika na ulinzi;

(d) Waziri anayehusika na mashauri ya kigeni;

(e) Waziri anayehusika na usalama wa taifa;

(f) Mwanasheria Mkuu

(g) Mkuu wa Majeshi ya Kenya;

(h) Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za kitaifa za Upelelezi; na

(i) Inspekta-Mkuu wa Huduma za Polisi za kitaifa.

(3) Baraza litakuwa na mamlaka ya kusimamia idara za usalama wa kitaifa na kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa sheria ya nchi.

(4) Rais atakuwa mwenyekiti wa mikutano ya baraza.

(5) Baraza litateua katibu wake.

(6) Baraza -

(a) litaunganisha sera za humu nchini, za kigeni na za kijeshi zinazohusiana na usalama wa kitaifa ili kuziwezesha idara za usalama wa kitaifa kushirikiana na kufanya kazi kikamilifu; na

(b) litatathmini na kukadiria malengo, kujitolea katika utendakazi, na hatari zozote kwa Jamhuri kuhusiana na uwezo wa usalama wa kitaifa.

(7) Baraza litatoa ripoti kwa Bunge kila mwaka kuhusiana na hali ya usalama nchini Kenya.

(8) Kupitia kwa idhini ya Bunge, Baraza linaweza –

(a) kupeleka wanajeshi wa kitaifa nje ya Kenya kwa ajili ya –

(i) kuhifadhi amani katika eneo hili au kudumisha usalama wa Kimataifa; au

Draft for approval

(ii) shughuli nyingine za kudumisha amani; na

(b) kuidhinisha kupelekwa kwa majeshi ya kigeni nchini Kenya.

**Sehemu 2 - Majeshi ya Ulinzi wa Kenya**

**Kuundwa kwa Majeshi ya Ulinzi na Baraza la Ulinzi**

**241.** (1) Majeshi ya Ulinzi wa Kenya yameundwa.

(2) Majeshi ya ulinzi yanahusisha-

(a) Jeshi la Kenya la Nchi Kavu;

(b) Jeshi la Kenya la Wanahewa; na

(c) Jeshi la Kenya la Wanamaji.

(3) Majeshi ya Ulinzi-

(a) yana wajibu wa kulinda na kutetea mamlaka na mipaka ya Jamhuri;

(b) yatasaidia na kushirikiana na idara zingine katika hali za dharura au majanga, na kutoa ripoti kwa Baraza Kuu la Kitaifa wakati wowote yanapotekeleza shughuli kama hizo; na

(c) yanaweza kupelekwa ili kurejesha amani katika sehemu yoyote ya Kenya inayokumbwa na machafuko, lakini kwa idhini ya Baraza Kuu la Kitaifa pekee.

(4) Uongozi katika Majeshi ya Ulinzi utabainisha tofauti za kimaeneo na za kijamii za watu wa Kenya.

(5) Baraza la Ulinzi limeundwa.

(6) Baraza linahusisha-

(a) Waziri anayehusika na ulinzi ambaye ni mwenyekiti;

(b)Mkuu wa majeshi ya Ulinzi ya Kenya;

(c) Makamanda watatu wa Majeshi ya Ulinzi; na

(d) Katibu Mkuu katika wizara inayohusika na ulinzi.

(7) Baraza -

(a) linahusika na sera kwa ujumla, kudhibiti na kusimamia Majeshi ya Ulinzi ya Kenya; na

(b) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa sheria ya nchi.

Draft for approval

**Sehemu 3 – Huduma za Kitaifa za Upelelezi**

**Kuundwa kwa Huduma za Upelelezi za Kitaifa**

**242.** (1) Huduma za Kitaifa za Upelelezi zimeundwa.

(2) Huduma za Kitaifa za Upelelezi-

(a) zitahusika na shughuli za kiupelelezi na zile za kuzuia upelelezi kuhusu usalama ili kuimarisha usalama wa kitaifa kwa mujibu wa Katiba hii; na

(b) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa sheria ya nchi..

**Sehemu 4 – Huduma za Polisi za Kitaifa**

**Kuundwa kwa Huduma za Polisi za Kitaifa**

**243.** (1) Huduma za Polisi za Kitaifa zimeundwa.

(2) Huduma za Polisi za Kitaifa inahusisha-

(a) Huduma za Polisi wa Kenya; na

(b) Huduma za Polisi wa Utawala.

(3) Huduma za Polisi za Kitaifa ni huduma za kitaifa ambazo zitatekeleza majukumu yake kote nchini Kenya.

(4) Bunge litatunga sheria kuidhinisha utekelezaji wa Kifungu hiki kikamilifu.

Draft for approval

**Malengo na Majukumu ya Huduma za Polisi za Kitaifa**

**244.** (1) Huduma za Polisi za Kitaifa

(a) zitajitahidi kufikia viwango vya juu vya kitaaluma na kinidhamu miongoni mwa wafanyakazi wake;

(b) zitazuia ufisadi, kukuza na kutekeleza uwazi na uwajibikaji;

(c) zitazingatia viwango vya kikatiba vya haki za binadamu na uhuru wa kimsingi;

(d) zitawapa wafanyikazi wake mafunzo hadi kufikia viwango vya juu zaidi vya kitaaluma na kimaadili kwa wafanyikazi wake, na kuheshimu haki za binadamu, uhuru wa kimsingi; na

(e) zitajenga na kukuza mahusiano na jamii pana.

**Uongozi katika Huduma za Polisi za Kitaifa**

**245.** (1) Afisi ya Inspekta-Mkuu wa Huduma za Polisi za Kitaifa imeundwa.

(2) Inspekta-Mkuu -

(a) atateuliwa na Rais kwa idhini ya Bunge; na

(b) atakuwa na mamlaka huru ya kuongoza Huduma za Polisi za Kitaifa na kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa sheria ya nchi.

(3) Huduma za Polisi na Huduma za Polisi wa Utawala, kila kimoja katika vikosi hivi kitaongozwa na Naibu Inspekta-Mkuu atakayeteuliwa na Rais kulingana na mapendekezo ya Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa.

(4) Waziri anayehusika na huduma za polisi anaweza kutoa agizo kisheria kwa Inspekta-Mkuu kuhusu suala lolote la sera kwa Huduma za Polisi za Kitaifa; lakini hakuna mtu yeyote atakayetoa agizo kwa Inspekta-Mkuu kuhusiana na –

(a) upelelezi wa kosa fulani au makosa fulani;

(b) utekelezaji wa sheria dhidi ya mtu au watu; au

(c) kuajiri, kutoa majukumu, kupandisha cheo, kusimamisha au kufuta kazi kwa mfanyakazi yeyote wa Huduma za Polisi za Kitaifa.

(5) Agizo lolote linalotolewa kwa Inspekta-Mkuu na Waziri anayehusika na huduma za polisi chini ya ibara ya (4), au agizo lolote analopewa Inspekta-Mkuu na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma chini ya kifungu cha 157(4), litakuwa kwa maandishi.

(6) Inspekta-Mkuu atahudumu katika wadhifa huo kwa kipindi kimoja cha miaka minne na hatateuliwa tena kwa kipindi kingine.

(7) Inspekta-Mkuu huweza kuondolewa mamlakani na Rais lakini kwa sababu ya –

(a) kukiuka Katiba hii au sheria nyingine yoyote, pamoja na kukiuka sura ya sita;

(b) utovu wa nidhamu ama katika utekelezaji wa majukumu ya kiafisi au vinginevyo;

(c) kutokuwa na uwezo wa kimwili au kiakili utakaomzuia kutekeleza majukumu ya afisi yake;

(d) kushindwa kutekeleza majukumu yake;

(e) kufilisika; au

(f) sababu nyingine yoyote inayoridhisha.

(8) Bunge litatunga sheria itakayoidhinisha kutekelezwa kikamilifu kwa Kifungu hiki.

Draft for approval

**Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa**

**246.** (1) Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa imeundwa.

(2) Tume inahusisha–

(a) watu wafuatao, kila mmoja wao akiwa ameteuliwa na Rais-

(i) mtu anayestahili kuteuliwa kama Jaji wa Mahakama ya Juu;

(ii) maafisa wawili wa polisi wa ngazi za juu waliostaafu; na

(iii) watu watatu wenye maadili mema ambao wamewahi kuhudumu serikalini kwa umahiri mkubwa.

(b) Inspekta-Mkuu wa Huduma za Polisi za Kitaifa.

(c) Manaibu wote wawili wa Inspekta-Mkuu wa Huduma za Polisi za Kitaifa.

(3) Tume -

(a) itaajiri na kuteua watu kuhudumu au kushikilia kwa muda afisi za huduma hiyo, kuidhinisha uteuzi na kuamua watakaopandishwa vyeo na kuhamishwa katika huduma za polisi za kitaifa.

(b) itazingatia utaratibu wa sheria, kutekeleza majukumu ya kinidhamu na kuwaondoa watu wanaohudumu au kushikilia kwa muda afisi za huduma hii; na

(c) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa sheria ya nchi..

(4) Uajiri katika Huduma za Polisi za Kitaifa utabainisha tofauti za kimaeneo na za jamii mbalimbali za watu wa Kenya.

Draft for approval

**Huduma nyingine za Polisi**

**247.** Bunge linaweza kutunga sheria zitakazounda huduma nyingine za polisi chini ya usimamizi wa Huduma za Polisi za Kitaifa na usimamizi wa Inspekta-Mkuu wa huduma hii.

## SURA YA KUMI NA TANO

## TUME NA AFISI HURU

**Utekelezezaji wa Sura**

**248.** (1) Sura hii inahusu Tume zote zilizotajwa katika ibara ya (2) na afisi huru zilizotajwa katika ibara ya (3), isipokuwa pale ambapo imetajwa vinginevyo.

(2) Tume hizo ni-

(a) Tume ya Haki za Binadamu na Usawa;

(b) Tume ya Kitaifa ya Ardhi;

(c) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka;

(d) Tume ya Huduma za Bunge;

(e) Tume ya Huduma za Mahakama;

(f) Tume ya Ugavi wa Mapato;

(g) Tume ya Huduma za umma;

(h) Tume ya Ajira na Kuzawidi;

(i) Tume ya Kuwaajiri Walimu; na

(j) Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa.

(3) Afisi huru ni –

(a) Mkaguzi – Mkuu wa Mahesabu

(b) Msimamizi wa Bajeti.

Draft for approval

**Malengo, mamlaka na ufadhili wa Tume na afisi huru**

**249**. (1) Malengo ya Tume na afisi huru ni –

(a) kulinda mamlaka ya watu;

(b) kuhakikisha kwamba idara zote za serikali zinazingatia kanuni na maadili ya kidemokrasia; na

(c ) kuendeleza mfumo wa kikatiba.

(2) Tume na wanaoshikilia nyadhifa za afisi huru –

(a) wako chini ya Katiba hii pamoja na sheria; na

(b) wako huru na hawawezi kuelekezwa au kudhibitiwa na mtu yeyote au idara.

(3) Bunge litatenga fedha za kutosha kuwezesha kila tume na afisi huru kutekeleza majukumu yake na bajeti ya kila tume na afisi huru itakuwa kando.

**Wafanyikazi, uteuzi na masharti ya kiafisi**

**250**. (1) Kila Tume itakuwa na angalau wanachama watatu, lakini wasiozidi tisa.

(2) Mwenyekiti na kila mwanachama wa tume, pamoja na anayeshikilia wadhifa wa afisi huru -

(a) watatambuliwa na kupendekezwa kwa uteuzi kwa namna ilivyoagizwa na Sheria ya nchi;

(b) wataidhinishwa na Baraza Kuu la Kitaifa; na

(c) watateuliwa na Rais.

(3) Ili kuteuliwa, mtu anastahili kutimiza vigezo vilivyowekwa na Katiba hii au Sheria ya nchi.

(4) Uteuzi wa maafisa wa tume na afisi huru utatilia maanani maadili ya kitaifa yanayorejelewa katika kifungu cha 10, na kanuni ya kwamba maafisa katika tume na afisi huru, kwa jumla, watawakilisha maeneo na jamii mbalimbali za watu wa Kenya.

(5) Mwanachama wa tume anaweza kuhudumu kwa muda.

(6) Mwanachama wa tume, au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru-

(a) Isipokuwa ni kutokana na cheo chake, atateuliwa kwa kipindi kimoja cha miaka sita na hatateul;iwa tena; na

(b) Isipokuwa ni kutokana na cheo chake au anahudumu kwa muda, hataruhusiwa kutumikia afisi nyingine au kuajiriwa ili apate faida, iwe ni kazi ya serikali au ya kibinafsi.

(7) Faida au zawadi inayolipwa kwa, au kutokana na mtu kuwa mwanachama wa tume au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru itatoka katika Mfuko wa Jumla.

(8) Faida au zawadi inayolipwa kwa, au kutokana na mtu kuwa mwanachama wa tume au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru haitabadilishwa kwa hasara ya mtu huyo wakati anapokuwa kazini.

(9) Mwanachama wa tume au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru hatawajibika kisheria kwa jambo lolote linalofanywa kwa nia njema katika kutekeleza kazi ya afisi hiyo.

(10) Wanachama wa tume watamchagua naibu-mwenyekiti kutoka miongoni mwao –

(a) katika kikao cha kwanza cha Tume; na

(b) kila inapohitajika kujaza nafasi hiyo katika afisi ya naibu-mwenyekiti

Draft for approval

(11) Mwenyekiti na naibu-mwenyekiti hawatakuwa wa jinsia moja.

(12) Kutakuwepo na katibu wa kila tume ambaye –

(a) atateuliwa na tume; na

(b) atakuwa afisa mkuu wa tume.

**Kuondolewa afisini**

**251**. (1) Mwanachama wa Tume (isipokuwa aliye mwanachama kutokana na wadhifa wake) , au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru, anaweza kuondolewa afisini kwa sababu ya-

(a) ukiukaji uliokithiri wa Katiba hii au sheria yoyote ikiwa ni pamoja na kuvunja sheria katika sura ya sita;

(b) utovu wa nidhamu ama ni katika utendakazi wa mwanachama au yule anayeshikilia wadhifa wa afisi huru;

(c) kutokuwa na uwezo wa kimwili au kiakili katika kutekeleza majukumu ya kiafisi;

(d) kushindwa kufanya kazi; au

(e) kufilisika.

(2) Mtu anayeazimia kuondolewa kwa mwanachama wa tume au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru kwa misingi yoyote iliyotajwa katika ibara ya (1) anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Baraza la Bunge huku akifafanua yale yote yanayothibitisha azma hiyo.

(3) Baraza la Bunge litachunguza malalamiko hayo na , iwapo litaridhika kwamba yana mashiko chini ya ibara ya (1), litatuma malalamiko hayo kwa Rais.

(4) Pindi tu baada ya kupokea malalamiko hayo chini ya ibara ya (3),Rais –

(a) anaweza kumsimamisha kazi mwanachama wa tume au anayeshikiia wadhifa wa afisi huru huku akisubiri matokeo ya uchunguzi wa malalamiko hayo; na

(b) atateua mahakama maalum kulingana na ibara ya (5).

(5) Mahakama hii maalum itahusisha –

(a) mtu ambaye anahudumu, au amewahi kuhudumu kama jaji wa mahakama yenye mamlaka makuu, ambaye pia atakuwa mwenyekiti;

(b) angalau watu wawili ambao wanastahili kuteuliwa kama majaji wa Mahakama ya Juu; na

(c) mwanachama mwingine mmoja ambaye ana uwezo wa kuchunguza ushahidi kuhusiana na msingi mahususi wa kumtaka afisa huyo aondolewe.

(6) Mahakama maluum itachunguza suala hilo kwa haraka, na kutoa ripoti ya matokeo na mapendekezo yenye mashiko kwa Rais, ambaye atachukua hatua kulingana na mapendekezo hayo katika kipindi cha siku thelathini.

Draft for approval

(7) Mtu atakayesimamishwa kazi chini ya Kifungu hiki ana haki ya kuendelea kupokea nusu ya zawadi na faida ya afisi akiwa amesimamishwa kazi.

**Majukumu na Mamlaka ya jumla**

**252**. (1) Kila tume, na anayeshikilia wadhifa wa afisi huru –

(a) anaweza kuchukua hatua ya kufanya uchunguzi au kufuatia malalamiko yaliyotolewa na mwananchi;

(b) ana mamlaka muhimu ya kupatanisha , kusuluhisha na kujadiliana ili kupata maafikiano;

(c) itaajiri wafanyakazi wake; na

(d) inaweza kutekeleza majukumu na mamlaka mengine yoyote iliyopewa na sheria, mbali na majukumu na mamlaka iliyopewa na Katiba hii.

(2) Malalamiko kwa Tume au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru yanaweza kuwasilishwa na mtu yeyote mwenye kibali cha kuendeleza mashtaka chini ya kifungu cha 22 (1) na (2) .

(3) Tume na afisi huru zifuatazo zina mamlaka ya kumwita shahidi kutoa usaidizi kwa madhumuni ya kufanya uchunguzi wao-

(a) Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya;

(b) Tume ya Huduma za Mahakama;

(c) Tume ya Kitaifa ya Ardhi;

(d) Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu.

Draft for approval

**Ushirikishwaji wa tume na afisi huru**

**253**. Kila tume na afisi huru-

(a) ni asasi shirikishi iliyo na msururu wa urithi na muhuri wake; na

(b) inaweza kushtaki na kushtakiwa katika jina lake la kiushirika.

**Kuripoti kwa tume na afisi huru**

**254.** (1) Mwishoni mwa kila mwaka wa makadirio ya fedha, kila tume na anayeshikilia wadhifa wa afisi huru, watawasilisha ripoti kwa Rais na Bunge, haraka iwezekanavyo.

(2) Wakati wowote, Rais, Baraza la Kitaifa au Seneti wanaweza kuitaka tume au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru kuhusu suala lolote kuwasilisha ripoti kuhusu suala mahususi.

(3) Kila ripoti itakayohitajika kutoka kwa tume au anayeshikilia wadhifa wa afisi huru chini ya Kifungu hiki, itachapishwa na kutangazwa.

Draft for approval

## SURA YA KUMI NA SITA

## MAREKEBISHO YA KATIBA HII

**Marekebisho ya Katiba hii**

**255.** (1) Pendekezo la marekebisho ya Katiba hii litatekelezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 256 au 257, na kupitishwa kwa mujibu wa ibara ya (2) kwenye kura ya maamuzi, iwapo marekebisho hayo yanahusu suala lolote kati ya masuala yafuatayo-

(a) mamlaka makuu ya Katiba;

(b) mipaka ya Kenya;

(c) mamlaka ya watu;

(d) maadili ya kitaifa, kanuni za kiutawala zilizoorodheshwa katika Kifungu cha 10 (2) (a) hadi (d);

(e) Sheria ya Haki;

(f) kipindi cha kuhudumu cha Rais;

(g) uhuru wa Idara ya Mahakama, Tume, na afisi huru zinazorejelewa katika Sura ya Kumi na tano;

(h) majukumu ya Bunge;

(i) malengo, kanuni na muundo wa serikali ya ugatuzi; au

(j) masharti ya Sura hii,

(2) Pendekezo la marekebisho litapitishwa kwa kura ya maamuzi chini ya ibara ya (1) iwapo-

(a) angalau asilimia ishirini ya wapiga kura waliosajiliwa katika angalau nusu ya idadi ya kaunti itapiga kura katika kura ya maamuzi; na

(b) marekebisho yanaungwa mkono na wananchi wengi wanaopiga kura katika kura ya maamuzi.

(3) marekebisho katika Katiba hii ambayo hayahusiani na yale yaliyofafanuliwa katika ibara ya (1) yataidhinishwa ama –

(a) na Bunge, kulingana na Kifungu cha 256; au

(b) na watu pamoja na Bunge, kulingana na Kifungu cha 257.

**Marekebisho yanayotokana na juhudi za Bunge**

**256.** (1) Mswada wa kurekebisha Katiba hii –

(a) unaweza kuwasilishwa katika mojawapo ya viwango vya Bunge;

Draft for approval

(b) haupaswi kuangazia suala lolote jingine isipokuwa yale yanayotokana na marekebisho ya sheria katika Mswada huo;

(c ) hautafikishwa kusomwa kwa mara ya pili katika mojawapo ya vitengo vya Bunge, katika muda wa siku tisini baada ya kusomwa kwa Mswada kwa mara ya kwanza katika Bunge hilo; na

(d) utakuwa umepitishwa na Bunge wakati kila mojawapo ya vitengo vya Bunge kimepitisha Mswada huo katika kusomwa kwa mara ya pili na tatu, kwa idadi isiyopungua thuluthi mbili ya wabunge wote katika ngazi hiyo.

(2) Bunge litatangaza Mswada wowote wa kurekebisha Katiba hii, na kuandaa mjadala wa umma kuhusiana na Mswada huo.

(3) Baada ya Bunge kupitisha Mswada wa kurekebisha Katiba hii, Maspika wa viwango vyote viwili vya Bunge watawasilisha kwa pamoja kwa Rais –

(a) Mswada, kutiwa saini na kuchapishwa; na

(b) cheti kwamba Mswada huo umepitishwa na Bunge kwa mujibu wa Kifungu hiki.

(4) Kulingana na ibara ya (5), Rais atautia sahihi Mswada huo na kuufanya uchapishwe katika muda wa siku thelathini baada ya Mswada huo kuidhinishwa na Bunge.

(5) Iwapo Mswada wa kurekebisha Katiba hii unapendekeza marekebisho yanayotajwa katika katika Kifungu cha 255 (1), –

(a) kabla ya Rais kuutia sahihi Mswada huo, ataiomba Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kufanya kura ya maamuzi ya kitaifa katika muda wa siku tisini ili kuidhinisha Mswada huo; na

(b) katika muda wa siku thelathini baada ya mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na Mipaka kumthibitishia Rais kwamba Mswada huo umepitishwa kulingana na Kifungu cha 255 (2), Rais atautia sahihi Mswada huo na kuufanya uchapishwe.

Draft for approval

**Marekebisho yanayotokana na juhudi za wengi**

**257.** (1) Marekebisho ya Katiba hii yanaweza kupendekezwa kutokana na juhudi za wengi ikiwa angalau watu milioni moja waliojiandikisha kupiga kura wametia sahihi.

(2) Juhudi za wengi za marekebisho ya Katiba hii zinaweza kuchukua muundo wa pendekezo la jumla au kupitia kwa rasimu ya Mswada iliyotayarishwa.

(3) Iwapo juhudi za wengi zitahusisha kupitia kwa njia ya pendekezo la jumla, wanaoendeleza pendekezo hili watalitayarisha liwe kama rasimu ya Mswada kupitia kwa wadhamini wao.

(4) Wadhamini wanaoendeleza juhudi za wengi watawasilisha rasimu ya Mswada pamoja na sahihi walizokusanya kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ambayo itathibitisha kwamba pendekezo hilo linaungwa mkono na angalau na wapiga kura milioni moja waliosajiliwa.

(5) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itakaporidhika kwamba pendekezo hilo limetimiza masharti ya Kifungu hiki, Tume hii itawasilisha pendekezo hilo kwa kila baraza la kaunti ili kujadiliwa katika muda wa miezi mitatu baada ya tarehe ya kuwasilishwa na Tume hiyo.

(6) Iwapo baraza la kaunti litaidhinisha rasimu ya Mswada katika kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ilipowasilishwa na Tume, Spika wa baraza la kaunti atawasilisha nakala ya rasimu ya Mswada kwa Maspika wawili wa viwango vyote viwili vya Bunge, pamoja na cheti kwamba baraza la kaunti limeidhinisha.

(7) Iwapo rasimu ya Mswada imeidhinishwa na mabaraza mengi ya kaunti, rasimu hiyo itawasilishwa Bungeni bila kuchelewa.

(8) Chini ya kifungu hiki, Mswada utaidhinishwa na Bunge iwapo utaungwa mkono na wabunge wengi katika kila kiwango cha Bunge.

(9) Iwapo Bunge litaupitisha Mswada huo, utapelekewa Rais kutiwa sahihi kulingana na Kifungu cha 256 (4) na (5).

(10) Iwapo kila ngazi ya Bunge haitapitisha Mswada, au Mswada huo unahusu suala lililotajwa katika kifungu cha 255 (1), Mswada huo uliopendekezwa utapalekwa kwa watu kwa kura ya maamuzi

(11) Kifungu cha 255 (2) kitatumika, kukiwemo na marekebisho muhimu yoyote, katika kura ya maamuzi chini ya ibara ya (10).

Draft for approval

## SURA YA KUMI NA SABA

## MASHARTI YA JUMLA

**Utekelezaji wa Katiba hii**

**258.** (1) Kila mtu ana haki ya kuwasilisha kesi mahakamani, akidai kuwa Katiba hii imekiukwa , au inatishiwa na kukiukwa.

(2) Pamoja na mtu anayefanya hivyo kwa maslahi yake mwenyewe kesi inaweza kuwasilishwa mahakamani na- kulingana na ibara ya (1)-

(a) mtu anayewasilisha kwa niaba ya mwingine ambaye hawezi kufanya hivyo yeye binafsi;

(b ) mtu anayewasilisha kama mwanachama wa, au kwa maslahi ya, kundi au makundi ya watu;

(c) mtu anayewasilisha kwa niaba ya maslahi ya umma; au

(d) chama kinachowasilisha kwa maslahi ya mmoja au zaidi ya wanachama wake.

**Kufasiri Katiba hii**

**259**. (1) Katiba hii itafasiriwa kwa namna ambayo –

(a) inakuza malengo, maadili na kanuni zake;

(b) inaendeleza utawala wa sheria, haki za binadamu na uhuru wa kimsingi ulioko katika Sheria ya Haki;

(c) inaruhusu maendeleo ya sheria; na

(d) inachangia utawala bora.

(2) Iwapo kuna mkinzano kati ya matoleo ya lugha tofauti ya Katiba hii, toleo la lugha ya Kiingereza ndilo litakalotawala.

(3) kila sharti la Katiba hii litafasiriwa kulingana na kanuni za ufasiri kwamba sheria kila mara inazungumza, na hivyo basi, miongoni mwa vitu vingine –

(a) jukumu la mamlaka lililotolewa na Katiba hii kwa afisi linaweza kufanywa au kutekelezwa na mtu anayeshikilia wadhifa katika afisi hiyo kama inavyohitajika;

(b) rejeleo lolote katika Katiba hii kwa serikali au kwa afisi nyingine ya umma au afisa, au mtu anayeshilikia afisi hiyo ni rejeleo kwa mtu anayeshikilia afisi hiyo kwa muda au anayetekeleza majukumu ya afisi hiyo wakati wowote ule;

(c) rejeleo katika Katiba hii kwa afisi, idara ya serikali au mahali palipotajwa kwenye Katiba hii litasomwa pamoja na badiliko lolote rasmi linalohitajika ili likubalike katika mazingira hayo; na

(d) rejeleo katika Katiba hii kwa afisi, kundi au shirika, ikiwa ni afisi, na iwapo kundi au shirika halipo tena, basi yule aliyerithi ndiye atakayerejelewa au yeyote husika

Draft for approval

katika afisi, kundi au shirika.

(4) Katika Katiba hii, isipokuwa pale ambapo muktadha unahitaji vinginevyo-

(a) iwapo neno au maelezo yamefafanuliwa katika Katiba hii, tofauti zozote za kisarufi au matumizi ya neno linalohusiana na jingine, soma ukizingatia mabadiliko yanayotokana na muktadha; na

(b) neno "-kiwemo" linamaanisha "ikiwemo, lakini bila mpaka";

(5) Katika kuhesabu wakati baina ya matukio mawili kwa shughuli yoyote katika Katiba hii, kama wakati umeelezwa-

(a) kama siku, basi siku ambayo tukio la kwanza linatokea haitazingatiwa, na siku ambayo tukio la mwisho linaweza kutokea itahusishwa;

(b) kama miezi, kipindi cha muda uliowekwa huisha mwanzoni mwa siku katika mwezi husika-

(i) ambao una nambari sawa kama tarehe ambapo kipindi hicho kilianza, iwapo mwezi huo una tarehe inayolingana; au

(ii) hiyo ndiyo siku ya mwisho ya mwezi huo; au

(c) kama miaka, kipindi cha muda huo kinamalizika mwanzoni mwa tarehe ya mwaka husika inayolingana na tarehe ambayo kipindi hicho kilianza.

(6) Iwapo muda uliotengwa katika Katiba hii kwa lengo lolote ni siku sita au chini yake, Jumapili na siku za mapumziko hazitahesabiwa wakati wa kuhesabu muda.

(7) Iwapo, katika hali yoyote maalumu, kipindi cha muda kilichoelezwa na Katiba hii kinakamilika Jumapili au siku ya mapumziko, muda huo unaongezwa hadi siku inayofuata ambayo siyo Jumapili au siku ya mapumziko.

(8) Iwapo muda fulani haukuelezwa na Katiba hii ili kuekeleza kitendo fulani, kitendo hicho kitafanywa bila kuchelewa na kulingana na wakati wowote shughuli hiyo inapohitajika.

(9) Iwapo mtu yeyote au idara ya Serikali ina mamlaka chini ya Katiba hii kuongeza kipindi cha muda unaoruhusiwa katika Katiba hii, mamlaka hayo yanaweza kutekelezwa kabla au baada ya mwisho wa kipindi hicho isipokuwa pale ambapo nia tofauti imeelezwa wazi katika sharti linalotoa mamlaka hayo.

(10) Isipokuwa pale ambapo Katiba hii inaeleza tofauti, ikiwa mtu ameondoka katika afisi iliyoundwa na Katiba hii, iwapo mtu huyo anastahili kutokana na umahiri wake kazini, anaweza kuteuliwa tena, kuchaguliwa kwa kupigiwa kura au vinginevyo kuchaguliwa tu kuchukua afisi hiyo kulingana na Katiba hii.

(11) Ikiwa jukumu au mamlaka yaliyopewa mtu chini ya Katiba hii hutekelezwa na mtu huyo tu kupitia kwa ushauri au pendekezo, kupitia kwa kuidhinisha au kukubali kwa, au kupitia kwa mashauriano na mtu mwingine, jukumu linaweza kufanywa ama mamlaka kutekelezwa kupitia tu kwa ushauri huo, pendekezo, kwa kuidhinisha au kukubali huko, au baada ya mashauriano hayo, isipokuwa pale ambapo Katiba hii inaeleza vinginevyo.

Draft for approval

**Ufasiri**

**260**. Isipokuwa pale ambapo muktadha unahitaji vinginevyo, katika Katiba hii–

"mtu mzima" inamaanisha mtu ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na minane;

"kitendo sawazishi" huhusisha hatua yoyote inayolenga kuondolea mbali ukosefu wa usawa au kumnyima mtu au kuingilia uhuru wake wa kimsingi;

"mtoto" inamaanisha mtu ambaye hajatimiza umri wa miaka kumi na minane;

"kukiuka" inahusisha kukosa kufanya inavyostahili;

"sheria ya kaunti" inamaanisha sheria iliyotungwa na serikali ya kaunti au chini ya mamlaka yaliyopewa baraza la kaunti;

"ulemavu" inahusisha ulemavu wowote wa kimwili, kihisia, kiakili, kisaikolojia au ulemavu wa aina nyingine, hali au ugonjwa ambao, au unaochukuliwa na sekta mahususi za kijamii kuwa na athari za muda mrefu kwa mtu kuweza kutekeleza majukumu yake ya kawaida ya kila siku;

"stakabadhi" inahusisha-

(a) chapisho lolote au suala lolote lililoandikwa, kuelezwa au kuandikwa juu ya kitu kwa kutumia herufi, michoro au alama au zaidi ya mojawapo ya njia hizo ambayo inadhamiriwa kutumiwa au inaweza kutumiwa kwa ajili ya kurekodi suala hilo; na

(b) majalada ya kielektroniki;

"tarehe ya kutekelezwa" inamaanisha tarehe ambayo Katiba hii ilianza kutumika;

" kushindwa" inahusisha kukataa;

"mwaka wa fedha" inamaanisha kipindi cha miezi kumi na miwili kinachomalizika katika siku ya thelathini ya mwezi wa Juni au siku nyingine iliyoelezwa na sheria ya kitaifa, lakini mwaka wa mwanzo wa fedha wa asasi yoyote ni kipindi cha wakati tangu ilipoanza mpaka mara tu kufikia siku ya thelathini ya Juni, au siku yoyote ile itakayoelezwa na sheria ya kitaifa;

*"Gazeti*" inamaanisha *Gazeti Rasmi la Serikali* linalochapishwa kutokana na kibali cha serikali ya kitaifa, au gazeti jingine linalochapishwa pamoja na *Gazeti rasmi la Kenya;*

*"*dhamana" inamaanisha ahadi kamili au ahadi yenye masharti, kujitolea kwa serikali ya kitaifa kulipa nusu au kulipa kabisa mkopo wowote wa serikali ya kaunti au wa mtu yeyote;

"afisa wa mahakama" inamaanisha msajili, naibu wa msajili, hakimu, Kadhi au afisa msimamizi wa mahakama yaliyoundwa chini ya Kifungu cha 169 (1)(d);

"ardhi" inahusisha

(a) eneo juu ya ardhi au chini ya mwamba;

Draft for approval

(b) eneo lolote la maji au chini ya ardhi;

(c ) maji ya bahari katika eneo la bahari kwenye mipaka ya nchi na la kiuchumi;

(d) maliasili zilizopo juu au chini ya ardhi; na

(e) eneo la anga juu ya ardhi;

"utungaji sheria" unahusisha-

(a) Sheria ya Bunge, au sheria iliyotungwa chini ya mamlaka yaliyotolewa na sheria ya Bunge; au

(b) sheria iliyotungwa na baraza la serikali ya kaunti, au chini ya mamlaka yaliyotolewa na sheria kama hiyo;

" mkopo" unajumlisha njia yoyote ya kukopa, kukopesha au malipo ya baadaye ambapo pesa kutoka kwa mfuko wa umma zinaweza kutumiwa, au zinahitaji kutumiwa ili kulipa au kulipia tena;

"jamii iliyotengwa" inamaanisha–

(a) jamii ambayo kutokana na idadi ndogo ya watu wake, au kwa sababu nyingineyo, imeshindwa kushiriki kikamilifu katika ujumla wa shughuli za maisha ya kijamii na kiuchumi ya Kenya;

(b) jamii ya kitamaduni, ambayo kutokana na hamu ya kuhifadhi utamaduni wake wa kipekee na utambulisho wake ili usimezwe, imebakia nje ya ujumla wa maisha ya kijamii na kiuchumi ya Kenya;

(c) jamii asilia ambayo imebakia kudumisha maisha na mitindo ya kitamaduni inayojikita kwenye uchumi wa shughuli za usasi na ukusanyaji; au

(d) wafugaji au jamii za ufugaji , ikiwa ni –

(i) wa kuhamahama; au

(ii) jamii zinazoishi mahala pamoja ambazo, kwa sababu ya kutengwa kijiografia, hazijashirikishwa kikamilifu katika shughuli za kijumla za kijamii na kiuchumi za Kenya.

"kundi lililotengwa" inamaanisha kundi la watu ambalo, kutokana na sheria au mazoea kabla, wakati wa, au baada ya tarehe ya utekelezaji wa Katiba hii, walikuwa wamebaguliwa katika mojawapo au zaidi ya misingi inayotajwa katika Kifungu cha 27 (4);

" sheria ya kitaifa" inamaanisha sheria ya Bunge, au sheria inayotungwa chini ya mamlaka ya Sheria ya Bunge;

"maliasili" inamaanisha vitu au hali za kimaumbile zisizo za kibinadamu ambazo zinaweza kutumiwa tena au zisitumiwe, pamoja na-

(a) mwanga wa jua;

Draft for approval

(b) maji kwenye ardhi na chini ya ardhi;

(c) misitu, uanuwai wa kiasili na kinasaba, na

(d) miamba, madini, malighafi ya mafuta na vianzo vingine vya kawi;

"mzee katika jamii" inamaanisha mtu ambaye amefikisha umri wa miaka sitini;

"mtu" inahusisha kampuni, chama au kundi la watu , liwe la shirika au lisilo la shirika;

"chama cha kisiasa" inamaanisha muungano wa watu uliobuniwa kwa madhumuni ambayo yametajwa katika sehemu ya 3 ya sura ya saba;

"mali" inahusisha nia au haki ya , au inayotokana na –

(a) ardhi  au vitu vya kudumu kwenye ardhi, au kustawisha ardhi

(b) bidhaa au mali ya kibinafsi;

(c) hakimiliki au

(d) fedha au vifaa.

"afisa wa umma" inamaanisha

(a) afisa yeyote wa serikali; au

(b) mtu yeyote mbali na afisa wa serikali anayeshikilia afisi ya umma

"afisi ya umma" inamaanisha afisi katika serikali ya kitaifa, serikali ya kaunti au katika huduma za umma, iwapo zawadi na faida za afisi hulipwa kutoka katika Mfuko wa Jumla au moja kwa moja kutoka kwa pesa zinazotolewa na Bunge.

"huduma ya umma" inamaanisha watu wote kwa pamoja, mbali na maafisa wa serikali, wanaofanya kazi katika idara ya Serikali;

"jamhuri" inamaanisha Jamhuri ya Kenya;

"serikali" inapotumiwa kama nomino, ina maana ya  mseto wa afisa, idara na asasi zingine zinazounda serikali ya Jamhuri chini ya Katiba hii;

"afisi ya serikali" inamaanisha yoyote katika hizi –

(a) Rais;

(b) Naibu wa Rais;

(c) Waziri;

(d) Mbunge;

(e) Majaji na Mahakimu;

(f) Mwanachama wa Tume chini ya Sura ya Kumi na tano;

Draft for approval

(g) Anayeshikilia wadhifa wa afisi huru chini ya Sura ya Kumi na tano;

(h) Mwanachama wa baraza la kaunti, gavana au naibu wa gavana wa kaunti, au mwanachama yeyote wa mamlaka kuu ya kaunti;

(i) Mwanasheria Mkuu;

(j) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma;

(k) Katibu wa Baraza la Mawaziri;

(l) Katibu Mkuu;

(m) Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi;

(n) Kamanda wa huduma ya Majeshi ya Ulinzi ya Kenya;

(o) Mkurugenzi-Mkuu wa Huduma za Kitaifa za Upelelezi;

(p) Inspekta-Mkuu, na Naibu wa Inspekta-Mkuu, wa Huduma za Polisi za Kitaifa; au

(q) afisi ambayo imeundwa na kuchukuliwa kama afisi ya serikali chini ya sheria ya kitaifa;

"afisa wa serikali" inamaanisha mtu anayeshikilia afisi ya Kitaifa;

"idara ya Serikali" inamaanisha Tume, afisi, shirika au asasi nyingine iliyoundwa chini ya Katiba hii;

"Maandishi" inahusisha upigaji chapa, upigaji picha, lithografia, upigaji taipu, breli na njia yoyote nyingine inayowakilisha au kuzalisha maneno kwa njia inayoonekana; na

"vijana" inamaanisha ujumla wa watu wote katika Jamhuri ambao –

(a) wametimiza umri wa miaka kumi na minane; lakini

(b) hawajatimiza umri wa miaka thelathini na mitano.

Draft for approval

## SURA YA KUMI NA NANE

## MASHARTI YA MPITO NA MATOKEO

**Sheria zinazohusiana na Matokeo**

**261.** (1) Bunge litatunga sheria yoyote inayohitajiwa na Katiba hii, itungwe ili kushughulikia jambo fulani katika muda ulioelezwa katika Mpangilio wa Tano, kuanzia tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii.

(2) Licha ya ibara ya (1), Baraza Kuu la Kitaifa linaweza, kupitia kwa uamuzi utakaoungwa mkono na idadi ya kura isiyopungua thuluthi mbili ya Wabunge wote, Baraza Kuu la Kitaifa linaweza kuongeza muda uliowekwa kuhusiana na suala lolote kama inavyoelezwa katika ibara ya (1), kwa muda usiozidi mwaka mmoja.

( 3) Uwezo wa Baraza la Kitaifa kama ulivyoelezwa katika ibara ya (2) unaweza kutumika-

(a) Mara moja tu kuhusiana na suala fulani; na

(b) Katika hali maalum ambayo itaidhinishwa na Spika wa Baraza la Kitaifa.

(4) Kwa sababu ya ibara ya (1), Mwanasheria Mkuu akishauriana na Tume ya Utekelezaji wa Katiba hii, atatayarisha na kuwasilisha Miswada Bungeni, kwa haraka inavyowezekana, ili kuwezesha Bunge kupitisha sheria katika muda uliowekwa.

(5) Kama Bunge litashindwa kupitisha sheria yoyote kwa kipindi kilichowekwa, mtu yeyote anaweza kupeleka malalamiko kwa Mahakama ya Juu kuhusiana na jambo hilo.

(6) Katika kuamua juu ya malalamiko hayo chini ya ibara ya (5) , Mahakama ya Juu inaweza-

(a) Kutoa agizo kuhusu jambo hilo; na

(b) Kuelekeza agizo hilo kwa Bunge na Mwanasheria Mkuu ili kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba sheria inayohitajika imepitishwa katika muda uliowekwa katika agizo hilo, na kutoa ripoti kuhusu utekelezaji huo kwa Jaji Mkuu.

(7) Iwapo Bunge litashindwa kuunda sheria kulingana na agizo chini ya ibara ya (6) (b), Mwanasheria Mkuu atamshauri Rais kuvunja Bunge na Rais atalivunja Bunge.

(8) Iwapo Bunge limevunjwa chini ya ibara ya (7), Bunge jipya litaunda sheria hiyo inayohitajika katika muda uliolezwa katika Mpangilio wa Tano, kuanzia tarehe ya kuanza kwa kipindi cha Bunge jipya.

(9) Ikiwa Bunge jipya litashindwa kuunda sheria kulingana na ibara ya (8), masharti ya ibara ya (1) hadi ya (8) yatatekelezwa upya.

Draft for approval

**Masharti ya Mpito na matokeo**

**262.** Masharti ya mpito na matokeo yanayoelezwa katika Mpangilio wa Sita yataanzwa kutekelezwa siku ya kuanza kutekeleza Katiba hii.

**Tarehe ya Kutekelezwa kwa Katiba**

**263.** Katiba hii itaanza kutumika Rais atakapotangaza rasmi au baada ya muda wa siku kumi na nne tokea tarehe ya kuchapisha matokeo ya mwisho ya kura ya maamuzi kuidhinisha Katiba hii katika Gazeti rasmi la serikali, yoyote itakayokuja mwanzo kati ya hatua hizo mbili.

**Kubatilishwa kwa Katiba ya awali**

**264.** Kwa mujibu wa Mpangilio wa sita, ili kuondoa shaka, Katiba inayotumika kabla ya tarehe ya kuidhinisha Katiba hii, itabatilishwa kwenye tarehe hiyo.

Draft for approval

**MPANGILIO WA KWANZA**

**Kifungu cha 6(1))**

**KAUNTI**

1. Mombasa

2. Kwale

3. Kilifi

4. Tana River

5. Lamu

6. Taita /Taveta

7. Garissa

8. Wajir

9. Mandera

10.Marsabit

11. Isiolo

12. Meru

13. Tharaka-Nithi

14. Embu

15. Kitui

16. Machakos

17. Makueni

18. Nyandarua

19. Nyeri

20. Kirinyaga

21.Murang'a

22.Kiambu

23. Turkana

24. West Pokot

25. Samburu

Draft for approval

26. Trans Nzoia
27. Uasin Gishu
28. Elgeyo/Marakwet
29. Nandi
30. Baringo
31. Laikipia
32. Nakuru
33. Narok
34. Kajiado
35. Kericho
36. Bomet
37. Kakamega
38. Vihiga
39. Bungoma
40. Busia
41. Siaya
42. Kisumu
43. Homa Bay
44. Migori
45. Kisii
46. Nyamira
47. Nairobi City


Draft for approval

**MPANGILIO WA PILI**

**(Kifungu cha (9) (2))**

**NEMBO ZA KITAIFA**

(a) Bendera ya Taifa




*Tanbihi:* Vipimo vyote vilivyotolewa haviwakilishi urefu au upana wowote na hivyo vinawiana tu.

**Maelezo**:

Mistari mitatu mikubwa yenye upana sawa yenye rangi nyeusi, nyekundu, na kijani kutoka juu hadi chini na kutenganishwa na mistari myembamba myeupe, yenye ngao linganifu na mishale myeupe iliyowekwa juu katikati ya bendera.

(b) Wimbo wa Taifa

**1**

Ee Mungu nguvu yetu

Ilete baraka kwetu.

Haki iwe ngao na mlinzi

Na tukae na undugu

Amani na uhuru

Raha tupate na ustawi.

**2**

Amkeni ndugu zetu

Tufanye sote bidii.

Nasi tujitoe kwa nguvu,

Nchi yetu ya Kenya,

Tunayoipenda,

Tuwe tayari kuilinda.

**3**

Na tujenge taifa letu

Ee, ndio wajibu wetu,

Kenya istahili heshima

Tuungane mikono

Pamoja kazini

Kila siku tuwe na shukrani.


Draft for approval

(c) Ngao ya Serikali




Draft for ap al

(d) Muhuri wa Serikali



**MPANGILIO WA TATU**

**(Vifungu vya 74, 141 (3) 148 (5) na 152 (4) )**

**VIAPO VYA KITAIFA NA UTHIBITISHO**

**KIAPO AMA KUKUBALI KUWA NA UAMINIFU KWA RAIS WA TAIFA /KAIMU RAIS NA NAIBU RAIS**

Mimi, ……………. , nikifahamu kuwa jukumu muhimu ninalochukua kama Rais / Naibu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya, naapa /nakiri kwa dhati kuwa nitakuwa mwaminifu kwa Jamjuri ya Kenya; kwamba nitafuata, kuhifadhi, kutetea, Katiba ya Kenya, kulingana na sheria iliyowekwa, na sheria nyingie zote za Jamhuri, na kwamba nitalinda na kutetea uhuru, uadilifu na heshima ya watu wa Kenya. ( Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie)

**KIAPO AMA KUKUBALI KWA DHATI MAMLAKA YA AFISI YA RAIS/KAIMU WA RAIS**

Mimi, ……………… , naapa/nakubali kwa dhati kuwa nitawatumikia watu wote wa Jamhuri ya Kenya kwa bidii katika afisi ya Rais/ Kaimu Rais wa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza majukumu na wajibu wangu kwa uaminifu katika afisi ya Rais /Kaimu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya; na nitatenda haki kwa wote kulingana na Katiba hii, na kupitia kwa sheria zilizowekwa bila woga, upendeleo, upendo au chuki. (Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie)

**KIAPO AMA KUKUBALI KWA DHATI MAMLAKA YA AFISI YA NAIBU WA RAIS**

Mimi, ……………… , naapa ya kwamba/nakubali kwa dhati kwamba kila wakati Naibu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza wajibu wangu kwa bidii na kutekeleza kazi zangu katika afisi hiyo kwa uwezo wangu wote; na kwamba kwa wakati wowote ule nitakaohitajika, kumshauri Rais wa Jamhuri ya Kenya kwa uaminifu na ukweli; kwamba nitatenda haki kwa wote bila woga, upendeleo, upendo au chuki; na kwamba sitatoa siri zozote zitakazonifikia katika shughuli zangu za kazi ama moja kwa moja au kupitia kwa yeyote. (Kama ni kiapo: Ee Mungu nisaidie)

**KIAPO AMA KUKUBALI KWA DHATI MAMLAKA YA AFISI YA WAZIRI**

Mimi.................................., ninayeteuliwa kuwa Waziri wa Kenya, ninaapa ya kwamba/ninakubali kwa dhati kwamba nitakuwa mwaminifu wakati wowote kwa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitaitii, nitaiheshimu na kuitetea Katiba hii ya Kenya na sheria nyingine zote za Jamhuri; kwamba nitawahudumia vyema na kwa uaminifu watu na Jamhuri ya Kenya katika Afisi ya Waziri; kwamba nitaitumikia afisi yangu kama Waziri kwa heshima na hadhi; kwamba nitakuwa mshauri wa kweli

Draft for approval

na mwaminifu kwa Rais au kwa usimamizi mwema wa masuala ya umma katika Jamhuri ya Kenya; kwamba sitatoa siri zozote zitakazonifikia katika shughuli zangu za kazi ama moja kwa moja au kupitia kwa yeyote isipokuwa pale inapohitajika katika utekelezaji wa kazi zangu za uwaziri; na kwamba nitatekeleza majukumu ya afisi yangu kwa uangalifu na kwa uwezo wangu. ( Kama ni kiapo –Ee Mungu nisaidie)

**KIAPO AMA KUKUBALI KWA DHATI MAMLAKA YA AFISI YA KATIBU WA BARAZA LA MAWAZIRI/KATIBU MKUU**

Mimi, ……………………, nikiwa ninahitajika kuchukua wajibu wa katibu wa Baraza la Mawaziri/ Katibu Mkuu ninaapa ya kwamba/ninakubali kwa dhati kwamba, isipokuwa kwa idhini ya Rais, sitafichua habari za shughuli yoyote, taratibu au nyaraka za Baraza la Mawaziri ninazohitaji kuzihifadhi kwa siri, kwa njia ya moja kwa moja au kupitia kwa yeyote, isipokuwa pale ambapo zinahitajika kutokana na shughuli zangu za kazi kama Katibu wa Baraza la Mawaziri/Katibu Mkuu. (Kama ni kiapo:-Ee Mungu nisaidie)

**VIAPO KWA JAJI MKUU/RAIS WA MAHAKAMA KUU, MAJAJI WA MAHAKAMA KUU, MAJAJI WA MAHAKAMA YA RUFANI NA MAJAJI WA MAHAKAMA YA JUU**

Mimi, ……………………, (Jaji Mkuu /Rais wa Mahakama Kuu, jaji wa Mahakama Kuu, jaji wa Mahakama ya Rufani, jaji wa Mahakama ya Juu) nina (apa kwa jina la Mwenyezi Mungu)/( nakubali kwa dhati) kutumikia watu wa Jamhuri ya Kenya na kutekeleza haki bila mapendeleo kulingana na Katiba hii na kwa sheria zilizowekwa, na sheria na desturi za Jamhuri, bila woga wowote, upendeleo, ubaguzi, upendo, chuki, ama athari ya kisiasa, kidini, ama ushawishi wowote. Katika kutekeleza majukumu ya kisheria ambayo nimepewa, kwa uwezo wangu wote, na kwa wakati wangu wote, nitalinda, nitasimamia, na kutetea Katiba hii kwa ajili ya kulinda hadhi na heshima ya mahakama na mfumo wa mahakama za Kenya na kukuza haki, uhuru, uwezo na uadilifu ndani yake. (Ee Mungu nisaidie)

**KIAPO/KUKIRI KUWA MBUNGE (SENETI/BARAZA KUU LA KITAIFA)**

Mimi,……………………, nikiwa nimechaguliwa mwachama wa Seneti/Baraza Kuu la Kitaifa ninaapa (Kwa jina la Mwenyezi Mungu) (ninathibitisha kwa dhati) kwamba nitakuwa mwaminifu na mtiifu kwa Watu na Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatii, kuheshimu, kutetea, kulinda na kuhifadhi Katiba ya Jamhuri ya Kenya; na kwamba nitatekeleza majukumu yangu ya ubunge kwa uaminifu na uangalifu. (Ee Mungu nisaidie).

**KIAPO CHA SPIKA/NAIBU WA SPIKA WA SENETI/BARAZA KUULA KITAIFA**

Mimi ,……………….. , nikiwa nimechaguliwa kama Spika/ Naibu wa Spika wa Seneti/ Baraza Kuu la Kitaifa ninaapa kwamba(kwa jina la Mwenyezi Mungu)

Draft for approval

(nakubali kwa dhati) kwamba nitakuwa mwaminifu kwa watu na Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza kwa uaminifu na uangalifu kazi zangu kama Spika/Naibu wa Spika wa Seneti/Baraza Kuu la Kitaifa; kwamba nitatii, nitaheshimu, nitatea, nitahifadhi, nitalinda na kuitetea Katiba hii ya Jamhuri ya Kenya; na kwamba nitafanya haki kwa watu wote kulingana na Katiba hii ya Kenya na sheria na desturi za Bunge bila woga au upendeleo, upendo au chuki. (Ee Mungu nisaidie).

Draft for approval

**MPANGILIO WA NNE**

**(Kifungu cha 185 (2), 186 (1) na 187 (2)**

**MGAO WA MAJUKUMU KATI YA SERIKALI YA KITAIFA NA SERIKALI ZA KAUNTI**

**Sehemu ya 1 – Serikali ya Kitaifa**

1. Mashauri ya kigeni, sera ya kigeni, na biashara ya kimataifa.

2. Matumizi ya maji ya kimataifa na rasilimali za maji.

3. Uhamiaji na uraia.

4. Uhusiano kati ya dini na serikali.

5. Sera ya lugha na ukuzaji wa lugha rasmi na lugha za kiasili.

6. Ulinzi wa kitaifa na matumizi ya huduma za ulinzi za kitaifa..

7. Huduma za polisi , pamoja na—

   (a) Kuweka viwango vya kuajiri, mafunzo kwa polisi na matumizi ya huduma za polisi;

   (b) Sheria ya jinai; na

   (c) Huduma za Marekebisho.

8. Mahakama.

9. Sera ya kitaifa ya uchumi na mipango.

10. Sera ya fedha, sarafu, benki (pamoja na benki kuu) kuanzishwa pamoja na usimamizi wa shughuli za benki, bima na mashirika ya kifedha.

11. Takwimu za kitaifa na data kuhusu idadi ya watu, uchumi na jamii kwa jumla.

12. Haki miliki

13. Viwango vya utendakazi.

14. Ulinzi wa watumiaji, pamoja na viwango vya usalama wa kijamii na mipango ya kitaalamu ya kustaafu.

15. Sera ya Elimu, viwango, Mitalaa, mitihani, na utoaji wa hati za vyuo vikuu.

16. Vyuo Vikuu, taasisi za mafunzo ya kati na taasisi nyingine za utafiti na masomo ya juu na shule za msingi, elimu maalumu, shule za upili na vyuo vya elimu maalumu.

17. Ukuzaji wa michezo na elimu ya michezo.

18. Uchukuzi na mawasiliano, pamoja na, hasa—

Draft for approval

(a) Usafiri wa barabara;

(b) Ujenzi na matumizi ya barabara kuu za kitaifa

(c) Viwango vya ujenzi na uhifadhi wa barabara zingine za kaunti;

(d) Reli;

(e) Mifereji ya mabomba;

(f) Usafiri wa baharini;

(g) vyombo vya anga vinavyotumiwa na raia;

(h) Usafiri wa angani;

(i) Huduma za posta;

(j) Mawasiliano ya simu, redio na runinga na;

(k) matangazo ya redio na runinga.

19. Huduma ya kitaifa ya kazi za umma.

20. Sera ya nyumba.

21. Kanuni za kijumla za mipango ya ardhi na ushirikishaji wa mipango na kaunti.

22. Uhifadhi wa mazingira na maliasili kwa mpango wa kuanzisha mfumo wa maendeleo endelevu, pamoja na, hasa—

(a) Uvuvi, usasi na ukusanyaji;

(b) Ulinzi wa wanyama wa kufugwa na wanyama pori;

(c) Uhifadhi wa maji, kuhifadhi wa mabaki ya maji, uhandisi unaohusu maji na usalama wa mabwawa; na

(d) Sera ya kawi .

23. Hospitali za Kitaifa.

24. Usimamizi wa majanga.

25. Minara ya zamani ya kihistoria yenye umuhimu wa kitaifa.

26. Chaguzi za kitaifa.

28. Sera ya Afya.

29. Sera ya Kilimo.

30. Sera ya utatibu wa mifugo.

31. Sera ya kawi pamoja na nguvu za umeme, mtandao wa gesi, na usimamiaji wa kawi.

Draft for approval

32. Ujenzi wa utendakazi na usaidizi wa kiufundi katika kaunti

33. Uwekezaji wa umma.

34. Uwekaji dau wa kitaifa, makasino na aina mbalimbali za uchezaji kamari.

35. Sera ya utalii na maendeleo.

**Sehemu ya 2—Serikali za Kaunti**

Mamlaka na kazi za kaunti ni—

1. Kilimo, pamoja na-

    (a) Kilimo cha mimea na wanyama;

    (b) Viwanja vya kuuzia wanyama;

    (c) Vichinjio vya kauni;

    (d) Udhibiti wa magonjwa ya mimea na wanyama; na

    (e) Uvuvi.

2. Huduma za afya za kaunti pamoja na, hasa—

    (a) Vituo vya afya vya kaunti na maduka ya dawa;

    (b) huduma za magari ya wagonjwa;

    (c) Kuimarisha afya ya kimsingi;

    (d) Kutoa leseni na kusimamia shughulia za kuuza vyakula kwa umma;

    (e) Huduma za utabibu wa wanyama (isipokuwa usimamizi wa taaluma hii);

    (f) Makaburi, kumbi za matanga na tanuu za kuchomea maiti; na

    (g) Uondoaji taka, maeneo ya kutupa taka na utupaji taka.

3. Kudhibiti uchafuzi wa hewa, uchafuzi wa mazingira kupitia kelele, na usumbufu mwingine kwa umma na utangazaji nje ya makazi.

4. Shughuli za kitamaduni, burudani za umma na huduma za kufurahisha umma pamoja na—

    (a) Kucheza dau, kasino na njia nyingine za kamari;

    (b) mashindano ya mbio;

    (c) Utaoji leseni kwa pombe;

    (d) majumba ya Sinema;

Draft for approval

(e) maonyesho ya video na kukodisha;

(f) maktaba;

(g) makavazi;

(h) michezo na shughuli za kitamaduni na vifaa; na

(i) bustani za kaunti, fuo na nyenzo za burudani.

5. uchukuzi katika kaunti, pamoja na —

(a) barabara za kaunti;

(b) taa za barabarani;

(c) magari na uegeshaji;

(d) usafiri wa barabarani kwa umma ; na

(e) vivuko na bandari, isipokuwa usimamizi wa usafiri majini wa kitaifa na kimataifa na shughuli zinazohusiana na hizo.

6. Udhibiti na hali ya wanyama, pamoja na-

(a) kutoa leseni kwa mbwa; na

(b) Nyenzo za kuhifadhi, kutunza na kuzika wanyama.

7. Ustawishaji wa biashara na usimamizi, pamoja na—

(a) masoko;

(b) leseni za biashara (isipokuwa udhibiti wa taaluma hizo);

(c) usawa katika shughuli za kibiashara;

(d) utalii wa humu nchini; na

(e) vyama vya ushirika.

8. Mipango na maendeleo ya kaunti, pamoja na—

(a) takwimu;

(b) usoroveya na uchoraji ramani;

(c) mipaka na ujenzi wa nyua;

(d) makazi; na

(e) Uunganishaji na udhibiti wa nguvu za umeme na gesi.

9. Elimu ya chekechea, elimu, vyuo vya ufundi anuwai, vituo vya utengenezaji wa vyombo vya kinyumbani na nyenzo za utunzaji wa watoto.

Draft for approval

10. Utekelezwaji wa sera maalum za serikali ya kitaifa kuhusu maliasili na uhifadhi wa mazingira, pamoja na—

    (a) uhifadhi wa udongo na maji; na

    (b) misitu.

11. Huduma za kazi kwa umma katika kaunti pamoja na —

    (a) mfumo wa usimamizi wa maji ya tufani katika sehemu za majengo; na

    (b) huduma za maji na usafi.

12. huduma za kuzima moto, na usimamizi wa majanga

13. udhibiti wa dawa na ponografia.

14. kuhakikisha na kusimamia ushiriki wa jamii na sehemu za mashambani katika utawala wa viwango hivyo vya mashinani na kuzisaidia jamii pamoja na maeneo hayo kujenga uwezo wa kiusimamizi ili kuwezesha matumizi ya mamlaka na majukumu na kushiriki katika utawala wa mashinani.

Draft for approval

**MPANGILIO WA TANO**

**(Kifungu cha 261 cha (1))**

**SHERIA ZITAKAZOTUNGWA NA BUN**

| SURA NA KIFUNGU | MUDA ULIOWEKWA |
|---|---|
| **SURA YA PILI – JAMHURI** | |
| Sheria kuhusu utamaduni (Kifungu cha 11 (3)) | Miaka mitano |
| **SURA YA TATU – URAIA** | |
| Sheria kuhusu uraia (Kifungu cha 18) | Mwaka mmoja |
| **SURA YA NNE – SHERIA YA HAKI** | |
| Uhuru wa vyombo vya habari (Kifungu cha 34) | Miaka mitatu |
| Familia (Kifungu cha 45) | Miaka mitano |
| Ulinzi kwa watumiaji bidhaa (Kifungu cha 46) | Miaka minne |
| Haki katika mambo ya kiutawala (Kifungu cha 47) | Miaka minne |
| Haki ya kusikilizwa (Kifungu cha 50) | Miaka minne |
| Haki ya watu walio kizuizini, walioshikwa au waliofungiwa (Kifungu cha 51) | Miaka minne |
| Tume ya kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya (Kifungu cha 59) | Mwaka mmoja |
| **SURA YA TANO – ARDHI NA MAZINGIRA** | |
| Ardhi ya jamii (Kifungu cha 63) | Miaka mitano |
| Usimamizi wa matumizi ya ardhi na mali (Kifungu cha 66) | Miaka mitano |
| Sheria ya ardhi (Kifungu cha 68) | Miezi 18 |
| Maafikiano kuhusu maliasili (Kifungu cha 71) | Miaka mitano |
| Sheria kuhusu mazingira (Kifungu cha 72) | Miaka minne |
| **SURA YA SITA – UONGOZI NA MAADILI** | |
| Tume ya Maadili na kupambana na Ufisadi (Kifungu cha 79) | Mwaka mmoja |
| Sheria ya uongozi (Kifungu cha 80) | Miaka miwili |
| **SURA YA SABA – UWAKILISHI WA WATU** | |
| Sheria ya uchaguzi (Kifungu cha 82) | Mwaka mmoja |
| Mizozo ya kiuchaguzi (Kifungu cha 87) | Mwaka mmoja |
| Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (Kifungu cha 88) | Mwaka mmoja |
| Sheria ya vyama vya kisiasa (Kifungu cha 92) | Mwaka mmoja |

Draft for approval

| | |
|---|---|
| **SURA YA NANE – BUNGE** | |
| Kuimarisha uwakilishi wa jamii zilizotengwa (Kifungu cha 100) | Miaka mitano |
| Kuachwa wazi kwa afisi ya mbunge (Kifungu cha 103) | Mwaka mmoja |
| Haki ya kumwondoa mbunge (Kifungu cha 104) | Miaka miwili |
| Uamuzi wa masuala ya uanachama wa Bunge (Kifungu cha 105) | Miaka miwili |
| Haki ya kupeleka malalamiko kwa Bunge (Kifungu cha 119) | Miaka miwili |
| **SURA YA TISA – MAMLAKA YA UTAWALA** | |
| Mamlaka ya kusamehe (Kifungu cha 133) | Mwaka mmoja |
| Kuchukua mamlaka ya afisi ya Rais (Kifungu cha 141) | Miaka miwili |
| **SURA YA KUMI - MAHAKAMA** | |
| Utaratibu wa mahakama (Kifungu cha 162) | Mwaka mmoja |
| Kuondolewa afisini (Kifungu cha 168) | Mwaka mmoja |
| Mfuko wa Mahakama (Kifungu cha 173) | Miaka miwili |
| Ukaguzi wa majaji na mahakimu (Mpangilio wa sita sehemu ya 23) | Mwaka mmoja |
| **SURA YA KUMI NA MOJA – SERIKALI YA UGATUZI** | |
| Spika wa baraza la kaunti (Kifungu cha 178) | Mwaka mmoja |
| Sehemu za miji na majiji (Kifungu cha 183) | Mwaka mmoja |
| Usaidizi kwa serikali za kaunti (Kifungu cha 190) | Miaka mitatu |
| Kuondolewa kwa gavana wa kaunti (Kifungu cha 181) | Miezi kumi na minane |
| Kuachwa wazi kwa afisi ya mwanachama wa baraza la kaunti (Kifungu cha 194) | Miezi kumi na minane |
| Kushiriki kwa umma na mamlaka ya baraza la kaunti, mapendeleo na kinga | Miaka mitatu |
| Usawa wa kijinsia na tofauti za kijamii katika baraza la kaunti (Kifungu cha 197) | Miaka mitatu |
| Sheria ya kuanza kutumiwa kwa Sura ya kumi na moja (Kifungu cha 200 na mpangilio wa sita sehemu ya 15) | Miezi kumi na minane |

Draft for approval

| | |
|---|---|
| **SURA YA KUMI NA MBILI – FEDHA ZA UMMA** | |
| Mapato ya pesa kwa serikali za kaunti (Kifungu cha 207) | Miezi kumi na minane |
| Mfuko wa Dharura (Kifungu cha 208) | Mwaka mmoja |
| Udhamini wa mikopo na serikali ya kitaifa (Kifungu cha 213) | Mwaka mmoja |
| Usimamizi wa pesa (Kifungu cha 225) | Miaka miwili |
| Mahesabu na ukaguzi wa mashirika ya umma (Kifungu cha 226) | Miaka minne |
| Ununuzi wa bidhaa na huduma za umma (Kifungu cha 227) | Miaka minne |
| **SURA YA KUMI NA TATU – HUDUMA ZA UMMA** | |
| Maadili na kanuni za huduma za umma (Kifungu cha 232) | Miaka minne |
| **SURA YA KUMI NA NNE – USALAMA WA KITAIFA** | |
| Idara za usalama wa kitaifa (Kifungu cha 239) | Miaka miwili |
| Utawala wa huduma ya polisi ya kitaifa (Kifungu cha 245) | Miaka miwili |
| **KAULI YA JUMLA** | |
| Sheria nyingine yoyote itakayohitajiwa na Katiba hii | Miaka mitano |
| | |

Draft for approval

**MPANGILIO WA SITA**

**(Kifungu cha 262)**

**MASHARTI YA MPITO NA MATOKEO**

**Sehemu ya 1- Kwa ujumla**

**Ufasiri**

**1.** Katika Mpangilio huu, isipokuwa tu muktadha uonyeshe vinginevyo-

(a) " Tume ya Mipaka inamaanisha Tume Huru ya Muda ya Mipaka ;

(b) "Tume ya Uchaguzi" inamaamisha Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi ;

(c) "Katiba ya awali" inamaanisha Katiba iliyotumika kabla ya Katiba hii kutekelezwa.

**Kuahirisha masharti ya Katiba hii**

**2.** (1) Masharti yafuatayo ya Katiba hii yameahirishwa mpaka matangazo ya mwisho ya majibu yote ya uchaguzi mkuu wa kwanza wa Bunge chini ya

Katiba hii-

(a) Sura ya Saba, isipokuwa masharti ya sura hii yatahusu uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba hii;

(b) Sura ya Nane , isipokuwa masharti ya sura hii yanayohusiana na uchaguzi wa Baraza Kuu la Kitaifa na Seneti yatahusishwa katika uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba hii; na

(c) Vifungu vya 129 hadi 155 vya Sura ya Tisa, isipokuwa masharti ya Sura yanayohusiana na uchaguzi wa Rais, yatahusishwa katika uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba hii.

(2) Masharti ya Katiba hii yanayohusu serikali ya ugatuzi, kukiwemo kifungu cha 187, yamesimamishwa hadi tarehe ya uchaguzi wa kwanza wa mabaraza ya kaunti na magavana utakaofanywa chini ya Katiba hii.

(3) Licha ya ibara ndogo ya (2)-

(a) Uchaguzi wa mabaraza ya kaunti na magavana utafanywa kwa mujibu wa vifungu vya 177 na 180 vya Katiba hii; na

(b) Sheria zinazohusu serikali ya ugatuzi, zinazohitajika katika Mpangilio huu na katika Sura za Kumi na Moja na Kumi Mbili za Katiba hii, zitatungwa katika muda uliowekwa katika Mpangilio wa Tano.

Draft for approval

**Kuongezwa kwa muda wa kutumia masharti ya Katiba ya awali**

**3.** (1) Hadi pale Bunge litakapopitisha Sheria inayotarajiwa katika Vifungu vya 15 na 18, sehemu ya 93 ya Katiba ya awali inaendelea kutumika.

(2) Sehemu za 30 hadi 40, 43 hadi 46, 48 hadi 58 za Katiba ya awali, masharti ya Katiba ya awali kuhusu mamlaka ya serikali, na Mwafaka wa Kitaifa na Sheria ya Maridhiano, ya mwaka wa 2008 (Na. 4 ya 2008) zitaendelea kutumika hadi uchaguzi mkuu wa kwanza utakapofanywa chini ya Katiba hii, lakini masharti ya Katiba hii kuhusu mfumo wa uchaguzi, ustahili wa mtu katika uchaguzi na utaratibu wa uchaguzi utatumika katika uchaguzi huo.

(3) Hadi pale ambapo Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa inayorejelewa katika Kifungu cha 246 imeundwa, sehemu ya 108 (2) ya Katiba ya awali itatumika katika uteuzi wa kazi, masuala ya nidhamu na kuachishwa kazi kwa watu katika Huduma za Polisi za Kitaifa.

**Kamati Teule ya Bunge**

**4.** Kutakuwa na kamati teule ya Baraza la Kitaifa itakayojulikana kama Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Katiba itakayowajibikia kusimamia utekelezaji wa Katiba hii, na ambayo, miongoni mwa vitu vingine-

(a) Itapokea ripoti za kila mara kutoka kwa Tume ya Utekelezaji wa Katiba ikiwa ni pamoja na ripoti kuhusu-

(i) Kuandaa sheria inayohitajika na Katiba hii na changamoto zozote kuihusu;

(ii) Hatua za kuunda tume mpya;

(iii) Hatua ya kuunda miundo misingi inayohitajika kutekeleza shughuli za kila kaunti kwa njia mwafaka pamoja na hatua za kutambua afisi na mabaraza pamoja na kuajiri na kuhamisha wafanyikazi.

(iv) Ugatuzi wa mamlaka na majukumu kwa kaunti chini ya sheria iliyozingatiwa katika sehemu ya 15 ya Mpangilio huu; na

(v) vizuizi vyovyote katika hatua za utekelezaji wa Katiba hii.

(b) Kushirikiana na Mwanasheria Mkuu, Tume ya Utekelezaji wa Katiba na kamati husika za Bunge kuhakikisha sheria inayohitajiwa na Katiba hii imewasilishwa na kupitishwa kwa wakati ufaao; na

a) Kuchukua hatua mwafaka za ripoti ikiwa ni pamoja na kutatua matatizo yoyote katika utekelezaji wa Katiba hii.

**Tume ya Utekelezaji wa Katiba**

**5.** (1) Tume ya Utekelezaji wa Katiba imeundwa.

(2) Tume inahusisha-

Draft for approval

(a) Mwenyekiti; na

(b) Wanachama wengine wanane.

(3) Wanachama wa Tume-

(a) ni pamoja na watu wenye tajriba katika uongozi wa umma, haki za binadamu na serikali; na

(b) haitahusisha mtu yeyote aliyekuwa mwanachama katika Tume ya wataalamu iliyoteuliwa chini ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, 2008.

(4) Vifungu vya 248 na 254 vinahusu Tume hii.

(5) Baada ya Tume ya Ugavi wa Mapato kuundwa, Tume ya Utekelezaji wa Katiba itatuma taarifa za mikutano kwa Tume hiyo , na mwanachama wa Tume ya Ugavi wa Mapato ataruhusiwa kuhudhuria na kushiriki katika mikutano yoyote kama hiyo, lakini hatapiga kura.

(6) Majukumu ya Tume hii yatakuwa-

(a) kuchunguza, kusimamia na kuhimiza utungaji wa sheria na hatua zinazohitajika katika kutekeleza Katiba hii;

(b) kushirikiana na Mwanasheria Mkuu na Tume ya Marekebisho ya Sheria ya Kenya katika kutayarisha sheria itakayowasilishwa Bungeni ambayo itahitajika ili kutekeleza katiba hii; na

(c) kutoa ripoti za kila mara kwa Tume ya Kusimamia Utekelezaji wa Katiba kuhusu:-

(i) hatua katika utekelezaji wa katika; na

(ii) vizuizi vyovyote katika utekelezaji wake; na

(d) kufanya kazi na kila Tume ya kikatiba kuhakikisha kuwa nia ya Katiba hii imeheshimiwa.

(7) Tume ya Utekelezaji wa Katiba hii itavunjwa miaka mitano tangu kuundwa kwake au baada ya kutekelezwa kikamilifu kwa Katiba hii kama itakavyoamuliwa na Bunge, yoyote ijayo mwanzo, lakini Baraza Kuu la Kitaifa, linaweza kufanya uamuzi wa kuiongezea muda.

**Sehemu ya 2 : Wajibu, Sheria na haki zilizopo**

**Haki, Majukumu na Wajibu wa Serikali**

**6.** Isipokuwa pale ambapo Katiba hii inaeleza vinginevyo, haki zote na wajibu wa Serikali na Jamhuri zilizoko na zinazochukua nafasi mara tu kabla ya tarehe ya utekelezaji wa Katiba hii, zitaendelea kama haki na wajibu wa serikali ya kitaifa au Jamhuri chini ya Katiba hii.

Draft for approval

**Sheria Zilizopo**

**7.** (1) Sheria zote zinazotumika kabla ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii zitaendelea kuwepo na zitafanyiwa marekebisho muhimu ili ziweze kuafikiana na Katiba hii.

(2) Iwapo, kwa mujibu wa suala lolote-

(a) Sheria iliyokuwa ikitumika mara tu kabla ya tarehe ya kutekelezwa inaipa jukumu idara fulani ya serikali au afisi ya umma; au

(b) Sharti la Katiba hii linalotumika linaipa majukumu idara tofauti ya serikali au afisa wa umma, Masharti ya Katiba hii ndiyo yatakayopewa umuhimu.

Draft for approval

**Umiliki wa ardhi uliopo na makubaliano kuhusu maliasili**

**8.** (1) Katika tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii ardhi yoyote inayomilikiwa na mtu ambaye si raia wa Kenya bila masharti litarejeshwa kwa Jamhuri ya Kenya ili kulihifadhi kwa niaba ya watu wa Kenya, na Serikali itampa mtu huyo kipindi cha miaka tisini na tisa kukodi shamba hilo kwa kulipa kiasi kidogo cha kodi.

(2) Katika tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, mtu yeyote asiye raia wa Kenya anayemiliki shamba kwa mkataba wa kupangisha uliozidi miaka tisini na tisa, mkataba huo utabadilishwa na kuwa wa miaka tisini na tisa.

(3) Masharti ya Kifungu cha 71 hayataanza kutekelezwa hadi sheria inayorejelewa katika Kifungu hicho itungwe.

**Sehemu ya 3 – Serikali ya Kitaifa**

**Uchaguzi na Uchaguzi mdogo**

**9.** (1) Uchaguzi wa kwanza wa Rais, Baraza Kuu la Kitaifa, Seneti, mabaraza ya kaunti na magavana wa kaunti chini ya Katiba hii utafanywa wakati mmoja, katika muda wa siku sitini baada ya kuvunjwa kwa Baraza Kuu la Kitaifa kipindi chake kitakapokamilika.

(2) Licha ya ibara ndogo ya (1), iwapo muungano uliobuniwa chini ya Muafaka wa Maridhiano umevunjwa na uchaguzi mkuu kufanywa kabla ya 2012, uchaguzi wa kwanza wa mabaraza ya kaunti na magavana utafanywa mwaka huo wa 2012.

**Baraza la Kitaifa**

**10.** Baraza la Kitaifa lilipo kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii litaendelea kama Baraza Kuu la Kitaifa kwa minajili ya Katiba hii kwa muda uliosalia.

**Seneti**

**11.** (1) Hadi pale ambapo Seneti ya kwanza itachaguliwa chini ya Katiba hii-

(a) majukumu ya Seneti yatatekelezwa na Baraza Kuu la Kitaifa; na

(b) jukumu lolote au mamlaka yoyote yanayohitajika kutekelezwa kwa pamoja na viwango vyote viwili vya Bunge au kimoja baada ya kingine, yatatekelezwa na Baraza Kuu la Kitaifa.

(2) Jukumu lolote au mamlaka ya Seneti, iwapo yatatekelezwa na Baraza Kuu la Kitaifa kabla ya tarehe inayotajwa katika ibara ndogo ya (1) , yatachukuliwa kuwa yalitekelezwa kikamilifu na Seneti.

**Mamlaka Makuu ya Utawala**

**12.** (1) Watu wanaoshikilia mamlaka ya Rais na Waziri Mkuu, kabla tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, wataendelea kuhudumu kama Rais na Waziri Mkuu mtawalia, kwa mujibu wa Katiba ya awali katika Sheria ya mwaka wa 2008 ya Muafaka wa Kitaifa na Maridhiano hadi uchaguzi mkuu wa kwanza ufanyike chini ya Katiba hii, au waondoke afisini kwa mujibu wa Katiba ya awali na Muafaka wa Kitaifa na Maridhiano.

(2) Watu wanaoshikilia afisi ya Makamu wa Rais na Naibu-Waziri Mkuu au wanaoshikilia wadhifa katika Baraza la Mawaziri au Waziri Msaidizi mara tu kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, wataendelea kuhudumu kwa mujibu wa Katiba ya awali mpaka uchaguzi mkuu wa kwanza ufanywe chini ya Katiba hii, ila tu waondoke au kuondolewa afisini kwa mujibu wa Katiba ya awali na Sheria ya mwaka wa 2008 ya Muafaka wa Kitaifa na Mariadhiano.

(3) Mtu aliyechaguliwa Rais kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii hatagombea uchaguzi wa urais chini ya Katiba hii.

**Kiapo cha uaminifu kwa Katiba hii**

**13.** Katika tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, Rais na afisa yeyote wa Serikali, au mtu yeyote ambaye kabla ya tarehe ya kutekelezwa , alikuwa amekula kiapo ama kukubali kama ilivyo katika kiapo cha uaminifu ili kuchukua afisi chini ya Katiba ya awali, au anatakiwa kula kiapo au kukubali kuchukua afisi chini ya Katiba hii, ataapa na kukubali chini ya Katiba hii.

**Sehemu ya 4- Serikali ya Ugatuzi**

**Utekelezaji wa masharti yanayohusu serikali ya ugatuzi.**

**14.** (1) Sheria zinazotajwa katika ibara ya 2 (3) (b) na ibara ya 15 zinaweza kutekelezwa iwapo Tume ya Utekelezaji wa Katiba hii na, iwapo pia Tume ya Ugavi wa Mapato imeundwa, zote mbili zimeshauriwa na mapendekezo yoyote ya Tume hizi

Draft for approval

yamekubaliwa na Bunge.

(2) Tume hizi zitapewa angalau siku thelathini kuchunguza sheria chini ya ibara ndogo ya (1).

(3) Ibara ndogo za (1) na (2) zitaisha wakati Tume ya Utekelezaji wa Katiba itakapovunjwa.

**Masharti ya ugatuzi wa majukumu kuidhinishwa na Sheria ya Bunge**

**15.** (1) Kwa kuweka sheria, Bunge litatoa mwongozo wa kuhamisha kwa awamu, kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu, tokea wakati wa uchaguzi wa kwanza wa mabaraza ya kaunti, tokea serikali ya kitaifa hadi serikali za kaunti, majukumu yaliyopewa serikali hizo chini ya Kifungu cha 185.

(2) Sheria inayotajwa katika ibara ndogo ya (1)-

(a) kutoa mwongozo wa jinsi serikali ya kitaifa-

(i) itakavyosaidia katika ugatuzi wa mamlaka;

(ii) itakavyosaidia serikali za kaunti kujenga uwezo wao wa kujitawala na kutoa huduma zinazostahili kutoa; na

(iii)itakavyozisaidia serikali za kaunti;

(b) kuweka masharti yatakoyotimizwa kabla ya majukumu fulani kugatuliwa kwenda kwa serikali za kaunti, ili kuhakikisha kuwa serikali hizo hazipewi majukumu ambayo haziwezi kuyatekeleza; na

(c) kuruhusu ugatuzi wa mamlaka ili kuhakikisha kwamba majukumu yanagatuliwa kwa haraka kwa kaunti zile ambazo zina uwezo wa kuyatekeleza na kwamba pasiwe na kaunti ambayo imepewa majukumu isiyoweza kutekeleza; na

(d) kutoa utaratibu utakaohakikisha kwamba Tume ya Utekelezaji wa Katiba itatekeleza wajibu wake wa kufuatilia utekelezaji wa mfumo wa ugatuzi sawasawa.

**Ugavi wa Mapato**

**16.** Licha ya Kifungu cha 217 (1), vigezo vya kwanza na vya pili vya misingi ya ugavi wa mapato miongoni mwa kaunti vitafanywa katika kipindi cha baada ya kila miaka mitatu, badala ya baada ya miaka mitano kama inavyoonyeshwa katika Kifungu hicho.

**Utawala wa Mkoa**.

**17.** Katika kipindi cha miaka mitano baada ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, serikali ya kitaifa itafanya marekebisho katika mfumo wa utawala ulio maarufu kwa

Draft for approval

jina la utawala wa mkoa, ili uafikiane na kuheshimu mfumo wa serikali ya ugatuzi ulioundwa chini ya Katiba hii.

**Mabaraza ya Miji**

**18.** Mabaraza yote ya miji yaliyoundwa chini ya Sheria ya Mabaraza ya Miji ((Kifungu cha 265) yaliyopo mara tu kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, yataendelea kuwepo lakini kwa kutegemea sheria yoyote itakayoweza kuundwa.

**Sehemu ya 5 – Utekelezaji wa Haki.**

**Kanuni za Utekelezaji wa Haki za Msingi**

**19.** Hadi Jaji Mkuu atakapoweka sheria zinazorejelewa katika Kifungu cha 22, kanuni za utekelezaji wa haki za msingi na uhuru chini ya ibara ya 84 (6) ya Katiba ya awali zitaendelea kutumika kwa kufanyiwa marekebisho muhimu ili ziafikiane na Kifungu cha 22.

**Tume ya Huduma za Mahakama**

**20.** (1) Tume ya Huduma za Mahakama itateuliwa katika siku sitini baada ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii , na Tume hii itachukuliwa kuwa imeundwa chini ya Katiba hii licha ya kwamba huenda kukawa na nafasi wazi katika uanachama wake kwa kuwa idara yoyote inayowateua au kuwachagua wanachama haitakuwa imefanya hivyo.

(2) Licha ya ibara ndogo ya (1), Tume ya Huduma za Mahakama haitatekeleza majukumu yake hadi wanachama wasiopungua watano wawe wameteuliwa.

(3) Ili kuhakikisha kuna mwendelezo katika shughuli za Tume ya Huduma za Mahakama, licha ya Kifungu cha 171 (4), wakati Tume itakapoundwa kwa mara ya kwanza, wanachama wafuatao watateuliwa kuhudumu kwa miaka mitatu pekee-

(a) Jaji wa Mahakama ya Rufani atakayeteuliwa chini ya Kifungu cha 171 (4) (c );

(b) Jaji wa Mahakama ya Juu atakayeteuliwa chini ya Kifungu cha 171 (4) (d);

(c) Mmoja wa mawakili atakayeteuliwa chini ya Kifungu cha 171 (4) (f), atakayeteuliwa na idara inayosimamia shughuli za taaluma ya mawakili; na

(d) mmoja wa wanachama atakayeteuliwa na Rais chini ya Kifungu cha 171 (4) (h); atakayetambuliwa na Rais.

(4) Hadi Tume ya Huduma za Umma inayorejelewa katika Kifungu cha 233 itakapoundwa, mtu anayeteuliwa na Tume ya Huduma za Umma chini ya ibara ya 106 ya Katiba ya awali atahudumu katika Tume ya Huduma za Mahakama lakini, wakati Tume mpya ya Huduma za Umma itakapoundwa, mtu huyo ataacha kuwa mwanachama wa Tume ya Huduma za Mahakama na Tume hiyo mpya ya Huduma za Umma itamteua mtu atakayehudumu katika Tume ya Huduma za Mahakama.

Draft for approval

**Kuundwa kwa Mahakama Kuu**

**21.** (1) Kuundwa kwa Mahakama Kuu na kuteuliwa kwa majaji wa Mahakama hii kutakamilishwa katika muda wa mwaka mmoja kutoka tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii.

(2) Hadi pale ambapo Mahakama Kuu itaundwa, Mahakama ya Rufani itayashughulikia masuala yaliyopewa Mahakama Kuu.

**Kesi zilizo Mahakamani na masuala ambayo hayajakamilishwa**

**22.** Kesi zote zilizo katika mahakama yoyote zitaendelea kusikilizwa na uamuzi kutolewa na mahakama husika au mahakama ya kiwango sawa iliyoundwa chini ya Katiba hii au itakavyoelekezwa na Jaji Mkuu au Msajili wa Mahakama ya Juu.

**Majaji**

**23.** (1) Katika mwaka mmoja baada ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, Bunge litatunga sheria itakayotekelezwa licha ya Kifungu cha 160, 167 na 168, ambayo itaweka mikakati na utaratibu wa kuchunguza, katika muda utakaoamuliwa katika sheria hiyo, ustahili wa majaji na mahakimu wote waliokuwa afisini tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hiyo kuendelea kuhudumu kwa mujibu wa maadili na kanuni zilizo katika Vifungu vya 10 na 159.

(2) Kuondolewa au utaratibu utakaopelekea kuondolewa kwa jaji kutoka afisini kwa misingi ya utekelezaji wa sheria inayorejelewa katika ibara ndogo ya (1) hakutapingwa au kuchunguzwa upya, na mahakama yoyote.

**Jaji Mkuu**

**24.** (1) Jaji Mkuu aliye afisini mara tu kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, ataondoka afisini katika kipindi cha miezi sita tangu tarehe ya kutekelezwa na anaweza kuchagua ama-

(a) Kustaafu kutoka katika idara ya mahakama; au

(b) Kwa mujibu wa utaratibu wa kuchunguza chini ya ibara ya 23, kuendelea kuhudumu katika Mahakama ya Rufani.

(2) Jaji Mkuu mpya atateuliwa na Rais, kulingana na Sheria ya Muafaka wa Kitaifa na Maridhiano, na baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na kuidhinishwa na Baraza.

(3) Ibara ndogo ya (2) pia itatumika iwapo kuna nafasi za kazi zaidi katika afisi ya Jaji Mkuu kabla ya uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba hii.

Draft for approval

**Sehemu ya 6 – Tume na Afisi**

**Tume za Kikatiba**

**25.** (1) Tume ya Utekelezaji wa Katiba na Tume ya Ugavi wa Mapato zitaundwa katika siku tisini baada ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii.

(2) Tume ya Mishahara na Kuzawidi itaundwa katika miezi tisa baada ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii.

(3) Hadi pale ambapo sheria inayorejelewa katika Kifungu cha 256 itekelezwe, watu watakaoteuliwa kama wanachama au mwenyekiti wa Tume ya Mishahara na Kuzawidi watateuliwa na Rais, kutegemea Sheria ya Muafaka wa Kitaifa na Maridhiano, na baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na kuidhinishwa na Baraza Kuu la Kitaifa.

**Tume ya Haki za Binadamu na Usawa**

26. (1) Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Usawa walioteuliwa chini ya Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu ya Kenya ya mwaka wa 2002 ( Na. 9 ya 2002) na makamishna wa Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Maendeleo iliyoteuliwa chini ya Sheria ya mwaka wa 2003 (Na. 13 ya 2003), mbali na Makatibu Wakuu na Mwanasheria Mkuu au mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu, watakuwa wanachama wa Tume ya Haki za Binadamu na Usawa wa kudumu lakini kila mmoja wao atabakia na kanuni zake za utendakazi wakati wa kutekelezwa kwa Katiba hii.

(2) Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu atakuwa mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Usawa kwa kipindi cha kudumu cha wadhifa wake naye mwenyekiti wa Tume ya Jinsia na Maendeleo atakuwa Naibu – Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Usawa kwa kipindi cha kudumu kama vile mwenyekiti katika wadhifa wake.

Draft for approval

**Tume Huru ya Muda ya Mipaka**

**27.** (1) Tume ya Mipaka iliyobuniwa chini ya Katiba ya awali itaendelea kuhudumu kama ilivyoundwa katika Katiba hiyo na kwa masharti ya ibara za 41 B na 41 C lakini-

(a) Haitaweka mipaka ya kaunti zilizoundwa chini ya Katiba hii;

(b) Itaweka mipaka ya maeneo bunge na wadi ikitumia vigezo vilivyotajwa katika Katiba hii; na

(c)Wanachama wa Tume hii wataongozwa na Sura ya Saba ya Katiba hii.

(2) Yanayohitajika katika Kifungu cha 89 (2) kwamba uchunguzi upya wa mipaka ya maeneo bunge na wadi ukamilishwe angalau miezi kumi na miwili kabla ya uchaguzi mkuu hayatahusiana na uchunguzi upya wa mipaka kabla ya uchaguzi wa kwanza chini ya Katiba hii.

(3) Tume ya Mipaka itahakikisha kuwa uchunguzi upya wa kwanza wa mipaka

ya maeneo bunge chini ya Katiba hii hautasababisha kupotea kwa eneo bunge lililokuwepo wakati wa tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii.

**Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.**

**28.** (1) Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi iliyoundwa chini ya ibara ya 41 ya Katiba ya awali itaendelea kuhudumu chini ya masharti ya Katiba hiyo kwa kipindi chake cha kudumu au hadi Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itakayoundwa chini ya Katiba hii iundwe, yoyote itakayokuja baadaye.

(2) Wakati wanachama wa Tume ya Uchaguzi na Mipaka watakapoteuliwa, haja ya mwendelezo na kuhifadhi ujuzi na tajiriba itazingatiwa.

**Uteuzi Mpya**

**29.** (1) Utaratibu wa uteuzi wa watu wa kujaza nafasi zitakazopatikana kutokana na kutekelezwa kwa Katiba hii, utaanza tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hiyo na kukamilika katika kipindi cha mwaka mmoja.

(2) Isipokuwa pale ambapo Mpangilio huu ueleze kinyume, wakati Katiba hii itakapohitaji uteuzi ambao hauna budi kufanywa na Rais na kuidhinishwa na Baraza Kuu la Kitaifa, hadi baada ya uchaguzi wa kwanza chini ya Katiba hii, kwa mujibu wa Sheria ya Muafaka wa Kitaifa na Maridhiano, Rais atamteua mtu baada ya kushauriana na Waziri Mkuu kwa idhini ya Baraza Kuu la Kitaifa

**Sehemu ya 6 – Masuala ya Ziada**

**Uraia Kwa Kuzaliwa**

**30.** Raia wa Kenya ni raia kwa kuzaliwa iwapo-

(1) amepata uraia chini ya kifungu cha 87 au 88 (1) cha Katiba ya awali; au

(2) angepata uraia kama kifungu cha 87 (2) kingesomwa:

“ Kila mtu ambaye alizaliwa nje ya Kenya, na mnamo tarehe 11-Disemba, 1963 ni raia wa Uingereza na Koloni zake au mtu aliyepata ulinzi wa Uingereza atakuwa, iwapo mamake au babake atakuwa , au angekuwa lakini kwa sababu ya kifo cha mmoja au wote wamekuwa, raia wa Kenya kwa sababu ya ibara ndogo ya (1), atakuwa raia wa Kenya mnamo tarehe 12-Disemba, 1963.”

**Afisi zilizoko**

**31.** (1) Isipokuwa Mpangilio huu uonyeshe vinginevyo, mtu ambaye mara tu kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii alikuwa anahudumu au anashikilia afisi kwa muda katika afisi iliyoundwa na Katiba ya awali, kufikia tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii ataendelea kuhudumu au kushikilia afisi hiyo chini ya Katiba hii kwa muda wote, iwapo kuna kipindi chochote kilichosalia, cha mtu huyo.

Draft for approval

(2) Kwa mujibu wa ibara ndogo ya (7) na ibara ya 24, mtu ambaye mara tu kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii alikuwa na afisi au alikuwa anashikilia afisi ya umma iliyoundwa na sheria, ambayo bado inaafikiana na Katiba hii, ataendelea kuhudumu katika afisi hiyo au kuishikilia kana kwamba amefanyiwa uteuzi chini ya Katiba hii.

(3) Masharti ya sehemu hii hayataathiri mamlaka aliyopewa mtu yeyote au wajibu chini ya Katiba hii au sheria ya kuvunjilia mbali afisi au kumwondoa mtu kutoka katika afisi inayorejelewa katika ibara ndogo ya (2).

(4) Kama mtu ameondoka katika afisi ambayo alikuwa anahudumu kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, na ofisi hiyo ipo au imeundwa chini ya Katiba hii, mtu huyo anaweza, kama amehitimu, kuteuliwa upya, kuchaguliwa, au kuteuliwa kuhudumu katika afisi hiyo kwa mujibu wa Katiba hii, isipokuwa pale ambapo Katiba hii imeonyesha kinyume.

(5) Majukumu ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma yatatekelezwa na Mwanasheria Mkuu mpaka Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma ateuliwe chini ya Katiba hii.

(6) Majukumu ya Msimamizi wa Bajeti yatatekelezwa na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu hadi Msimamizi wa Bajeti atakapoteuliwa chini ya Katiba hii.

(7) Licha ya ibara ndogo ya (1), Mwanasheria Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu wataendelea kuhudumu afisini kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili baada ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, na uteuzi utakaofuata katika afisi hizi utakuwa chini ya Katiba hii.

**Malipo ya uzeeni, bahashishi na Marupurupu Mengine**

**32.** Sheria inayohusu malipo ya uzeeni kwa mujibu wa maafisa wa afisi za kikatiba chini ya Katiba ya awali ama itakuwa sheria iliyotumika wakati marupurupu hayo yalitolewa au tarehe nyingine ya baadaye ambayo haitamwathiri vibaya mtu huyo.

**Urithi wa taasisi, ofisi, mali na madeni**

**33.** Afisi au taasisi ambayo imeundwa chini ya Katiba hii ndiyo mrithi wa kisheria wa afisi au taasisi iliyokuwepo, ambayo iliundwa chini ya Katiba ya awali au Sheria ya Bunge iliyokuwa ikifanya kazi kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii, ikiwa itatambuliwa kwa jina lile au itapewa jina jipya.

**Fedha**

**34.** Hakuna chochote katika Kifungu cha 231 (4) kinochoathiri uhalali wa sarafu na noti zilizotolewa kabla ya tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii.

Draft for approval